**24 JUNI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Hamsini na Moja – Tarehe 24 Juni, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali; Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

Na. 445

**Hitaji la Gari la kubeba Wagonjwa – Simanjiro**

**MHE. REGINA N. QWARAY** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka Gari la kubebea Wagonjwa katika Wilaya ya Simanjiro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 itanunua magari 195 ya kubebea wagonjwa ambayo yatapelekwa kwenye halmashauri 184 nchini kote ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwakuwa Wilaya ya Simanjiro ni miongoni mwa Halmashauri ambazo jiografia yake ni ngumu sana lakini nae neo kubwa sana.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya Halmashauri hii kupewa magari mawili ili walau kuokoa maisha ya wananchi wengi wanaofuata huduma ya afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Simanjiro pamoja na kwamba vituo vingi vya afya katika tarafa zipo mbali sana na Halmashauri husika kufikia katika hospitali ya Wilaya;

Je, Serikali haioni haya kuna Kituo cha Afya cha Terrat kipatiwa gari la wagonjwa ili wananchi wale wanapozidiwa wapate huduma ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ina Halmashauri kubwa lakini ina jiografia ambayo ina changamoto maeneo kadhaa. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba magari haya yanayonunuliwa ni magari 195 *plus,* lakini tuna Halmashauri 184 yale magari mengine yanayozidi 184 tutakwenda kufanya tathmini na kuona vigezo hivyo ikiwemo ukubwa wa Jiographia pamoja na idadi ya watu. Kwa hiyo tumelichukua hilo, tutafanya tathmini kwa uwezekano wa kupata gari zaidi ya moja kwenye Halmashauri ya Simanjiro kikiwepo Kituo hiki cha Afya cha Terrat, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Getere.

Na. 446

**Ufunguzi wa Hospitali ya Halmashauri ya *Bunda DC* na Kituo cha Afya Mugeta**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza: -

Je, ni lini Hospitali ya Halmashauri ya *Bunda DC* na Kituo cha Afya Mugeta vitafunguliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ilianza kutoa Huduma za Wagonjwa wa nje *(OPD)*, Chanjo na Huduma ya Mama na Mtoto *(RCH)* tangu mwezi Julai, 2020. Aidha, Kituo cha Afya Mugeta kilishaanza kutoa huduma ikiwa ni pamoja na huduma za upasuaji tangu mwezi Julai 2020, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba wakati fulani tupate majibu angalau mtusaidie meza kwenye jambo kama hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Bunda ina vitanda vitatu tu. Haina mfumo wa umeme, ni jengo moja linayo, haina mfumo wa maji, ina waganga watatu tu, haina dawa, hailazi, zijawahi kuona hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ambayo rufaa yake inaenda zahanati, sijawahi kuona, ha yani maajabu ya dunia.

Je, ni lini sasa Serikali itafanya ufanisi wa kutosha kwenye hosptali hii ili ifanye kazi vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wakati tunajenga vituo vya afya 2017/2018 tuliambiwa kwamba vile vituo tumepewa milioni mia nne, milioni mia tatu zitakuja kuleta vifaa kwenye vituo vya afya. Sasa Kituo cha Afya Mgeta hakina jokofu. Miaka mingi sana watu wanahangaika sana kupeleka maiti *mortuary* Musoma, umbali wa kilometa takriban 400.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka jokofu kwenye Kituo cha Afya Mgeta na *ambulance,* gari la wagonjwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere Mbunge wa Jimbo la Bunda Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajenga hosptiali za halmashauri nchini kote. Safari ni hatua; tumeanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Bunda Vijijini, na Halmashauri hii imepokea bilioni tatu na milioni mia moja, fedha nyingi kuliko Halmashauri nyingi ambazo zimepokea. Kwa hiyo naomba kwanza Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba Serikali imepeleka fedha nyingi sana kwenye hospitali yake; bilioni tatu na milioni mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba haina vifaa tiba vya kutosha, haina watumishi wa kutosha lakini pia inahitaji kupewa gari la wagonjwa, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunakwenda kwa hatua. Kuna hatua ya ukamilishaji wa ujenzi, tumeanza kutoa huduma za *OPD,* lakini tunakwenda sasa kupeleka vifaa tiba; na ndiyo maana mwaka ujao wa fedha tumetenga bilioni 69.95 kwa ajili ya vifaa tiba kwenye hospitali zilizokamilika ikiwepo Hospitali hii ya Bunda Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kituo cha Afya cha Mugeta kukosa *ambulance* lakini pia vifaa tiba na jokofu la *mortuary* naomba tulichukue hili na Serikali tuone namna ya kufanya kupata fedha ili tuweze kupeleka huduma hizo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Husna.

Na. 447

**Ruzuku ya ukarabati wa miradi ya maji**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza kutoa ruzuku ya ukarabati wa miradi ya maji kama inavyofanya kwa miradi ya barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina utaratibu wa kila mwaka wa fedha kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miradi ya maji ili iendelee kutoa huduma iliyokusudiwa mijini na vijijini. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 miradi 181 imekarabatiwa na katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali itaendelea na ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali tumeshuhudia miradi ya maji vijijini haikarabatiwi hadi inapoharibika na muda mwingine inakaa muda mrefu haitoi huduma;

Je, ni lini sasa Serikali itaweka fedha kwa ajili ya kukarabati hiyo miradi badala ya kusubiri iharibike kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna utaratibu wa wale vibarua *(technicians)* wanaokarabati miradi ya maji vijijini wanalipwa na Kamati za Maji, jambo ambalo limekuwa ni mzigo mzito kwa wananchi vijijini;

Je, ni lini sasa Serikali itawaajiri hawa *technicians* wawe wanalipwa na Serikali badala ya kulipwa na Kamati za Huduma za Maji Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Husna Sekoboko kama ifautavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari, hata kwenye bajeti ambayo tumeipitisha hapa ndani tuna fungu la fedha kwa ajili ya ukarabati wa miradi. Hivyo hapa tutaendelea kufuatilia mikoa yote na wilaya zote ili kuhakikisha watendaji wetu wanatimiza majukumu yao. Kama ni fedha za kuajiri *technicians* tayari Wizara tumetenga. Hii ni moja ya mikakati ambayo Wizara imeendelea nayo. Tuna Chuo chetu cha Maji pale Dar es Salaam, tayari tunazalisha vijana wengi sana na tayari Mheshimiwa Waziri ameagiza wale vijana waweze kutumika. Aidha wale vijana wameshanza kupelekwa maeneo mbalimbali. Kwa Mkoa wa Tanga anakotoka Mheshimiwa Mbunge tutafuatilia kuona kwamba napo wanakwenda kupelekwa kwa ajili ya kukarabati miradi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Tuna mradi unaoendelea wa kujenga

pale Hai, mradi wa Kikafu kwenda Bomang'ombe na Serikali tayari imeshatenga fedha; na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais ametupa bilioni 3.39 lakini yule Mkandarasi anasuasua na tayari Mwenge ulimpa siku 14 amalize mradi ule.

Je, ni lini sasa Serikali itamsukuma Mkandarasi amalize kazi hii ya maji ili watu wa Hai waweze kupata maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mafuwe kama ifautavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kupokea shukrani anafahamu namna tunavyoweza kushirikiana na anafahamu Mheshimiwa Rais amepeleka bilioni za fedha pale zaidi ya bilioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mkandarasi hili ni suala dogo, tutalifuatilia kwa karibu na kuhakikisha anatimiza majukumu yake kulingana na mkataba ambao tumesainiana naye. Hili nitalifuatilia mimi mwenyewe Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Kiswaga.

Na. 448

**Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha Lami**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza: -

Je, ni lini barabara ya kwenda Makumbusho ya Mkwawa itajengwa kwa kiwango cha lami na kukarabati jengo la Chifu Adam Sapi Mkwawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, Wizara itaendelea kushirikiana na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(TARURA)* Mkoa wa Iringa, kuitunza na kuifanyia ukarabati barabara hiyo ili iweze kupitika kwa vipindi vyote. Aidha, jengo aliloishi Chifu Adam Sapi Mkwawa lipo nje ya mipaka ya hifadhi ya Kituo cha Makumbusho ya Kalenga yapata kiasi cha mita 250 na linaendelea kutumiwa na wanafamilia. Hivyo, Wizara itaendelea kushirikiana na wana familia kuona namna nzuri ya kulikarabati jengo hilo la kihistoria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa majibu haya ya Serikali, lakini kuhusiana na ukarabati wa jengo la Chifu Adam Sapi Mkwawa Rais wa awamu ya nne aliagiza ufanyiwe tathmini na likarabatiwe, kwa hiyo ningetegemea kumbukumbu hizi muwe nazo. Lakini pili kuhusiana na hii barabara nafikiri ni suala la maamuzi tu magumu kwamba hatufiki kilometa moja mnashindwaje kutengeneza iwe lami kwa kushirikiana na Wizara nyingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali; tunayo makumbusho mengine ya pale Isimila, mapango ya Isimila ni kumbukumbu muhimu sana kihistoria;

Je, ni lini Serikali itatufanyia mpango kurekebisha miundombinu katika mapango haya ili nayo yaendelee kutumika kwenye utalii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiswaga Mbunge wa Kalenga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe tu Mheshimiwa Kuswaga pamoja na wananchi wa Kalenga kwamba, maeneo haya yenye kumbukumbu za kihistoria za wapigania Uhuru wa kipindi kile Serikali inayatambua na ilishayaainisha. Kama ambavyo nimetoa jibu la msingi ni kwamba Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wana familia kwa kuwaya haya maeneo asilimia kubwa yalichukuliwa na wana familia na wakati huo huo Serikali ilichukua baadhi. Kwa hiyo tukifanya mazungumzo tukayaweka vizuri tutahakikisha utalii kule tunauhamasisha vizuri na unaenda kukuwa kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye eneo hili la makumbusho ambalo ameliongelea Mheshimiwa Mbunge, ninamuahidi tu kwamba tutakwenda kulitembelea lakini pia tutafanya utafiti wa makusanyo ya kumbukumbu hizi ili tuziingize katika kumbukumbu za kihistoria, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwakuwa tokea kufutwa kwa tawala za kichifu hapa nchini majengo mengi sana ya kichifu yameharibika; na kwakuwa nia nzuri ya Serikali ni

kukarabati majengo haya kwa kulinda mila, tamaduni, desturi na urithi wa kihistoria;

Je, ni lini Wizara ya Maliasili na Utalii itafika Ngara na kufanya tathmini ya kasri la Chifu Baramba pamoja na Chifu Usoro sambamba na kuyafanyia matengenezo? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisaba Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya kihistoria tumekuwa tukishirikiana na halmashauri za wilaya kuyatambua kuyalinda lakini pia kuyasimamia na baadaye yanapokamilika tunayatangaza na yanakuwa ni vivutio. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wa Ngara, kwamba kwenye eneo alilolisema Mheshimiwa Mbunge niiombe Halmashauri ya Wilaya ya Ngara watuandikie barua, wayatambue yale maeneo na kuyalinda vizuri. Sisi twenda kuyathibitisha na kuyatangaza maana haya maeneo huwa tunayapa *GN;* yakishapata *GN* tayari tunatangaza kuwa vivutio na watalii tunaanza kuwaleta katika maeneo hayo. Kwa hiyo tushirikiana kwa hili ili kuhakikisha maeneo mengi yenye kumbukumbu tunayaibua na kuyaweka kwenye *GN*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufahamu ni lini Serikali itatuwekea lami katika barabara iendayo kwenye Kimondo katika Wilaya ya Mbozi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Shonza kuna wapigania uhuru waliokuwepo huko? Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Rungwe kuna vivutio vingi sana vya Utalii ikiwemo daraja la Mungu, kijungu na ziwa Ngozi lakini hakufikiki kabisa;

Je, ni lini Serikali itatujengea barabara ili kurahisisha watalii kufika maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepata fedha za UVIKO-19 na moja ya maeneo ambayo tunayakarabati ni pamoja na maeneo aliyoyataja ikiwemo ziwa Ngozi. Yote haya tumeyaweka vizuri ili tuanza kuleta watalii katika maeneo haya. Kwa hiyo nimhakikishie kwamba utalii utaanza kukuwa katika maeneo haya ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar, jiandae Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza niipongeze Wizara kwa kutoa fidia kwa wananchi waliopoteza maisha yao kwa kushambuliwa na Wanyama wakali kama vile Fisi; lakini cha ajabu ni kwamba waliofidiwa ni 12 wahanga ni zaidi ya 21.

Je, Wizara ina uwezo tena wa kurudia kufuatilia wahanga waliopoteza maisha yao ili waweze kupata fidia wote? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nyang'hwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wale wote walioathirika na wanyama wakali na waharibifu. Nimhakikishie tu Mbunge kwamba kwa eneo lake kama hawajalipwa basi ninamuahidi twende kufuatilia ili tuhakikishe wananchi hawa wanalipwa haki yao, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa changamoto za ukosefu wa miundombinu katika makumbusho inaikumba Makumbusho ya Magofu ya Kunduchi yaliyopo Wilaya ya Kinondoni: Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuboresha miundombinu ya magofu ya Kunduchi yale ya Ukoloni wa Mwarabu, yaani kwenye makaburi ya Waarabu ya Ukoloni, ili yaweze sasa kufahamika na kuendeleza ubora wake? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu za Makumbusho ya Kunduchi ambapo ndani yake kuna magofu ya makaburi na kadhalika, Serikali inayatambua na tulikuwa tumeanza kuyakarabati. Hivi sasa ninavyoongea ukarabati unaendelea. Pia tunatarajia kuweka uwekezaji katika maeneo hayo, zikiwemo hoteli za kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua na inaendelea na mchakato wa kuboresha maeneo hayo ili kuhamasisha watalii waweze kufika na kuzuru makaburi hayo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

Na. 449

**Ujenzi wa barabara ya Ifakara hadi Mahenge Mjini**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, ni lini barabara ya Ifakara Kibaoni hadi Mahenge Mjini itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ifakara (Kibaoni) hadi Mahenge Mjini (kilometa 70) ni sehemu ya barabara ya

Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo hadi Lumecha. Barabara hii kutoka Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo – Lumecha, ipo katika mpango wa miradi itakayojengwa kwa utaratibu wa *EPC + Financing*. Mpango huu unaratajiwa kuanza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nashukuru kwa majibu aliyonipatia, ingawa niliuliza barabara ya kwenda Mahenge Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, naishukuru Serikali kwa barabara ya kutokea Magole – Mvomero – Turiani kwa sababu imekamilika; je, kipande cha Turiani – Mziha – Handeni ni lini kitajengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Barabara ya kutoka Dumila – Ludewa – Kilosa inaendelea vizuri, lakini kipande cha Kilosa kwenda Ulaya mpaka Mikumi ni lini kitajengwa? Hata kwenye mpango wa bajeti sijakisikia, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Turiani kwenda Handeni ipo kwenye mpango kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, na ndiyo maana kipande cha kwanza tumeshakijenga. Pia kwenye hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa

Waziri wa Ujenzi wakati anasoma, imeoneshwa. Halikadhalika, barabara aliyoitaja ya Kilosa – Ulaya kwenda Mikumi pia kwenye kitabu cha bajeti cha mwaka huu cha Mheshimiwa Waziri imesomwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba Serikali ina mpango wa kuzijenga hizo barabara zote mbili kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mtenga.

Na. 450

**Kukarabati Kituo cha Polisi Mtwara**

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakarabati Kituo cha Polisi Mtwara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uchakavu wa Kituo cha Polisi Mtwara. Tathmini kwa ajili ya ukarabati imefanyika mwaka huu 2022, na kubaini kuwa kiasi cha shilingi 80,521,000 kinahitajika kwa ajili ya kugharamia ukarabati wa kituo hicho. Serikali itakiingiza Kituo cha Polisi Mtwara katika mpango wa ukarabati katika mwaka wa fedha 2023/2024 kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mtwara ni Mji ambao uko mpakani mwa nchi jirani, na inasababisha Askari wetu wa Polisi kufanya kazi ngumu kwa kukosa usafiri: Ni lini Serikali itatupatia gari la Polisi pale Mtwara Mjini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja Mtwara Mjini kuona changamoto ambazo zipo na zinazoendelea ili mambo haya yote tunayoyazungumza yapate ufumbuzi kwa urahisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuhusu ukosefu wa usafiri, na kwa sabbau ya changamoto zilizopo Mtwara, namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika *consignment* ya awali ya magari tutakayopokea, Mtwara itazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwenda Mtwara, nakumbuka wiki mbili zilizopita nilikuwa Mtwara kwa shughuli za uhamiaji, lakini nilipata nafasi ya kutembelea kituo hiki na kujiridhisha kwamba kina uchakavu mkubwa, na ndiyo maana tumekubaliana katika bajeti ijayo ataona tukisoma hizi shilingi milioni 80 kuwekwa pale kwa ajili ya ukarabati wa kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulitambua hilo, tumeweza kutenga zaidi ya shilingi 1,200,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya *RPC* Mtwara ambayo haikuwepo, na ujenzi wake unaanza mwaka wa fedha ujao, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya.

Na. 451

**Ulazima wa wakalimani wa lugha za alama katika vyombo vya habari**

**MHE. KHADIJA S. TAYA** aliuliza:-

Je, ni lini uwepo wa wakalimani wa lugha ya alama kwa vipindi vya habari vya televisheni, na ziara za viongozi utakuwa wa lazima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018 Serikali iliweka takwa la kuwa na wakalimani wa lugha ya alama kwenye vyombo vya habari kisheria, kwenye Kanuni za Maudhui ya Redio na Televisheni. Kanuni hizi zinavitaka vyombo vya habari kuwa na wakalimani wa lugha ya alama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Televisheni kama vile *TBC1, Azam TV, Channel Ten, Clouds TV, ITV, Upendo TV* na *Hope Channel* tayari zinatumia wakalimani. Hivyo, nitoe wito kwa vituo vingine vya televisheni kufuata sheria na kuhakikisha wanawatumia wakalimani wa lugha ya alama katika taarifa zao za habari na matukio mengine ya Kitaifa ili kuhakikisha kwamba ndugu zetu wenye ulemavu wa kutosikia nao waweze kuhabarishwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa jibu zuri. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kuna baadhi ya televisheni tayari wanatekeleza hii sheria. Je, kwa hivyo vituo vingine ambavyo havitekelezi sheria, ni nani mwenye jukumu la kuwasimamia au kuwalazimisha ili waanze kutekeleza hiyo sheria? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ya kutoa wito kwa vyombo vingine vyote kuhakikisha kwamba wanatumia wakalimani wa lugha ya alama ili kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata kuhabarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile labda nisisitize kwenye mamlaka husika kuwakumbusha wamiliki wote wa vyombo vya habari na wale ambao wanaratibu makongamano na matukio ya viongozi kuhakikisha kwamba wanazingatia utaratibu huu, kwa sababu ni takwa la kisheria. Kinyume na hapo, ni uvunjifu wa sheria, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Tarimba Gulam.

Na. 452

**Changamoto za Uuzaji na Ununuzi wa Fedha za Kigeni**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza: -

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu uuzaji na ununuzi fedha za kigeni kwa kulipa kima tofauti kwa *USD 100, USD 20, USD 10* na *USD 5?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za kigeni zinapokuwepo nchini huchukuliwa kama bidhaa ambayo hutunzwa na kuuzwa kwa thamani tofauti. Aidha, gharama za kutunza sarafu ndogo ni kubwa ukilinganisha na gharama za kutunza sarafu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya sarafu kubwa yapo juu zaidi kuzidi mahitaji ya sarafu ndogo. Hivyo bei yake ya kununuliwa huwa juu, kulingana na gharama ya utunzaji, mahitaji na wepesi wa kuziuza. Sarafu za Dola za Marekani 100 na zile za 50 hununuliwa kwa bei ya juu kuliko sarafu za dola za Marekani 20, 10, tano na moja, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali, hali halisi ni kwamba unaponunua shilingi, bei ya dola 100, 50 na zile za shilingi 20 na ndogo ndogo huwa ni sawasawa kama ilivyo wakati unavyobadilisha. Sasa kama hivyo ndivyo, ni kwa nini basi Benki Kuu isiwe inatoa bei elekezi hata kwa hizi noti ndogo ndogo ili kuweza kupunguza unyonyaji ambao nauona dhahiri kabisa wa kununua na kuuza ili bei iwe sawa sawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan ameitangaza sana Tanzania kiutalii, na watalii wako wengi sana nchini wanakuja; maduka ya kubadilisha fedha ni machache.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupunguza masharti ya ufunguaji wa biashara hii ili Watanzania wengi waweze kuingia katika biashara na vilevile kurahisisha upatikanaji wa huduma hii kwa wageni wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

Naibu Waziri akijibu mtampigia makofi vilevile.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kiasi na namna anavyopambana na kulipigania jimbo lake na wananchi wa Tanzania kuwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza; Serikali tayari imeliona hilo na imelizingatia na Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania itatoa bei elekezi kwa noti zote zile kubwa na ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili; ni kweli kabisa, na hapa ni lazima tumpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kiasi kikubwa alivyotangaza utalii na vivutio vyetu ndani ya nchi yetu. Hapa Serikali tumezingatia suala la kupunguza masharti. Wataalam wetu tayari wameshakaa, wanayachakata na hivi karibuni yatatoka masharti nafuu sana kwa ajili ya wawekezaji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Pondeza.

Na. 453

**Mtaala wa somo la historia nchini**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, Zanzibar wameshirikishwaje kuandaa Mtaala wa somo la Historia ikizingatiwa historia ya Zanzibar na Bara ipo tofauti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida huwa hatuna Mtaala wa Somo la Historia, isipokua tuna muhtasari wa somo la Historia. Hivyo, uandaaji wa muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania ulishirikisha wataalam na wadau kutoka Zanzibar kwa kila hatua ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi. Wataalam na wadau hao ni pamoja na Taasisi ya Elimu Zanzibar, *State University of Zanzibar, SUMAIT University,* Chuo cha Kiislamu cha Mazizini, watu mashuhuri na viongozi wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pondeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Tunatambua kuwa Serikali sasa inafanya mapitio ya mitaala na mihtasari yake ambapo masomo haya yataingia. Je, ni muda gani sasa Serikali itaweza kuleta hiyo mitaala mipya ambayo ina somo la Historia, iweze kutumika? Hilo ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nakumbuka Hayati Rais, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, alitoa agizo kuwa Somo la Historia liandikwe upya na liwe ni somo la lazima katika masomo yetu ya Tanzania; je, mchakato huu umefikia hatua gani sasa ili kuweza kufundishwa katika shule? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa tunafanya mapitio ya mitaala. Vilevile Mheshimiwa Rais mwaka 2021 wakati analihutubia Bunge, tarehe 22, Aprili, aliagiza jambo hili, nasi kama Wizara tulishaanza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba mpaka ifikapo Januari, 2024, mitaala hii mipya itakuwa tayari kwa kuanza kutumika. Sambamba na hilo, tutautumia mwaka 2023 kwa ajili ya kuandaa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, pamoja na kufanya majaribio ya mitaala hii mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, amezungumzia maagizo ambayo aliyatoa Marehemu Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli; jambo hili la uandaaji wa somo la Historia linaendelea vizuri. Naomba nikuhakikishie wewe na Bunge lako Tukufu kwamba somo la Historia tayari uandaaji wake ulikamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa vile sasa tunafanya mapitio ya mitaala hii, tunakwenda kulifanyia marekebisho kidogo ili mtaala mpya utakapoanza nalo liweze kufundishwa. Litakuwa ni somo kamili linalojitegemea na litafundishwa katika ngazi ya shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya. Mheshimiwa Michael Costantino.

Na. 454

**Kuanzisha Vitengo vya Wagonjwa wa Afya ya Akili katika kila Halmashauri nchini**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kitengo cha kutibu wagonjwa wa afya ya akili kwenye kila hospitali za Halmashauri nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri 175 zina waratibu wa huduma ya afya ya akili, na katika hospitali zote za mikoa kuna vitengo vya kutibu afya ya akili. Hata hivyo, Serikali inajipanga kuongeza nguvu kwenye utoaji wa elimu kwa umma kuhusu afya ya akili, sambamba na kuimarisha huduma za afya ya akili kwa wananchi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Costantino.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa swali langu la msingi lilihusu kuwepo kwa vitengo vya kutoa huduma kwa wagonjwa hawa, na majibu ni kwamba kila Halmashauri kuna waratibu: Je, waratibu hawa wana utaalam wa kutosha wa kushughulikia magonjwa hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Sote tunafahamu kwamba Hospitali ya Mirembe iliyopo Dodoma ndiyo hospitali pekee kubwa inayoshughulika na utoaji wa huduma ya wagonjwa wa afya ya akili, lakini sote tunafahamu kwamba hospitali hii ni kongwe na ya miaka mingi na majengo yake yamechakaa; je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha majengo ya hospitali hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kwamba waratibu ambao wamepangwa kule katika wilayani kama wana uwezo wa kutoa huduma hiyo; kwanza, ieleweke kwamba ugonjwa wa akili ni kama tunapozungumzia kichocho na mambo mengine. Daktari yeyote anajua kumhudumia mgonjwa wa afya ya akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachozungumziwa ambacho nafikiri yeye ndicho anachokiwaza, ni kuhusu watu walio-*specialize* kwenye afya ya akili (madaktari bigwa wa afya ya akili) ambao ndio hao tunaozungumzia sasa baada ya madaktari hao ambao sio bingwa wanapowashughulikia wale wagonjwa kwenye *level* ya wilaya, sasa wanaweze wakapelekwa kwenye mkoa na kupata huduma za kibigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema waratibu; wanaratibu vilevile masuala ya afya ya akili yaingie kwenye mipango kabambe ya Halmashauri na kuingia kwenye bajeti na hasa kwenye masuala ya dawa za wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu Hospitali ya Mirembe, sasa hivi Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu

Hassan, amepeleka zaidi ya Shilingi bilioni tano na zinafanya kazi, na kuna ukarabati na ujenzi mkubwa unaendelea pale.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, maswali yetu yamekwisha. Nina matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni waliopo Jukwaa la Spika wageni 17 wa Bunge kutoka Kanisa la *Tanzania Assemblies of God, Sinai Miracle Center* ya Ifakara Mkoani Morogoro wakiongozwa na *Reverend* William Msimbe, Mchungaji Kiongozi *Sinai Miracle Center,* pia kuna Dkt. Zephania Asenga, Mwenyekiti wa Idara ya *CMF-Sinai Miracle Center,* karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Bunge waliotembelea Bunge, wasimame kwa pamoja, wageni wa Waheshimiwa Wabunge tafadhali simameni kwa pamoja. Ahsanteni sana na karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 28 na viongozi watatu wa Kitivo cha Sayansi ya Siasa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kutoka Mkoani Iringa, karibuni. *(Makofi)*

Pia kuna wanafunzi 126 na walimu saba kutoka Shule ya Msingi Martin Luther ya Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wapo vilevile wanafunzi 50 na Walimu tisa kutoka shule ya Sekondari Kibwengere ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 63 na Walimu wanne kutoka Shule ya Daru-ul-Muslimeen ya Jijini Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Naibu Waziri wa Utamaduni na Sanaa Mheshimiwa Pauline Gekul, pamoja na Mheshimiwa Antony Mavunde Naibu Waziri Kilimo wanawatangazia Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge kwamba, wanawakaribisha kwenye

tamasha la kuchoma nyama itakayofanyika leo Ijumaa jioni kwenye Ukumbi wa *Royal Village* Dodoma ambapo wasanii mbalimbali watatumbuiza ambao ni Christian Bella na *Bushoke Band*, *VIP* shilingi 50,000 na kawaida ni shilingi 10,000; wote mnakaribishwa.

Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Semina ya Wabunge wote kuhusu masuala ya uwekezaji inayoratibiwa na *CRDB,* itafanyika leo siku ya Ijumaa tarehe 24 saa saba na nusu mchana katika Ukumbi wa Msekwa. Aidha, siku ya Jumamosi tarehe 25 kutakuwa na bonanza ya michezo kati ya Bunge, *CRDB* na wadau mbalimbali kwa utaratibu ufuatao:-

Saa kumi na mbili asubuhi mazoezi ya kutembea yataanza Bungeni kuelekea Uwanja wa Jamhuri, mazoezi ya ufunguzi rasmi na michezo mbalimbali itaendelea katika Uwanja wa Jamhuri na mchapalo kwa Wabunge na washiriki wote utafanyika saa 12 jioni katika Viwanja vya Bunge. Mgeni rasmi katika matukio yote hayo atakuwa ni Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano, tunaanza na Mheshimiwa Nyongo, wajiandae

Mheshimiwa Mathayo Manyinyi na Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa niendelee kuishukuru sana Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa wanayoifanya na hasa katika jimbo langu la Maswa Mashariki. Ni kwa mara ya kwanza toka tumepata uhuru mwaka 1961, Maswa imepata kiasi cha fedha kwa mwaka huu wa fedha bilioni 30, kwa mara moja katika Wilaya yetu ya Maswa. Hili ni jambo la kujivunia sana na sasa hivi tutaendelea kuboresha mifumo ya maji, barabara, shule, ujenzi wa vituo vya afya pamoja na kilometa moja ya lami katika Mji wa Maswa ambao sasa hivi ujenzi unaendelea. Tunashukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kupongeza Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa wanayoifanya na leo niko katika kutoa ushauri hasa ukitazama katika ile hotuba ya hali ya uchumi katika nchi yetu. Tuna maadui wakubwa watatu; tuna ujinga, maradhi na umaskini. Adui mkubwa ni umaskini ambao tukiwa na umaskini ni rahisi kumpata adui mwingine ambaye ni maradhi na maadui wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia kuhusu maradhi nitazungumzia zaidi kuhusu magonjwa na nini tufanye. Wataalam wanatuambia mtu mmoja kwa mwaka anaugua wastani wa mara nne kwa mwaka, yaani wewe unaweza ukawa umeugua mara kumi, mwenzako kaugua mara moja, ukipiga hesabu wastani binadamu mmoja anaugua mara nne kwa mwaka mmoja. Sisi Watanzania tuko milioni 60, maana yake ni kwamba tunaugua mara milioni 240 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuseme hivi wewe unayeugua ukatumia *paracetamol* tu kidonge kimoja kwa mwaka tunatumia *paracetamol* vidonge milioni 440, ukisema

utumie vidonge sita kwa siku, kutwa mara tatu utatumia vidonge 240 mara sita kwa siku moja. Nataka kusema hivi sababu gani? Tuna uhitaji mkubwa wa madawa katika nchi yetu na tuna upungufu mkubwa wa madawa na maradhi ni moja ya adui mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuwe na mipango inayoshirikisha Serikali yenyewe pamoja na sekta binafsi kuhakikisha tunapambana na adui huyu maradhi. Ukitazama hesabu za mwaka 2016, tumetumia fedha zetu kubadilisha kwenda kwenye fedha za kigeni ili tuweze kununua dawa kutoka nje ya nchi zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 457 mwaka 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017 tumetumia milioni 496 na tunategemea kutumia dola za Kimarekani milioni 730 ni *billions, billions* ya fedha za kitanzania. Wazalishaji wa ndani Tanzania wa dawa wako 18 tu na wazalishaji wa vifaatiba wako 24 tu, tuna-*spend importation* ya dawa kwa asilimia 94 ya dawa zote, tunatumia asilimia sita tu kwa dawa tunazozalisha ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nusu ya dawa zote tunazozingiza zinatoka India. Ukitazama dira na maendeleo na mpango tulionao tunataka tujikite kwenye kilimo, mifugo, uvuvi na nishati, suala la *pharmaceutical production* halimo kwenye *priority* zetu. Hii ni hatari, kama tunataka kupambana na adui maradhi ni lazima tutafute namna ya kujitegemea kuzalisha dawa, vifaatiba na vitendanishi. Hii hesabu ya kuugua mara nne kwa mwaka siyo ya Watanzania tu, ukienda Kongo wana hesabu yao, Kenya wana hesabu yao, Uganda wana hesabu yao na nchi zote za jirani na tupo kwenye *East Africa Community* na tuna mpango wa mwaka 2025, tupo kwenye *SADC,* haya yote ni masoko yetu, hivi sisi Serikali kwa nini tusifikirie namna bora ya kufanya uzalishaji wa madawa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri wa muda mfupi na muda mrefu. Ushauri wangu wa kwanza kwa wazalishaji waliopo Tanzania hawa wachache tulionao, tunaomba kupitia *MSD* wapewe zabuni ambayo ni *exclusive tender* ili waweze kupunguziwa kodi wazalishe dawa za kutosha ambazo wana uwezo nazo wa kuzizalisha. La pili, *MSD* iwafungulie wazalishaji wa ndani *local letters of credit* ili waweze kupata *discount* ya *local credit letters* zao ili waweze kupata uwezesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakandarasi hapa Tanzania wanapewa *mobilization fund* mpaka asilimia 50, kisha wanafunguliwa *letter of credit,* baadaye wakimaliza kujenga wanapewa fedha hizo, kwa nini tusifanye kwenye *pharmaceutical producers.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine kuna wazalishaji wanazalisha dawa hapa nchini kwa nini tusifanye *single sourcing,* kama mtu anazalisha *paracetamol,* tununue *paracetamol* kutoka kwake tumwezeshe tusiingize na yule anayetaka kuingiza *paracetamol* kutoka nje ya nchi atozwe kodi kubwa ili tum- *discourage* asiingize hizo dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, wazalishaji wa ndani wapewe upendeleo wa bei mpaka asilimia 30, kwamba kama kuna mtu anauza dawa kidonge shilingi 100 mzalishaji wa kwako wa ndani anauza kwa shilingi 110, mpe kipaumbele yeye, usinunue ya kutoka nje ya shilingi 100 kwa sababu na wao huko nje, kwa mfano India, wanapewa *discount* ya asilimia 30 mpaka 40, wanawezesha kuzalisha. Kwa hiyo unaletewa dawa ambayo tayari ipo *discounted,* inakuja kushindana na dawa ya Mtanzania ambaye yeye amezalisha kwa gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine iondelewe kodi kwenye vifungashio, vinaongeza gharama ya *production.* Matokeo yake mzalishaji wa ndani anauza dawa kwa bei juu

anashindwa ku-*compete* na yule ambaye amezalisha nje na amepewa mazingira mazuri ya uzalishaji. Huo ni ushauri wangu nautoa kwa ajili ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa muda mrefu Serikali lazima tu-*intervene,* tushirikiane na sekta binafsi, kwa nini tusitengeneze sehemu au kijiji tukafanya *mobilization* ya kupeleka umeme tukapeleka maji, tukapeleka vitu vyote ambavyo vinahitajika katika uzalishaji wa madawa na tukauza na tuka-*supply* katika nchi za jirani na tukawa tume-*serve purpose* ya kujitosheleza kwa dawa sisi wenyewe; cha pili, tuka-*export* kwa maana ya ku-*balance,* iwe *balance of trade* kwa maana ya kwamba tukafanye biashara ya nje; na cha tatu tukatoa ajira tume-*serve purpose* tatu kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki zitoe mikopo kwa wazalishaji wa madawa, *special* mikopo kwa ajili ya kutoa *operating capital. TMDA* asiwe mdhibiti tu, *TMDA* awe ni mratibu na mwezeshaji ili kusudi wazalishaji wa ndani waweze ku-*qualify* ile *WHO pre-qualification* ili dawa zetu zikubalike, zizalishwe bora kwa bei nafuu na zikubalike kuuzwa hadi nje ya nchi, tutakuwa tumefika mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema tuwawekee mazingira mazuri wazalishaji wa nje waje watuletee ….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili malizia.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, tufanye *research and development,* lazima tuwekeze kwenye kufanya *research* ili tuweze kuzalisha dawa na tuweze kuuza hadi nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Manyinyi, jiandae Mheshimiwa Martha Gwau.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo katika Wizara hii. Naendelea kuishukuru Serikali kwa maana ya Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya lakini vilevile na kwa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme katika maeneo matatu; la kwanza, nianze na suala la hospitali ambalo kwetu njia ya kulitatua ni ndogo sana. Pale Musoma Mjini sisi hatuna hospitali ya wilaya tunatumia zaidi vituo vya afya pamoja na hospitali binafsi. Tumekuwa tukiahidiwa kwamba baada ya kuwa tumepata hospitali ya rufaa pale ile hospitali yetu ambayo ni ya mkoa tutapewa iwe hospitali ya wilaya na kama tunavyofahamu ile hospitali tukishapewa kama hospitali ya wilaya maana yake gharama za matibabu kwa watu wetu zitakuwa chini. Sasa ni imani yangu kwamba Serikali inahitaji itoe tamko ni lini itaturudishia ile hospitali yetu ili watu wetu waweze kutibiwa kwa gharama za chini kuliko wanavyoenda pale kama hospitali ya mkoa na gharama zinakuwa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo lipo suala la *NHIF*. Sasa tumesema tunataraji kwamba itoe huduma kwa watu wote, lakini nadhani vipo vitu vya kufanya maana mpaka sasa hivi inatoa huduma katika maeneo machache lakini bado haionyeshi kama utoaji wake ni mzuri sana. Wiki iliyopita nilienda Dar es Salaam, nikaamua kwenda kupima pale kwenye hospitali moja inaitwa Ibrahim Haji, ipo pale Kisutu, nilipotoa ile bima ya *NHIF* walinikatalia kwamba wao saa hizi hawa-*deal* na *NHIF otherwise* nitoe bima nyingine. Sasa nikaanza kujiuliza kwamba kama hawa wana watu

wachache tu hivi au vituo vichache vya kuhudumia na hawawezi kuvikubali, basi maana yake tutakapopeleka kwa watu wote, nadhani tutapata changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki hii tena imetutokea pale Musoma Mjini, kama nilivyosema kwamba pale Musoma Mjini tunayo hospitali moja inaitwa *Royal,* ni hospitali ya *private* lakini inahudumia wagonjwa wengi sana wa bima. Mfano kwa pale mjini ndiyo inayoongozwa, nilikuwa naangalia hapa kumbukumbu zangu kwenye mwezi Mei peke yake, imehudumia wagonjwa 5,000, lakini hizi zingine mpaka hospitali yetu ya mkoa imehudumiwa wagonjwa chini ya 2,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kilichotokea ile hospitali ya *Royal* ilipata shida kidogo nadhani kwenye upande wa malipo sijui ilkuwaje na ikapigwa faini na ikaja ikalipa ile faini. Kilichojitokeza ni kwamba pamoja na kulipa zile gharama ambazo walipaswa kulipa, ile hospitali leo imefungiwa, tafsiri yake ni kwamba zaidi ya wagonjwa 5,000 ambao wamekuwa wakitibiwa pale kwa mwezi nao sasa wanakosa huduma. Sasa kwa hali kama hiyo tukiiacha ikaendelea na wakati huo tunasema tunataraji kwamba sasa watatoa huduma kwa watu wote, nadhani hiyo ni changamoto moja kubwa ambayo itatuumiza sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niombe utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni ombi langu kwamba, Serikali hata kama hospitali imekuwa na shida, lakini matokeo yake ni kwamba wananchi ndiyo wanakuja kupewa hiyo adhabu. Kwa kweli sidhani kama hili linakubalika hata kidogo na naiomba Serikali iweze i-*intervene* haraka ili watu wa Musoma waendelee kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nilidhani nalo sasa Mheshimiwa Waziri anapaswa kuliangalia kwa macho yote, sisi kama nchi, nakumbuka kwamba hata zile nchi zote tunazoziona, nchi zilizoendelea, wakati zinaanza mchakato wa maendeleo walikuwa na mapinduzi. Moja, walifanya mapinduzi ya kilimo, wakahakikisha kwamba wanaweka nguvu kubwa kwenye ukulima na ndiyo maana mpaka leo yapo mashamba ya mikonge mengi na makubwa na mashamba ya mazao mbalimbali, hata hapa kwetu ni kwasababu walifanya mapinduzi ya kilimo. Walipotoka hapo wakafanya mapinduzi ya viwanda, walipotoka hapo wakafanya mapinduzi ya teknolojia. Sasa leo ndiyo maana wanaendelea na teknolojia katika kuboresha kilimo, teknolojia katika kuboresha viwanda na kutokana na hali hiyo wale wenzetu wanaenda kwa *speed*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijiuliza Tanzania hivi sasa tupo kwenye mapinduzi yapi? Kwenye kilimo hatupo, kwenye viwanda hatupo, kwenye teknolojia hatupo. Kwa hiyo ni ombi langu kwamba, leo sisi Watanzania tuna tatizo kubwa sana la ajira. Tunazalisha vijana zaidi ya milioni mbili kila mwaka wanaoingia kwenye soko la ajira na sehemu pekee inayoweza kutukomboa ni pale tutakapofanya mapinduzi ya kilimo, lakini kila mahali bado tunarashiarashia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa maana ya Mheshimiwa Waziri ameweza kupandisha bajeti ya kilimo mpaka sasa kwa zaidi ya bilioni 900, lakini ombi langu kubwa tuwe na mipango mahsusi. Nasema kwamba, ni vizuri fedha hizi zingejulikana kila mkoa unapata fedha kiasi gani na mipango madhubuti ikaanzishwa ya kuhakikisha kwamba kweli tunakuwa na mabonde kwa ajili ya umwagiliaji na mabonde kwa ajili ya kilimo. Nishauri kwamba hata wale Viongozi wetu wale wa Mikoa kama Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya pamoja na shughuli zingine za ulinzi na usalama, wawe wasimamizi wakubwa katika hiyo miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea kwamba tukiweka nguvu katika kilimo hata wale vijana wengi ambao wanahamia mijini hawana sababu ya kwenda mijini, lakini watu wengi leo wanahama vijijini na kwenda mjini ni kwa sababu kule vijijini hali ngumu, hakuna miundombinu ya kuwawezesha waendelee kuishi kule. Kwa hiyo kutonana na hili ndiyo maana watu wengi sasa wanaendelea kukimbilia mjini wanahama vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, katika kipindi hiki, kwenye bajeti hii, ningependa kujua kwamba kwenye Mkoa wetu wa Mara pale tunapata fedha kiasi gani na ili tuweze kujipanga tuhakikishe kwamba kilimo tunaendelea kukiboresha ili kiweze kuajiri watu wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Martha Gwau. Jiandae Mheshimiwa Mwita Waitara. Jiandae Mheshimiwa Zahor.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii na mimi uliyonipa ya kuchangia kwa siku ya leo. Kwanza kabisa naomba nishukuru kwa hotuba nzuri iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri. Lakini kwa mikakati na mipango mizuri aliyoianisha katika hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza ni kuhusu 4-4-2 ile mikopo yetu ya Halmashauri. Ni ukweli usiopingika kwamba akinamama wengi na vijana wengi ndiyo wapiga kura wa Mama Samia wa mwaka 2025. Lakini kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe amekiri Kaka yangu kwamba wanawake ni walipaji wazuri wa mikopo. Sasa tukiwatolea hiyo asilimia 10 tukawapa tano, hatutakuwa tumewasaidia na ukizingatia kwamba bado maombi ni mengi na uhitaji ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kaka yangu kwa sababu tunatoka wote Singida, sasa sijui tutaongozana wewe utapita Tabora mimi nipite wapi, lakini tukifika kule Singida sijui tutaongea lugha gani. Mimi ninachoomba ushauri, labda tuangalie namna nzuri sasa ya hii mikopo kurejeshwa. Kwa sababu najua kuna changamoto ya ulipaji wa hii mikopo, tuangalie namna nzuri watu hawa wapewe elimu kabla hawajapewa hiyo mikopo ili waweze kuilipa vizuri wakiwa na elimu nzuri ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tuangalie muda wa marejesho. Mara nyingi sana mikopo mingi ikiwa na muda mfupi wa marejesho inampa mzigo yule mtu kuilipa, kwa hiyo tuongeze muda wa marejesho ili watu waweze kulipa kidogo na waweze kufanikisha kulipa. Hii asilimia mliyotaka kuikata mnaweza mkapata sehemu nyingine kwa ajili ya ujenzi wa hizo stendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la Pili ni kuhusu *TIN Number*. Mimi naomba niipongeze Serikali kwa kuja na wazo zuri la miaka 18 kila mtu awe na *TIN Number*. Nadhani labda imepokelewa vibaya lakini ilimaanisha atalia kodi yule tu atakayekuwa na kipato, kitu ambacho ni kizuri. Ni lazima tujengee watu wengu *discipline* ya kuchangia maendeleo ya nchi yako. Tusipojenga *discipline* kuanzia mwanzo, tutashindwa kuendeleza nchi hii kwa sababu *discipline* inajengwa, wanakwambia samaki mkunje angali mbichi. Inabidi tujenge *discipline* kuanzia chini ili mtu anapopanda juu akifika miaka 20 anajua anaweza akalipa kodi ama akifika miaka 30 anajua anawajibu wa kuchangia maendeleo ya nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nashauri kitu kimoja au viwili, kuwe na siku ya mlipa kodi. Uwe umefanya kazi, umefanya biashara, hujafanya uta-*declare* nimepata sifuri sijafanya kazi mwaka huu na watakupa *certificate*

kwamba hujafanya kazi mwaka huu kuliko kuwa na *TIN* halafu tukae, hapana. Mwakani akienda hajafanya kazi anapewa sifuri analipa sifuri. Kwa hiyo, tukifanya hivyo tutamjengea tabia ya kuwa anasubiri ile Tarehe ya mlipa kodi anaenda ku-*declare* alichokitengeneza. *Whether* kwenye biashara, *whether* wapi atasema nimepata sifuri na atapewa *clearance* amelipa sifuri. Hii inamsaidia akija kukua anakuwa ni mlipa kodi mzuri. Hapo tunaongeza wigo wa asilimia ya walipa kodi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna *EFD machine* bahati nasibu inakuja. Mimi naomba nimpongeze sana kwa hiyo *idea,* kwa sababu itahamasisha watu wengi kutumia mashine za *EFD* na wakijua kwamba tutapata bahati nasibu. Ni kama motisha Serikali inatoa kwa watu wake kuhamasisha kulipa. Hilo ni wazo zuri, nampongeza sana, lakini tusisahau tarehe ya mlipa kodi ambayo kila mtu aka-*declare* fedha zake alizotengeneza na kama hana asiogope atasema *zero*. Kwa hiyo, hajapata atapewa cheti kwamba hajafanyakazi na kila mtu atakuwa na wajibu wa kusema ngoja nikaisaidie nchi yangu, nikaisaidie jamii yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni mabenki. Mabenki yana mchango mkubwa sana kuongeza wigo wa kodi. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba tunataka tuongeze wigo wa walipa kodi. Sasa mimi swali langu najiuliza, hawa tulionao tumewatumia vizuri? Hawa tulionao tume-*make sure* wamelipa kodi vizuri? Kabla hatujaongeza wengine je, hawa waliopo wanafanya vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri jambo, mabenki yana mchango mkubwa sana wa kutusaidia kuwafanya wafanyabiashara walipe kodi ipasavyo. Ukweli ni kwamba tunashida ya uaminifu. Uaminifu umekuwa ni kikwazo kikubwa sana katika nchi yetu. Mtu ana-*transaction* za benki anayo *inflow* na *outflow* kubwa lakini mwisho wa siku *TRA* ana-

*declare* amepata fedha ndogo ili tu alipe kodi kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa je, mabenki yana mchango gani katika kutusaidia kuwafanya hawa watu wanaostahili kulipa kodi walipe kodi stahiki, badala ya sasa hivi kwamba mimi naweza nikawa natengeneza shilingi milioni 500, milioni 200, milioni 100 ila naenda *TRA* nimelipa kodi shilingi milioni mbili. Sasa ushauri ni huu, benki mara nyingi hawa wafanyabiashara wetu wanaomba mikopo. Wakiomba mikopo wanapeleka *tax clearance* kama kigezo cha kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *tax clearance* haisemi huyu mtu kalipa shilingi ngapi? Ndiyo maana tunaishi kwenye nchi ambayo mabenki yanalalamika mikopo hailipiki, wateja wanalalamika wakopaji riba ni kubwa. Serikali inalalamika watu hawalipi kodi. Sasa kigezo umelipa kodi kiasi gani, kiwe kigezo namba moja cha mtu kukopesheka. Hii itasaidia kujenga *trust.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda benki kukopa *inflow* na *outflow* zako zinaonesha wewe ni mtu unapata shilingi milioni 300, 200, sasa iweje akichukua kodi yako uliyolipa Serikalini umelipa shilingi milioni moja, haina uwiano na *amount you are making* na kodi uliyolipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kabla hatujatengeneza walipa kodi wengine, hebu tujue jinsi ya kuhakikisha hawa waliopo *are they doing good or not* na tumewatumia kiasi gani. Kwa hiyo, ina maana ukijenga huo utamaduni kila mfanyabiashara anataka mkopo benki au kwenye hizi *financial institution* ndogo ndogo, sasa wanachofanya wanapeleka *tax clearance* kwamba Mheshimiwa Martha Gwao ni mlipakodi basi, *that does not make somebody to be responsible or does not make somebody to be trusted* na benki. *In order to for somebody to*

*be trusted, you have to be trusted in the Government first.* Wewe umelipa kodi Shilingi Milioni 10, wewe ni mwaminifu kwa Serikali yako, mkopo unapata kwa uaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia mabenki waache kulialia kila siku mikopo hailipiki. *They are doing loan to the wrong borrowers* kwa sababu hatujawasaidia sisi kama Serikali kuhakikisha kwamba wanajua mtu amelipa kodi kiasi gani. Kwa hiyo, uaminifu wa mkopaji utaanzia kwenye Serikali yake. Kalipa kiasi gani kutokana na *inflow* na *outflow* zitakazokuwa zimepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kuhusu vyuo vya kati. Kwa kweli naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais ametusaidia vijana wetu wa *Form Five* na *Form Six* sasa hivi wanasoma bure, lakini hili wazo la Mama ni zuri. Je, hawa watu wanaoenda Kidato cha Tano na Kidato cha Sita wanapata elimu bure…*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri kengele ya pili imepigwa.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara. Mheshimiwa Zahor. Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Kwanza naomba kuunga mkono hoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa bajeti ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nampongeza Mheshimiwa Rais kwa jambo kubwa ambalo anaenda kufanya kwamba kila fedha inayokusanywa inapelekwa katika kuendeleza miradi ya wananchi, hilo ni jambo kubwa sana ndiyo maana leo kila Mbunge akisimama hapa atataja

mradi ambao umefanyika katika Jimbo lake, hiyo ndiyo siasa na ndiyo kazi ambayo umma unahitaji ifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa bajeti nzuri sana ambayo ameisoma hapa Bungeni, Watanzania wengi wanasubiri tu utekelezaji wa ahadi kemkem ambazo zimetolewa na wanayo matumaini makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali pia kwa kuondoa ada katika kidato cha tano na cha sita. Niombe tu mambo mawili yafuatwe katika eneo hili. Jambo la kwanza ni vizuri tukaweka wazi kwamba hii ni elimu bila ada siyo elimu bila malipo. Kuna *confusion* kubwa kwa wananchi kule, kwamba kuna baadhi ya maeneo wazazi wenyewe au shule yenyewe au jamii ambayo inazunguka shule wanapanga mipango ya maendeleo na kuna watu ambao wamesoma katika eneo hilo, wafanyabiashara, watumishi ndani na nje ya nchi wanapanga mipango ambayo wanaweza wakachangia kuboresha shule yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukisema kwamba ni elimu bila malipo, watu wengine wanakataa kuchangia kwamba elimu ni bure moja kwa moja. Kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Waziri akaliweka wazi Waziri wa TAMISEMI kwamba wananchi wajue ada imeondolewa. Lakini pale ambapo mwananchi anaweza kuchangia maendeleo ya shule yake, ama ya msingi ama sekondari anaruhusiwa kufanya hivyo bila kushinikiza na bila kukandamiza wale ambao hawana uwezo kufanya hivyo katika maeneo hayo na watoto wasibaguliwe katika mashule. Mkisaidia hilo, mtafanya watu wawajibike katika maeneo yao, itapunguza mzigo wa Bunge kupiga kelele kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye ofisi ya Rais, TAMISEMI. Eneo hili, Wizara zote ambazo wamezungumza hapa, fedha hizi zote mwisho wa siku

zinaenda kwenye Mikoa zinaenda kwenye Halmashauri. Hili ni eneo ambalo Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI akijipanga vizuri na timu yake na najua uwezo huo anao, atamsaidia Mheshimiwa Rais, ataisaidia Serikali, atasaidia pia na Chama kiendelee kushinda katika maeneo yale kwa sababu miradi itatekelezwa vizuri na kuondoa manung'uniko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara 145 ya Katiba yetu na Ibara 146 imeelekeza kwa nini kumeanzishwa Serikali za Mitaa. Pia imeelekeza madaraka ya watu walioko kule ambao wanafanya kazi ya maendeleo na lengo kuu ni kupeleka miradi ya maendeleo katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili tunayoshida kubwa na hapa hatuwezi kuficha. Tunashida kubwa ya usimamizi wa miradi na uongozi ama kwenye Mikoa ama kwenye Wilaya au kwenye Halmashauri. Kwa sababu unakuta Baraza la Madiwani wamepanga mipango yao kulingana na vipaumbele vyao. Hawa Wenyeviti wa Vijiji, Madiwani, Wabunge, Mheshimiwa Rais wameenda kuomba kura kwa Watanzania na ili uchaguliwe ni lazima utoe ahadi kwamba hapa hakuna kituo cha afya utaleta lini? Hapa hakuna maji mtaleta lini? Hapa hakuna shule mtajenga lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama Madiwani katika Halmashauri zetu na Wabunge wamepanga mipango yao, halafu yanakuja maagizo ambao kwa kweli siyo sawasawa. Kama Mbunge na Halmashauri yake walipanga kujenga kituo cha afya eneo 'A', *order* ikatoka kwenye Mkoa au kwenye Wilaya ikasema hamisha kutoka 'A' peleka 'B' huo ni mgogoro tayari kwa sababu Mkurugenzi anakuwa *stranded*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna oda ya Mkuu wa Wilaya mahali anamwambia hamisha fedha, lakini sheria inasema Mkurugenzi hawezi kufanya jambo ambalo Madiwani hawakukubali, lakini anaogopa kwamba Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya ameniagiza. Sasa huyu mtu unamuweka

katika mazingira magumu sana katika kutekeleza kazi yake. Naomba jambo hili liwe wazi ili lisimamiwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni wakati muafaka kupitia Sheria ya Serikali za Mitaa. Vitu vingi tuli-*copy* na ku-*paste* tangu wakati wa ukoloni. Kwa hiyo, wakati wa sasa hivi inawezekanaje Mbunge katika eneo lake wamepanga mipango, yaani mimi nimesema kwenye Kata yangu, *let say* ya Bumera nitapeleka kituo cha afya, tumekubaliana mimi niko Bungeni hapa kuna mtu mwingine anaagiza hamisha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakijenga hicho kituo, Mbunge ukienda Jimboni wananchi wanasema huyu Mbunge hakutupenda, tusingepata kituo cha afya kama siyo DC au RC. Maana yake Mbunge anakuwa *very unpopular* katika eneo hilo. Hili ni lazima Waheshimiwa Wabunge tulikatae, tukubaliane kwamba ni lazima mipango tuliyopanga isimamiwe. Anayeenda kuomba kura za Rais za Chama cha Mapinduzi siyo Mkuu wa Mkoa, siyo Mkuu wa Wilaya ni Mbunge, Diwani, Mwenyekiti wa Kitongoji na Mheshimiwa Rais mwenyewe, tusichanganyane katika miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni migogoro ambayo ipo, nimeambiwa kuna maeneo hapa Kondoa shida ilitokea, kwa Mheshimiwa Kigwangalla shida imetokea, kule Tarime Vijijini shida imetokea, Kigoma shida imetokea. Sasa hili jambo Waheshimiwa Wabunge nataka niwaombe, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni lazima tukubaliane utaratibu kwa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuendeshana hapa kama magari mabovu, Mbunge anakuja hapa anasimama, najenga hoja, napata fedha, yuko mtu kule anabadilisha miradi, haiwezekani! Haiwezekani tukubaliane, kwa hiyo ni muhimu sana…*(Makofi)*

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Ninamshukuru Mheshimiwa Waitara kwa mchango mzuri anaoutoa. Nataka nimpe tu taarifa kwa mchango wake mzuri anaoendelea nao kwamba hata Wilaya ya Rorya, Baraza la Madiwani pamoja na wananchi waliridhia kujenga kituo sehemu 'A' lakini maelekezo yakatoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa maana ofisi *RAS* na *DC*, wakahamisha kutoka sehemu 'A' wakapeleka sehemu 'B' hivi ninavyozungumza mgogoro ni mkubwa kweli kule na haujatatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niendelee kumuongezea Mheshimiwa Waitara kwamba anachokisema ni sahihi na kinatokea kwenye Majimbo na Waziri wa TAMISEMI analifahamu. Kwa hiyo, ni vyema Waziri akatolea maelekezo mapema ili hii migogoro isiendelee maeneo mengi kwenye nchi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kuacha kupokea taarifa tamu kama hiyo. Nataka nikuambie na Serikali isikie vizuri. Katika eneo ambalo mnapaswa kumsaidia Mheshimiwa Rais ni eneo la kuimarisha Serikali za Mitaa, hilo lazima mpigie mstari. Kwa sababu hata nimekaa hapa Bunge nimeambiwa Vunjo kuna mgogoro. Nimeambiwa Rorya, tena kule Rorya nimeona kwenye mitandao, Mkuu wa Mkoa ameagiza DC asimamie, *can you imagine*! Kwamba Baraza limeamua, Mbunge yuko Bungeni anaongea mpaka na Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa TAMISEMI ameandika *massage* kumuagiza *RC* wa Mara, yule amemwambia *DC* endelea. Msingi wa kituo cha afya anachimba *DC* peke yake pale. Sasa Mwenyekiti wa Kijiji

amekamatwa yuko ndani wiki ya ngapi sijui sasa, wananchi wamekamatwa na wananchi wamegoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naona Ofisi ya Rais haijachukua hatua! Nataka niwaambie Waheshimiwa Viongozi na Wabunge hasa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, katika eneo ambalo tutasaidia hapa kuendelea kutawala nchi hii vizuri ni kuimarisha Serikali za Mitaa. Miradi mliyopanga ni lazima isimamiwe na Mbunge lazima uwe na sauti ya miradi kwenye eneo lako, na Diwani lazima asimamie. Haiwezekani *RC* anakuja eneo yaani naomba niishie hapo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuambie na Wabunge kwamba eneo hili kwa mfano, mkiangalia nchi nzima utakuta *RC* anaenda mahali ndiyo anawajibisha watumishi, hawa ni Wakuu wa Mikoa Watendaji. Niambie ni lini ulimuona Katibu Tawala kama Mkuu wa Utumishi anasimamia na kuongea na watumishi wake, lini uliona kwenye Mikoa yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yote watu waliosimamishwa ni Wakuu wa Mikoa. Sasa kwa nini tuna *DC* pale, tuna Katibu Tawala Mkuu wa utumishi, tuna Mkuu wa Mkoa kule, tunataka wote wafanye kazi zao. Watumishi wa Halmashauri zetu ndiyo maana kuna wizi mkubwa sana kwa sababu watu badala ya kuelezwa wanatishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu akija kwenye kikao ameita Waandishi wa Habari anaambiwa simama wewe, wewe ni mwizi. Watu wamesimamishwa miezi mitatu, sita, wengine ni watoto wa kike. Mimi nina *massage* hapa yuko mtumishi mmoja kule Tarime anaomba amuone Mheshimiwa Rais kama mwanamama mwenzake amsaidie kwa sababu ametishwa, kasimamishwa kazi, hakusikilizwa na yuko mtaani!*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Waitara.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Bunge tuna wageni kutoka *Karibu Tanzania Organization* ikiongozwa na Bi. Vivian Temu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Mheshimiwa Zahor na Mheshimiwa Mulugo jiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa muda. Pia kwa sababu ya muda mchache naomba nichangie maeneo machache na kwa muda mchache.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwanza naomba niishukuru Wizara kwa kuleta mpango wa maendeleo lakini kwa kuleta Bajeti yake hii Kuu. Kwa kweli ni bajeti ambayo ime-*cover* maeneo mengi lakini kwenye taarifa yake ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha mwaka 2021/2022. Kwa kweli kazi kubwa imefanyika na tuwapongeze. Kwa sababu kwenye ushahidi hapa 2021/2022 Serikali ilipanga kukusanya Shilingi Trilioni 37.99 lakini mpaka Aprili iliweza kukusanya Shilingi Trilioni 29.84. Hii ni kazi kubwa sana. Kwa hiyo, naomba tuwashukuru sana na tuwape moyo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo hiyo ninaomba tumshukuru na tumpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa sababu mirai yote inaendelea vizuri. Pamoja na changamoto lakini hakuna mradi ambao tumepewa taarifa kwamba umekwama. Naomba tumpe moyo na aendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba tumpongeze na tuipongeze Wizara ya Kilimo kwa sababu mwaka huu imefanya kazi kubwa ya kulielekeza taifa kwamba kilimo ni sehemu ya ajira na kilimo ndiyo sehemu ya ukombozi wetu kama Watanzania. Kwa hiyo ninaomba niipongeze Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Mama Samia kwa sababu kweli amedhihirisha kwamba kilimo ndicho ambacho kitatuokoa, na amengenga fedha nyingi; kwa hiyo tumpe moyo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa maana hiyo hiyo, kwa sababu kama Serikali inaendelea na kuhakikisha kwamba inawatunza kwa kuwajali wananchi wake kwenye suala la afya; amesema pale kaka yangu, kwamba inatumia fedha nyingi kuagiza dawa kutoka nje na akaiomba Serikali ihakikishe kwamba inajipanga ili kutoa nafasi ya kuweza kutengeneza dawa kwetu pamoja na kwa majirani zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa maana hiyo hiyo Serikali imejipanga kuongeze vyanzo vya mapato. Naomba sana, viko vyanzo vya mapato vinatupa pesa nyingi lakini vyanzo hivihivi vinatulelea madhara kesho na kutwa maana yake tunatengeneza bomu bila sisi kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika wiki iliyopita nilihudhuria kwenye mafunzo mafupi sana. Mafunzo haya ni juu ya kujaribu kuya-i*dentify* maradhi ambayo hayaambukizwi, maradhi hayo moja ya chanzo yanachangiwa na maisha yetu. Kwa mfano matumizi yetu ya tumbaku; tumbaku kwa mujibu wa taarifa za Serikali inatuingizia pesa nyingi sana, lakini tumbaku hii inatusababishia maradhi makubwa sana. Sasa mimi ningeomba tuchagua hapa kwamba tunapata pesa leo nyingi lakini tunaandaa maradhi kesho na kesho kutwa makubwa Serikali italazimika kutumia pesa nyingi sana.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa

**T A A R I F A**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji si tumbaku tu peke yake inayotupa madhara, hata soda hata ugali, ni kila kitu ukikizidisha madhara yake ni makubwa. Kwa hiyo nimuambie mzungumzaji kwamba sio tumbaku tu ni kila kitu hapa duniani ukikitumia bila utaratibu kina madhara, ahsante sana.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimimiwa Naibu Spika, nakiri kaka yangu amezungumza kwamba kila chenye ziada kina madhara; lakini tumbaku aihitaji ziada; tumbaku anaathirika mkulima, anaye-process, anayetumia, wote; kwa hiyo hili alihitaji ziada hili linahitaji hata ukaribu wako tun a tumbaku unaendelea kukuathiri. *(Makofi)*

Mheshimimiwa Naibu Spika, naomba niendelee, kwamba katika taarifa yetu hii kwenye suala la mipango mipango ni mizuri sana lakini mipango hii imeshirikisha kwa uchache sana eneo linaitwa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba ninukuu Katibu ya Jamhuri sura yetu hii ya nne inazungumza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuitaja kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri. Lakini naomba niinukuu Katiba ya Zanzibar sura ya kwanza sehemu ya kwanza. Wanasema Zanzibar ni nchi ambayo ni eneo na mipaka ni eneo la visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo. Kifungu cha pili inasema Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hii ni katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini; maana yake ni kwamba katika mipango yetu ya Tanzania Zanzibar ni

sehemu. Kwa hiyo ningeiomba Serikali wakati tunapanga mipango hii Zanzibar tuelewe kwamba ni sehemu na kwa kweli tuishirikishe ipasavyo kwa sababu tunalo tatizo la uchumi wa Zanzibar. Zanzibar inajitahidi lakini bado vyanzo vyake ni vidogo kwa sababu eneo lake ni dogo ardhi yake ni ndogo kwa hiyo maana yake lazima tuichukuwe Zanzibar kwamba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano na tusiiache mbali. Kwa sababu Waswahili wanasema kwamba njaa haina rafiki. Kwa hiyo maana yake ni kwamba lazima tujitahidi kuishirikisha Zanzibar kwenye mipango yetu ya maendeleo kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimimiwa Naibu Spika, lakini sehemu nyingine.

**MHE. SOUD MOHAMED JUMMAH:** Mheshimimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA**: Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. SOUD MOHAMED JUMMAH:** Mheshimimiwa Naibu Spika, ningeomba kumpa taarifa Mheshimiwa anayewasilisha mchango wake sasa hivi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga asilimia 21 ya bajeti yake, katika shughuli za maendeleo. Shughuli hizi mara nyingi zina inategemea miradi kama vile kupitia *ADB, World Bank* na kadhalika, ma-*signatory* ni kutoka Tanzania Bara yani upande wa pili wa muungano. Kwa hiyo tungeomba tu wenzetu waupunguze urasimu ili hii asilimia 21 iliyotengwa iweze kupatikana kwa ukamilifu ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Zahoro endelea.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimimiwa Naibu Spika, namshukuru mwenzangu lakini nadhani ametoka nje ya *point* ambayo nilikuwa naizungumza ninachosema ni hivi;

kwenye mipango yetu kama Jamhuri ya Muungano, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo tunapopanga tuko-*consider* kwamba wenzetu hawa ni *Parten parcel* ya Jamhuri kwa sababu ni vitu viwili.

Mheshimimiwa Naibu Spika, lakini kwa maana hiyohiyo ningeomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha alizungumza hapa kidogo kuhusu uchumi wa *blue;* bado iko haja ya kuzungumza nini maana ya uchumi wa *blue* kwa sababu tulio wengi hatuelewi ni maana ya uchumi wa *blue*. Ningeomba sana wenzetu wa Zanzibar wajitahidi lakini na Serikali ya Jamhuri ielewe kwamba uchumi wa *blue* si kwa maana ya Zanzibar tu hata sisi tunahitaji uchumi wa *blue* kwa upande huu ili uweze kueleweka vizuri zaidi.

Mheshimimiwa Naibu Spika, lakini kwa maana hiyohiyo ningeomba sasa naomba nikipongeze Chama Chetu Cha Mapinduzi, jana kilizungumza haja ya uwepo wa Katiba mpya; naomba nikipongeze sana Chama Chetu Cha Mapinduzi. Kwa sababu hii inatusaidia kuongeza nguvu ya kuonyesha kwamba sote ni watanzania, na tuna nafasi ya kuijenga Tanzania bila ya kujali vyama vyetu na kushirikishana. Hii ni kazi kubwa nakipongeza sana chama chetu.

Mheshimimiwa Naibu Spika, lakini kwa maana hiyo hiyo ningeomba basi; mwaka jana hapa nilizungumza mambo mawili makubwa. Kwanza ni juu ya Bunge kuchukuwa nafasi yake kuisimamia Serikali ili iweze kutekeleza yale ambayo sisi kama Bunge tumeyaamua. Nashukuru sana, Serikali inafanya vizuri sana lakini bado ipo haja ya kuendelea kulisikiliza Bunge kwa yale yote ambayo imeamua na kukubaliana.

Mheshimimiwa Naibu Spika, lakini kwa maana hiyo hiyo kwenye suala la utawala bora ningeomba sana Serikali …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango mzuri muda umekwisha.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:**… Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo, jiandae Mheshimiwa Hokororo, ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimimiwa Naibu Spika, ahsante sana nakushukuru sana na mimi kunipa wasaa huu wakuchangia Bajeti Kuu ya Serikari. Nitaongea mambo matatu; lakini la kwanza ni kuishukuru Serikali kwa miradi ambayo nimepata jimboni kwa mwaka mzima huu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake wote kwa namna ambavyo wanawezesha kupata vituo vya afya, zahanati, shule, maji na barabara hasa zile hasa za *TARURA* kwenye jimbo langu, nashukuru sana.

Mheshimimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niwapongeze Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mkuu wa Wilaya ya Songwe na Mkurugenzi kwa jinsi wanavyonipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu katika Jimbo langu la Songwe. Hata juzi tulikuwa na ziara ya Mkuu wa Mkoa niliongozana nao Ngwala, Guwa, Udinde na Kapalala, tumetembelea na tumekagua miradi ya maendeleo vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niingie kipengele cha kuishauri Serikali, mambo mawili matatu.

`Mheshimimiwa Naibu Spika, cha kwanza; Wilaya ya Songwe sasa ni Wilaya ya Kilimo, ni Wilaya ya Uvuvi wa Samaki Ziwa Rukwa lakini vilevile ni Wilaya ya Madini hasa

madini ya dhahabu. Na kule Ngwala utafiti unasema tuna madini adimu duniani *rare earth*. Madini ya dhahabu maeneo ya Mbangala, Saza Patamela, Mkwajuni na hata maeneo mengine ya makongorosi mpaka Chunya wachimbaji wadogo wanakosa sehemu za kuchimba.

Mheshimimiwa Naibu Spika, kuna leseni zinaitwa *PL (prospecting license)* zimekuwa nyingi sana maeneo za Saza, Patamela, Mkwajuni na Mbangala, kwa hiyo wachimbaji wadogo wanakosa maeneo. Kwa hiyo nilikuwa naishauri Serikali, haya maeneo ya *PL,* wale wote wanaokuja kuwekeza kwa ajili ya utafiti *PL* wakishapata dhahabu, Mheshimiwa wa madini unisikie, naomba itengwe asilimia hata kumi ya yale maeneo baada ya wale jamaa kufanya utafiti. Kwa sababu wao wanakuwa *geology survey,* wakishapata itenge eneo kidogo hata asilimia 10 mpaka 15 kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa maeneo husika, hiyo ndiyo iwe kama *CSR* ya maeneo ya Saza, Patamela, wapate kuchimba.

Mheshimimiwa Naibu Spika, mfano sasa hivi kuna leseni ya Bafex pale Patamela na Saza, wale wachimbaji wadogo hawana kwa kwenda, inakuwa kama vile ni vurugu. Wewe mwenyewe ulishakuja mwaka juzi ukaona unachimba sehemu ya eneo la *Bafex* na lina dhahabu sana lakini lile eneo ukienda kwenye *google* kwenye *portal* linasema *area reverted to the government,* kwa hiyo ni eneo la Serikali. Kwa hiyo nilikuwa nashauri eneo lile wapewe wachimbaji wadogo ili wawe uhuru, na wanaweza wakakata *PML* kama 10 hivi lakini wagawane kwenye yale maduara waweze kuchimba vizuri.

Mheshimimiwa Naibu Spika, na Mheshimiwa Waziri nataka nikuambie, wachimbaji wadogo katika nchi hii maeneo yote ya dhahabu wanaipa Serikali asilimia 38 ya bajeti yote ya Wizara ya Madini. Wizara ya Madini kwa mwaka 2021/2022 mmekusanya bilioni 580 lakini katika hizo bilioni 220 ni fedha zilizolipwa kodi na wachimbaji wadogo tu;

kwa hiyo hawa watu ni lazima wathaminiwe sana. Vilevile maeneo yote ya wachimbaji wadogo hawajafanyiwa utafiti kwa hiyo nilikuwa naomba kitengo cha utafiti pale wizarani *GST* waongezewe fedha weweze kufika na kwenye maeneo yetu ya kule Songwe na Chunya waweze kufanya utafiti.

Mheshimimiwa Naibu Spika, na Mheshimiwa Waziri *GST* hawajapewa bado kibali cha kucholonga ila *STAMICO* wamepewa kibali cha kucholonga naona wanafanya kama biashara, sasa hawa *GST* kwa sababu ni mali ya Serikali waje na kwenye maeneo yetu kule Songwe Saza, Mbangala, Mkwajuni na Patamela waje watusaidie kufanya utafiti wa maeneo yake kuna dhahabu sana ili wachimbaji wadogo waweze kuchimba kwa raha na amani.

Mheshimimiwa Naibu Spika, niende sehemu nyingine ya Wizara ya Elimu, mimi natoa kama ushauri. Kwanza naipogeza sana Serikali. Nadhani Tanzania sasa tumeingie kwenye rekodi ya nchi za kiafrika zakutoa elimu bure kuanzia Elimu ya Msingi mpaka Sekondari, na sasa hivi tumeingia mpaka kwenye *A level*. Mimi kama mwalimu napongeza sana njia hiyo, jambo hili ni kubwa sana, wengine wanaweza wakaona kama ni dogo, lakini ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ushauri wangu, ni nilikuwa naomba mgeukie kidogo na shule *private* mzisaidie, wale wazazi wapewe ruzuku kwa kutokuchangia fedha za baraza la mitihani, ile shilingi 50,000.

Mheshimimiwa Naibu Spika, ni Watoto, kama ambavyo huwa ninasema, kila siku ni watoto wa Watanzania, tusiwatenge sana. Hata kwenye fedha za UVIKO, na ninaomba niseme kidogo, hapa inauma sana. Wale watoto wanaosoma kwenye shule ambazo ni *Non-Government School* hawakupewa chochote kwenye zile fedha za UVIKO. Wale watoto ni wetu, ni wa ki-Tanzania nani alitaka wale watoto wafe kwa ajili ya UVIKO?

Mheshimimiwa Naibu Spika, shule za Serikali zilipewa fedha kwa ajili ya kujenga sehemu za kunawia maji *sanitizer* na mambo mengine, na hata zile shule za *private* na wenyewe walikuwa na mkusanyiko. Ni watoto wetu, lazima tuwajali. Sasa, zikija ofa kama hizi tugawane ile keki ya Serikali, kwa hiyo nilikuwa naomba nyakati nyingine tunapopewa misaada kama hiyo jamani tuangalie na wale Watoto. Mimi huwa ninasema kila siku hapa, Wabunge asilimia 90 hapa watoto wenu wanasoma kwenye zile shule zetu; sasa mlitaka wafe? Hebu mtuambie hapa kama ni nyinyi mlitaka watoto wafe kule shuleni?

Mheshimimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba, Serikali inapogawa ile keki tugawane na sisi tunakula kwenye shule za private ni watoto wa ki-Tanzania. Wote kwa pamoja zile fedha za UVIKO tungepata, hata kama ni milioni mbilimbili kila shule ingesaidia sana kuweza kujenga miundombinu ya kunawa maji, kutokuwa na mkusanyiko na kuongeza madawati katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo wewe ni mdau wa elimu kwa mujibu wa kanuni ya 68 unatakiwa ku.*declare interest* kama wewe una maslahi kwenye shughuli hiyo. Kwa sababu kama ukufanya hivyo kuna mtu anaweza kumuandikia Spika halafu kukulalamikia.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimimiwa Naibu Spika, ahsante mimi ni mwalimu nadecre interest nashauri Serikali kwa nia njema kwamba tunapopata misaada sehemu kama hizo basi tuangalie na hizi Shule za *Private*.

**NAIBU SPIKA:** Ina mambo mengi unatakiwa usema mpaka na pesa unazipata lakini. *(Makofi)(Kicheko)*

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa.

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, upande mwingine wa kuishauri Serikali kwanza nataka niipongeze Serikali Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi kwa kuja na mfumo wa *EPC Plus Finance Engineering Procurement and Construction plus Finance* ni njia ambayo sasa inakwenda kulikomboa Taifa kwenye upande wa barabara. Waheshimiwa Wabunge Serikali pekee haitaweza kujenga barabara ya lami kwenye maeneo yetu kwenye majimbo yetu nchi nyingine za kiarabu wanafanya hivyo ukienda hata Dubai na nashukuru sana hata Serikali ilituma wataalam wakaangalia huo mfumo ni mzuri sana.

Mheshimimiwa Naibu Spika, tunakwenda kuanza kujenga barabara kwa kutumia *private sectors* na hasa barabara za lami kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimuombe Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha; kila mwaka; huu ni mwaka wa 12 mimi niko Bungeni hapa nasema. Nimeomba sana Barabara ya Lami kutoka Mbalizi mpaka Mkwajuni Patamela to Makongolosi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kila siku naongea hapa; kwa nini sisi wengine keki ya Taifa hatugawani kwa pamoja? Kwa nini kila tukija hapa wengine wanapewa barabara sisi wengine hatupewi?

Mheshimimiwa Naibu Spika, nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, unisaidie mwaka huu. Ikija huu mtindo wa *EPC* basi Barabara ya Mbalizi mpaka Mkwajuni iwe ni barabara namba moja ya kuingizwa kwenye huu mfumo ili iweze kujengwa lami. Tayari upembuzi yakinifu umeshakamilika kutoka Mbalizi mpaka Galula na kutoka

Galula Mkwajuni mpaka Makongolosi wanaendelea, wanamaliza mwezi wa tisa. Nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Mwigulu rafiki yangu wa siku nyingi, hebu naomba sasa uweke Barabara ya Songwe iwe ni barabara namba moja.

Mheshimimiwa Naibu Spika, kule kuna madini, kama nilivyosema ya *rare earth*. Kuna madini yamepatikana kule Ngwala hapa Tanzania hayapo, kama vile *tanzanite;* inakuja *tanzanite* namba mbili, ya poko kule Ngwala jimboni kwangu; lakini Serikali kama vile haioni. Hata leseni yenyewe mpaka sasa bado hawajapata. Nilikuwa namuombe Mheshimiwa wa Madini aharakishe mchakato wa kupewa leseni wale watu wa *pick resource*.

Mheshimimiwa Naibu Spika, lakini na Serikali vilevile ione kwamba kule jimboni kwangu kuna mafuta, watu wameshafanya utafiti tayari; kuna mafuta pale Malesa, kuna *helium* kule chini ya Ziwa Rukwa. pia kuna madini na gesi. Maeneo kama hayo lazima wapewe barabara za lami. vilevile kuna kilimo na mifugo. Nnilikuwa naomba mpango huu ukija Mheshimiwa Waziri…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango mzuri kengele ya pili

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Mama yetu kipenzi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa bajeti hii ya kishindo. Bajeti inayojielekeza katika kujenga uchumi ili kukabiliana na umaskini na ukosefu wa ajira. Hongera sana, na sisi Watanzania wengi tunaendelea kuwa na imani na wewe, unaendelea kuipiga mwingi.

Mheshimimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mtwara pia wanaendelea kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais. Kwa uchache sana tumeziona fedha za Serikali ya Awamu ya Sita kwenye maeneo mbalimbali. UVIKO na elimu tumepokea bilioni 11, ukamilishaji wa airport ambayo sasa ndege inaweza kutua usiku bilioni 55, hospitali ya kanda bilioni 15, barabara ya kimkakati, barabara ya uchumi bilioni 268 na mambo mengi mazuri lukuki ambayo yametekelezwa na Serikali ya awamu ya sita hivyo tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye kuishauri Serikali yangu Sikivu. Kama ambavyo imeonekana; bajeti hii ina lengo pia la kuongeza uzalishaji; na hapo naona nishauri kwenye eneo la uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka kuongeza uzalishaji sisi wananchi wa Mtwara zao letu la biashara ni korosho kwa sasa mpaka pale litakapotokea mbadala. Sasa kwenye eneo hili kuna mambo kadhaa ambayo Serikali lazima iongeze usimamizi ama misuli katika kuyatekeleza. Eneo la kwanza ni viatilifu na pembejeo. Kwa sasa viatilifu vya korosho vinaagizwa na vyama vikuu vya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ikiharibu kama ilivyo sasa, kwa miaka kadhaa tumekuwa tukiona viatilifu vya korosho vinachelewa, lakini nimpongeza Mheshimwa Bashe alituahidi mwaka jana kwamba itawahi kuja na kweli imewahi kuja lakini imekuja kwa kiasi kidogo sana. Mpaka sasa tani 4500, iliyokuwa inasubiliwa ni tani 25,000 mahitaji yetu ni tani

45,000 lakini kuagiza vyama vikuu vya ushirika ni tani 45,000. Sasa vyama vikuu vya ushirika haviwezi kuagiza, havina uwezo. Naomba jukumu hili lirudishwe bodi. Bodi wakipewa jukumu hili inaweza kuwajibika. Mkurugenzi atawajibishwa, na Bodi ya Wakurugenzi itawabishwa kuliko ilivyo sasa. Sidhani kama Sheria ya Ushirika Namba 6 kama ina meno ya kuviwajibisha vyama vikuu vya ushirika.

Mheshimimiwa Naibu Spika, lakini eneo la pili ili kuongeza uzalishaji ni kuhusu Sheria ya *Export Levy*. Kwa sasa asilimia 50 inakwenda mfuko wa kuendeleza mazao na 50 inakwenda Mfuko Mkuu wa Serikali. Naomba sana Kaka yangu Bashe, mpiganaji ambaye tunaamini atatuletea mapinduzi makubwa kwenye sekta ya kilimo; asilimia hizi sasa irudi kwenye ile ya zamani. kwamba asilimia 65 iende Bodi ya Korosho ikatekeleze majukumu yale yaliyokuwa yameainishwa kwenye hiyo sheria iliyoianzisha na ambayo ni kuhakikisha tunapata viatilifu na pembajeo za korosho, kufanya utafiti, kupata miche ya korosho na kuhakikisha korosho tunatunza kwenye maghala yaliyo salama.

Mheshimimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu gani, hii *export levy* kw asana kule inakokwenda hatusema kwamba itapotea lakini tunajua wizara ina mzigo mkubwa sana. Na kwa sababu Sheria ya *Export Levy* iko kwenye zao moja tu la korosho. Je, itatekeleza yale matakwa? Ikitokea viwavi jeshi sasa hivi wizara inaweza ikachukuwa irudishe kule Bodi ya Korosho lakini Wizara iongeze misuli ya kuisimamia ili kuona kwamba hiyo fedha inatumika katika kuendeleza zao la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa fedha, na yale mapendekezo yake ya Muswada kwenye *Finance Bill* inasema, fedha hii kwa sasa itafanya kazi mbili tu; ya viwatilifu na utafiti. Hizi kazi nyingine tatu zilizobaki nani atafanya? Kwa hiyo, naomba turudi

kwenye misingi ile ya sheria ya awali, ikafanye zile kazi nyingine ambazo tulizikusudia kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuongeza thamani ya mazao. Nimeiona bajeti ya Wizara ya Fedha imepata fedha nyingi mara dufu kutoka Shilingi bilioni mia mbili mpaka mia tisa na kitu. Ni fedha nyingi imeongezewa, lakini tuna sababu sasa ya kuhakikisha tunaongeza thamani ya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba viwanda vya korosho vile vilivyokuwa vimekufa, ambavyo vilibinafsishwa, wale wawekezaji hawajaanza kuvifanyia kazi yoyote. Naiomba Serikali yangu kupitia Hazina, hivi viwanda sasa vipewe wawekezaji wengine ili vifufuliwe na viweze kufanya kazi yake, tuweze kuuza korosho yetu ambayo itakuwa na thamani kubwa, badala ya sasa ambapo kilo nne inaingia kwa kilo moja, na mkulima haoni manufaa yake kama tutakuwa hatujaongezea thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kabisa kwamba bajeti ya kilimo imeongezwa ili kuweza; kwanza, kuongeza uzalishaji wa mazao yote ili yaweze kututosheleza sisi ndani ya nchi na pia tuweze kupata fedha za kigeni. Kupata fedha za kigeni inatulazimu kwanza kuhakikisha viwanda vya ndani vinakuwepo na vinafanya kazi; pili, kuhakikisha tunayo masoko ya kuuza hayo mazao ambayo tutakwenda kuyazalisha; na tatu, kuhakikisha tunayo miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye eneo la miundombinu na hasa kwenye reli ya kusini. Mipango iliwekwa vizuri, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango aje atuambie hapa, hivi ule Mpango wa Maendeleo ya Kusini *(Mtwara Development Corridor)* umefikia wapi? Naomba Serikali ifufue huu mpango kwa sababu mle ndani kuna reli ya kusini; ile reli ya kutoka Mtwara

- Mbambabay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma. Huu mradi ukitekelezwa, zile fedha zilizowekezwa na Serikali kwenye bandari pale, ile shilingi bilioni 157.8 tutaona tija yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Bandari ya Mtwara haifanyi kazi kwa sababu haijaunganishwa. Ni muhimu reli ya kusini, ya Mtwara - Mbambabay ianze kujengwa, ifanye kazi na pia itakuwa na maslahi mengine. Kule Bandari ya Mbambabay tunaweza tukafanya biashara na jirani zetu wa Malawi, tuta-*connect* pia na jirani zetu wa Msumbiji. Mizigo yote sasa itakuwa inakuja kupitia Bandari ya Mtwara. Nafikiri tutaweza kusafirisha Chuma na makaa ya mawe kama ambavyo ilivyokusudiwa kutoka awali. Hivyo vitakuwa vyanzo vya mapato vya uhakika kwa upungufu ambao tunao.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Hokororo kwa mchango mzuri. Ni kengele ya pili.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, orodha niliyoletewa hapa yote imekwisha na sasa ni upande wa Serikali, Mawaziri wataanza kujibu na baadaye mtoa hoja atakuja kufanya majumuhisho. Mchana huu itakuwa ni majumuisho na jioni itakuwa kipindi cha kupiga kura tu.

Nachukua nafasi hii sasa kumwita *Right Honorable Dr. Tulia Ackson,* Spika wa Bunge la Tanzania kuja kuendelea na shughuli hapa. *(Makofi)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Tutaanza na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Adolf Faustine Mkenda na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa nianze kwa kuishukuru Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Mwanamke mahiri sana jemedari na sio mwingine, ni Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Tunashukuru sana kwa miradi yote ya maendeleo ambayo tulipatiwa ndani ya Jimbo la Momba. Hakika kwa niaba ya wana Momba nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa dhati kabisa moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa namna ambavyo anaendelea kujituma, na bajeti yake ambayo ameiwasilisha Mezani. Naomba kusema kwamba kuwasilisha bajeti ni jambo moja na utekelezaji ni jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, kile ambacho mmekiwasilisha, kama mtaenda kukisimamia vizuri pamoja na Wizara zote za kisekta, ni kweli tutaweza kusema, bajeti hii itaenda kuwafaidisha Watanzania kwa ujumla. Kupitia nafasi hii niongelee lile suala la watoto wa *form five* na *form six* kuondolewa ada.

Mheshimiwa Spika, tuliona, ambapo tulipata elimu bila malipo kutoka shule ya msingi mpaka *O' Level,* kiukweli ilikuwa haitii moyo, kwnai michango ilikuwa mingi na ile dhana ya Serikali kuonesha imetusaidia ilikuwa inaondoka. Matumaini yalikuwa yanaondoka kwa Watanzania kuona kwamba ni kama wameondolewa ada tu, lakini michango mingine imekuwa lukuki. Kwa hiyo, naendelea kuiomba Serikali yangu, kama tumekubali kufanya elimu bila malipo,

vile vitu vyote ambayo tunabeba *content* ya kufanya mzazi asiendelee kuchangishwa, basi Serikali iwekeze kwenye eneo hilo ili hii kauli iweze kuthibitika kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusiana na asilimia 10, naomba ifike asilimia 15.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye masuala matatu. Natamani kuishauri Serikali kuona mwisho wa bajeti hii ndiyo mwanzo wa bajeti nyingine. Tuone ni namna gani ambavyo tunaweza kuhakikisha tunaongeza mapato ili wakati mwingine tupunguze hata utagemezi wa vitu vingine, mapato yatoke kwenye vyanzo vyetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwamba kwenye bajeti kuu, Wizara ya kilimo imeongezewa bajeti zaidi ya mara mbili kutoka kwenye bajeti yake ambayo iliisha kwenye mwaka huo tulionao, lakini kama tunavyojua, wakulima wengi wa nchi hii wanatoka vijijini. Wakulima wengi wa nchi hii ni watu wa kawaida kabisa na kilimo ndiyo jambo peke yake ambalo mtu yeyote ambaye wala hajaenda shule anaweza akafanya bila kushinikizwa kwa ajili ya kujitafutia kipato. Ila kilimo cha nchi hii hakileti tija pale ambao miundombinu ya wakulima kule kijijini walipo ni mibovu. Hawajatengenezewa mazingira mazuri kuhakikisha mazao yao yanapata thamani. Hapa nataka kuongelea miundombinu.

Mheshimiwa Spika, barabara zetu za vijiji Tanzania nzima, zimekuwa siyo rafiki. Hapa tunaendelea kuishukuru Serikali kwa ongezeko la mwaka uliopita kwamba *TARURA* iliongezewa kipato kwa kiasi fulani, lakini wakati Waziri wa Uchukuzi alipokuwa anahitimisha bajeti yake hapa tuliona changamoto ambayo ilikuwepo kwa Wabunge waliokuwa wanalilia barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba sana Mfuko wa Barabara *(TARURA)* uongezewe bajeti. Barabara za vijijini

bado siyo rafiki, bado hazimpi mkulima tija. Pamoja na kwamba Wizara ya Kilimo imeongezewa bajeti mara mbili lakini bado mkulimwa huyu ameendelea kubaki masikini na mnyonge kwa sababu wale wachuuzi ambao wanaenda kununua mazao kijijini wanalazimika kujipangia bei wanavyotaka, wanakuwa ni *monopoly* kutokana na wao kuwa na mazingira magumu ya kutoa mazao kutoka kwenye maeneo magumu kuyapeleka mijini. Tunaomba mtusaidie sana kufungua barabara za vijijini na madaraja Viteputepu.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri natolea kwenye jimbo langu. Najua inaweza ikawa ni Tanzania kote. Kuna vijiji vinaitwa Sanja, Kaonga na Chuo; watu hawa toka wamezaliwa kwenye Tanzania hii hawajawahi kuona gari, kwa sababu hakuna daraja, wametengwa wakati wote, lakini watu hawa ndio wanalima mpunga kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, wakati wote wafanyabiashara wanapoenda kule, wanajipangia bei wanavyotaka. Ni lazima tuwekeze kwenye barabara ili mkulima apate tija. Tutajenga nchi hii pale ambapo mwananchi wa kawaida atajitengenezea kipato chake yeye mwenyewe kutoka kwenye mfuko.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusiana na teknolojia. Mheshimiwa Waziri nataka ku-*quote* kidogo kutoka kwenye bajeti yako kwenye kipengele cha 24 ukurasa wa 19, unasema hivi; "Mheshimiwa Spika, napenda kupendekeza matumizi ya mfumo wa TEHAMA iwe chaguo namba moja katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kubana matumizi. Kuanzia mwaka ujao wa fedha Ofisi za Serikali zianze *paperless operation* kwenye shughuli zake. Kila shughuli zifanyike kwa mtandao. Mbona Bunge wameweza?"

Mheshimiwa Spika, nataka kukwambia kitu Waziri kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. Hiki kitu ambacho unakipendekeza kwa watu ambao tupo kwenye ulimwengu wa teknolojia tunaita ni mambo ya *web one*. *Web one* ni teknolojia ambayo iliishia mwaka 2002 kutumika, sasa hivi

kwenye ulimwengu wa teknolojia, tupo kwenye teknolojia ambayo inaitwa *web three*.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema nini na kumaanisha nini? Tafsiri yake ni kwamba, hatutaki kukumbatia teknolojia, wakati wote tumeendelea kusubiri teknolojia ituache ndipo tuendelee kuambatana nayo. Ni wakati muafaka kwenye Wizara yako kama Waziri wa Fedha na Mipango, katika mipango ya nchi ni lazima uweke kitengo cha *Research and Development* kwenye masuala ya teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri sasa hivi kwenye deni letu la Taifa yapo baadhi ya madeni ambayo Rais wa Awamu ya Sita anayalipa, lakini yalikopwa na Baba wa Taifa. Nataka kusema nini? Mfano, sasa hivi wewe una miaka 52, mimi nina miaka 32; miaka 20 inayokuja, nafasi uliyokalia wewe sisi vijana wa umri huu ndio tutakalia hiyo nafasi yako. Sasa ni lazima mtengeneze mazingira ambayo itafika kipindi sisi ndiyo tutabeba madeni ambayo Serikali inayo. Sasa kama hatutaki kuendana na ulimwengu tulionao sasa hivi kwa sababu sisi siyo kisiwa, hatujajitenga na Mataifa mengine; kwa hiyo, kama tupo pamoja na Mataifa ya wenzetu ni lazima tuendane na *speed* ya dunia ilivyo.

Mheshimiwa Spika, karne hii ya 21 tuliyonayo ni ya viwanda ambayo tunasema ni ya mapinduzi ya nne ya viwanda *(fourth industry revolution)*. Katika mapinduzi ya nne ya viwanda, huwezi kukwepa kama *web three*. Kwa hiyo, sasa hivi dunia ipo kwenye *web three,* lakini nchi yetu inaongelea mambo ya *web one, web two*. Ukitaka ufafanuzi zaidi kwenye hayo mambo, nitakujulisha utakapokuwa umeandaa ya mambo ya *research and development* kwenye Wizara yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine hapo hapo kwenye teknolojia, nitolee mfano wa *Royal Tour* ya mama. Ni kweli *Royal Tour* ya Mheshimiwa Rais imeongeza ufanisi sana katika

kuwavutia sana watu kutamani kuja kutembelea kwenye nchi yetu, lakini kuna kitu tumekosa hapa. Tungekuwa tumetumia teknolojia, kuna kitu kinaitwa *non fungible token* ambayo tunaita *NFT* kwenye ulimwengu wa teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kama kwenye *Royal Tour* ile ya mama tungetumia *NFT,* achilia watalii kuongezeka kwenye nchi yetu, lakini ingekuwa imetuingizia zaidi ya fedha hata trilioni, lakini mambo haya Serikali haiyajui, na Serikali haitamani kutaka kujifunza zaidi. Sasa sisi vijana wa Taifa hili ambao tunawategemea, miaka inayokuja watatokea Mawaziri Wakuu, na Mawaziri wa Fedha kama wewe, ndipo tutaendelea kuijenga hii nchi? Tunawapa mpango wa sasa ambao miaka 20 inayokuja tutatamani kuona mambo haya kwenye Serikali. Chukulia kwenye teknolojia tungeajiri vijana wengi sana. Matajiri wote…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagong. Ahsante sana.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Fedha kwa kutoa Bajeti ya mwaka 2122/2223 kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mwigulu Nchemba pamoja na Naibu wake

Mheshimiwa Chande na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, mimi nichangie sekta ya elimu; napenda kuishauri Serikali kuhusiana na ukusanyaji wa kodi napenda kuwepo na semina au makongamano elekezi kwa walipa kodi wetu kwani wengi walikosa elimu ya juu ya ulipaji kodi na umuhimu wake na yanasaidia sana wafanyabiashara kulipa kodi bila kulazimishwa kwani tayari wanakuwa wamepata elimu juu ya was kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, pia wafanyabiashara wanahitaji kuelewa na kuelimishwa zaidi juu ya umuhimu wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu bure kwa kidato cha tano na sita naunga mkono kwa asilimia zote na naipongeza Serikali kwa huruma hizi kwa wananchi wetu, lakini naiomba Serikali iangalie namna bora ya michango mingine kupunguza mashuleni kwani ipo michango ambayo ni zaidi ya ada wazazi wanalipa hapo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli ada itafutwa lakini michango inakuwa inaongezeka zaidi huko mashuleni. Naishauri Serikali kuona namna bora ya kusimamia michango isiwe mingi mashuleni bado Watanzania wengi wanaumizwa na suala la michango.

**MHE. ZUBEIDA KHAMIS SHAIB:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia afya njema na uzima. Pia nikupongeze wewe na wasaidizi wako wote kwa kuendesha vikao kwa uadilifu na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kabla kutoa mchango wangu au ushauri wangu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa

kwa uongozi wake uliotukuta na wenye matokeo chanya kwa Tanzania. Mwenyezi Mungu amjaalie kheri na mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Spika, pongezi pia kwa uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na watendaji wake wote.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni nzuri na kama itasimamiwa na kutekelezwa kwa umakini tutafikia malengo tuliokusudia. Mheshimiwa Rais ameifungua nchi yetu kiuchumi na kidiplomasia kupitia nyanja tofauti ikiwemo ziara zake kwa Mataifa tofauti, lakini zaidi filamu yake ya *Royal Tour*. Hakika matokeo ya filamu ya *Royal Tour* tumeanza kujionea mara tuu baada ya uzinduzi wa filamu hiyo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta tunazozitegemea katika kukuuza uchumi wa Taifa letu kwa asilimia kumi na saba, filamu ya *Royal Tour* ina mchango mkubwa sana kuinua sekta hii; kwanza kuvitangaza vivutio tofauti tulivyonavyo Tanzania. Mfano, wanyama, mbuga, Mlima Kilimanjaro na kadhalika; pili, kuutangaza utamaduni wa Mtanzania; na tatu, kutangaza fursa za uwekezaji nchini hasa katika sekta ya utalii. Mfano, uwekezaji wa ujenzi wa mahoteli nchini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuiongezea fedha sekta ya kilimo; sekta ya kilimo inapunguza ukali wa upungufu wa ajira kwa rika tofauti, lakini pia sekta hii inachangia sana kukuuza uchumi wa Taifa letu. Lakini pia Taifa lolote duniani ni muhimu sana kuwa na uhakika wa chakula cha kutosha muda wote, sasa kwa mantiki hii naipongeza Serikali kwa kuipa nguvu sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, uhifadhi wa mazingira ni jambo muhimu sana kwa ustawi mzuri wa nchi yoyote duniani. Uchafuzi wa mazingira unachangiwa au unasababishwa na vitu vikuu viwili; moja matumizi ya shughuli tofauti

zinazofanywa na binadamu ambazo ni za kiuchumi na kijamii; lakini pili mazingira yanaharibika kutokana na mabadiliko tabianchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri yote hayo lakini ninaishauri Serikali kuboresha miundombinu tofauti hasa ya barabara katika sehemu muhimu kwa shughuli za kiuchumi kwa mfano katika mbuga zetu, hifadhi na kadhalika. Aidha, utanuzi wa viwanja vya ndege tofauti ili kurahisha shughuli za utalii , biashara na usafirishaji.

Mwisho kabisa nachukua fursa hii kuvipongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kudumisha amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana na naomba kuwasilisha.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nianze na pongezi; napenda kuwapongeza kwa bajeti nzuri ambayo kwetu sisi watu wa Mafinga ambao kwetu misitu ni maisha na ni uchumi itasaidia sana kusisimua sana uchumi na kuongeza mapato ya mtu mmoja mmoja, Halmashauri na Taifa kwa ujumla. Kuondolewa kwa *VAT* kwenye miti - *standing trees,* na kupunguzwa *cess* kutoka 5% hadi 3% ni jambo la kupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuondoa ada mpaka kidato cha sita ni jambo jema sana.

Pia kumuongezea fedha *CAG* na Mkaguzi wa Ndani ni jambo muhimu sana, hasa kwa Mkaguzi wa Ndani ambaye kwa mwaka huu amefanya kazi kwa 20% tu, tukiweza kuimarisha ofisi kifedha na kimuundo itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 100 kipengele cha (vi) kuhusu kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji kwa hisa

ambazo Serikali itakuwa sehemu ya umiliki kama ilivyo kwenye zile za madini 16% ni hatua njema sana.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwanza madeni kwa *suppliers* wa nguzo za umeme; tumetenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya madeni ya wakandarasi. Ninaomba malipo kwa wazalishaji wa nguzo ambao wanadai malipo kwa muda mrefu sana, kutolipwa kwa watu hawa kunaathiri mnyororo mkubwa wa ajira, kuanzia mwenye shamba, vijana wanaomenya nguzo, wanaopakia, wanaosafirisha na kadhalika. Naomba watu hawa walipwe ili waweze kuwalipa watu wanaowadai vikiwemo vituo vya mafuta na wajasiriamali wadogo wanaonunua nguzo kwa wakulima binafsi.

Kuhusu kufanya biashara kwa saa 24; katika ukurasa wa 35 wa hotuba ya bajeti imeeleza kwamba tukiwa na viwanda vijana watafanya kazi saa 24 kwa siku saba. Nashauri iwe ni sheria au kanuni, naomba miji kama Mafinga ambayo kwanza iko kando ya *highway* turuhusiwe kufanya biashara saa 24, hii itasaidia kuongeza mapato ya *individual, LGA* na Serikali Kuu. Kazi ya Serikali/dola duniani kote ni ulinzi na usalama, kisha *welfare*, hivyo ili kuboresha *welfare* acha watu wafanye biashara kwa saa 24, miji kama Chalinze, Mikumi, Ruaha Mbuyuni, Mafinga, Makambako, Igawa na kadhalika kwa barabara ya *TANZAM* au miji kama Korogwe, Mombo, Himo na kadhalika tuweke utaratibu rasmi iwe wa kikanuni au sheria, kuliko ilivyo sasa kwamba leo akija *DC* au *OCD* muelewa watu wanafanya biashara, akija asiyekuwa muelewa biashara zinafungwa saa nne usiku. Hivi Mji kama Mafinga ufunge biashara saa nne, unajenga uchumi au unadidimiza/ Ndio maana naomba iwe rasmi kama ni sheria au kanuni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupunguza *palm crude oil* kutoka 25% hadi 0% kwangu ni *no*. Pamoja na hoja kwamba hii itasaidia kupunguza bei ya mafuta ya kula na kuongeza

ajira ya vijana kwa kuchakata mafuta, tukiwa na dhamira huru *with honest opinion* jambo hili linaenda kunufaisha watu wachache wakiwemo wafanyabishara wakubwa na baadhi ya wafanya maamuzi na sababu ziko wazi, kwanza hao jamaa watasingizia kuwa wameingiza *crude* lakini ukweli watakuwa wameingiza *refined,* hoja ya sijui tutaongeza ajira ni Sanaa, hakuna uhalisia *and we all knows that*. Tuwe wakweli ndugu zangu, hata tulipotoa ile shilingi 100 ya *REA,* je, mtumiaji wa mwisho ali-*feel any relief?* Ukweli ni kuwa hakuna.

Kwa hiyo, kwenye hili jambo ndugu zangu *from 25% to 0%!!!!* Labda kama tunaamua sasa katika mafuta ya kula tumeamua kuwa Taifa la wachuuzi. Ushauri wangu, kama nia ni hii *as we are saying* kupunguza ukali wa bei na kuongeza ajira, na kwa kuwa viwanda vya ndani havijawa na *capacity* ya kutosha, iwe walau kati ya 15% au 10%.

Mheshimiwa Spika, mgao wa 10% ya *own source* kujumuisha wamachinga; kwa sisi tunaotoka maeneo ya mijini kama Mafinga, jambo hili ni hatua muhimu sana, hata hivyo kila kundi tungewapunguzia 1% kwa maana ya ile 4+4+2 sasa iwe 3+3+3+1 (wanawake +vijana + machinga +watu wenye ulemavu).

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo na misaada (mabadiliko ya tabia nchi na mradi wa *REGROW;* bajeti yetu kama niko sahihi karibu 32% inategemea mikopo na misaada, *that being the case* ni muhimu sana kuchangamkia fursa ambazo ni *grants*, kwa mfano kuna fedha nyingi sana katika suala zima la namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, lakini sisi kama Taifa wala hatujachangamkia fursa hii zaidi ya CRDB na baadhi ya miradi na kimsingi ili ku-*access* hizi *funds* lazima upate *accreditation* ambayo wenzetu nchi kama Kenya kuna zaidi ya taasisi kumi na nane, sisi ziko mbili tu CRDB na *NEMC*. Nashauri tuchangamkie fursa hii na fedha hizi zitasaidia kupunguza makali ya athari za

mabadiliko ya tabianchi kwa kuelimisha wananchi kupanda miti, kujenga miradi ya umwagiliaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, *REGROW* ni mradi wa usimamizi wa maliasili na kuendeleza utalii Kanda ya Kusini; mradi huu ambao ni mkopo wa *World Bank* wa dola milioni 150 ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais, Mkoani Iringa tarehe 12/2/2018 na mpaka kufikia mwaka huu wa 2022 ilipaswa kiasi cha dola milioni 111 ziwe zimeshatumika. Hata hivyo utekelezaji umekuwa wa kusuasua sana, moja ya lengo la mradi huu ni pamoja na ku- *upgrade airstrips* 14 katika Hifadhi za Taifa za Mikumi, Ruaha, Selous na kadhalika, ujenzi wa barabara za kilometa 2051, kuboresha njia za utalii za miguu za kilometa 132, kutoa mafunzo ya ujuzi kazi kwa wananchi wanaozunguka hifadhi ikiwa ni pamoja na elimu ya uhifadhi ili kuleta ushiriki wa jamii hizo katika sekta ya utalii. Vijiji 61 na zaidi ya Kaya 40,000 zingenufaika na mradi huu. Kwa ufupi mradi huu ungeboresha mazingira ya sekta ya utalii na hivyo kuongeza mapato; pili huu ni mkopo, tunapochelewesha utekelezaji tunachelewa kupata *returns,* tunajiumiza wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ya Fedha ifuatilie kujua kama kuna vikwazo vitatuliwe, kama ni uzembe ijulikane, kwa mujibu wa kalenda mradi huu unapaswa kukamilika mwaka 2023 japo nasikia wame-*extend* muda.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, kutokana na muda wangu kuisha, naomba mchango wangu uliobaki niulete kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nikianza na mikopo ya magari kwa watumishi; gharama kubwa za matumizi ya Serikali kwa magari chanzo kikubwa ni taasisi ya Serikali *(TEMESA),* si kwamba watumishi wanatumia magari vibaya. Na Sheria ya

Manunuzi inataja kabisa lazima magari ya Serikali yatengenezwe *TEMESA*. Sheria hii iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, gharama ya kutengeneza gari *TEMESA* na *garage* ya mtu binafsi ni mara tatu; kwa mfano gharama ya matengenezo ya kawaida *(service)* kwa gari ni shilingi milioni 1.5 wakati *garage* binafsi ni shilingi 350000. Taasisi hii iangaliwe upya, tunapoteza fedha nyingi kwa kulipa watumishi ambao hawana tija yoyote. Taasisi hii imekuwa ni hasara kwa Serikali. Serikali ijikite kuangalia huduma hata *garage* binafsi.

Mheshimiwa Spika, nijikite kwenye *GePG*, mfumo huu umekuwa mkombozi kwa kukusanya maduhuli, umewezesha kukusanya shilingi trilioni 2.03 hadi shilingi trilioni 3.05 hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha kutoka shilingi bilioni 800 kabla ya mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu umetengenezwa na watumishi wetu wa Kitanzania, watumishi hawa waangaliwe na kuwezeshwa kuongeza ujuzi wao, maslahi yao na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nchi zingine hawa watumishi hawajulikani wanapofanyia kazi wala wanapoishi, ili wasije wakarubuniwa. Niombe Wizara ya Fedha na Mipango iwaangalie kwa maslahi yao na kuwaongezea ujuzi wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na uzima wa afya. Pia naomba kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake uliotukuka kwa maslahi mapana kwa Taifa letu. Cha kumlipa

hatuna zaidi ya kumpatia mashirikiano ya dhati na kumuombea kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kheri, baraka na mafanikio mema zaidi.

Aidha, nikupongeze wewe Spika, wasaidizi wako na watendaji wako wote kwa kuliongoza Bunge kwa ufanisi na umahiri. Lakini pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kuchangia hotuba hii napenda kutoa pongezi kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kulifanya Taifa letu kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, utalii ni miongoni mwa sekta muhimu sana katika kukuunza uchumi wa Tanzania. Sekta hii ina mchango zaidi asilimia 16.9 ya pato la Taifa letu. Kutokana na umuhimu wa sekta hii, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amejitolea mwenyewe kuitangaza Tanzania kupitia filamu ya *Royal Tour*. Baada ya uzinduzi wa filamu hiyo tumeshuhudia ongezeko la watalii nchini pamoja na wawekezaji. Faida za filamu hiyo ni kukuuza pato la nchini, kuongezeka kwa wawekezaji nchini, ajira kwa Watanzania, kuengezeka kwa fedha za kigeni na kadhalika, hivyo Serikali iendeleze juhudi alizozifanya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania. Naipongeza Serikali kwa kuiongezea fedha sekta hii na tunaimani itasaidia kukuuza uchumi wa Tanzania, lakini pia ustawi mzuri wa jamii na nchi yetu kwa ujumla. Chakula ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Kuna faida tofauti zinapatikana kupitia sekta hii nazo ni afya bora, ajira kwa Watanzania, biashara za ndani na nje ya nchi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sekta ya miundombinu ni jambo muhimu sana kuweza kufanikisha malengo ya bajeti hii ya mwaka 2022/2023. Naipongeza Serikali kwa kuboresha miundombinu tofauti zikiwemo barabara, viwanja vya ndege, miundombinu ya maji, umeme na kadhalika, hivyo naishauri Serikali kuendeleza uboreshaji wa miundombinu katika sehemu zenye kuchangia ukuaji wa uchumi wa Tanzania, mfano ni hifadhi zetu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, aidha natoa pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuboresha mahusiano mema na mataifa tofauti. Mahusiano mema na mataifa mengine tofauti ni sehemu inayotoa fursa kwa baadhi ya sekta za kiuchumi ikiwemo biashara, utalii na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano kati ya SMT na SMZ ni jambo muhimu sana, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale sio za Muungano, lakini ukiwepo ushirikiano kwa Wizara hizo kutasaidia sana kuongeza idadi ya watalii na kutangaza vivutio vivyopo Zanzibar na Tanzania Bara. Hii itapelekea kukuuza uchumi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa mazingira ni jambo muhimu sana, kuna njia mbili kuu za uchafuzi wa mazingira nazo ni mabadiliko ya tabianchi na pili ni uchafuzi unaotoka na matumizi ya mkono wa binadamu kwa shughuli za kiuchumi ikiwemo mifugo, kilimo viwanda na nyingine matumizi ya sheria ikiwemo utupaji wa taka kiholela. Hivyo basi nashauri Serikali iliangalie suala hili la kutunza mazingira kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Spika, namaliza kwa kuunga mkono hoja iliyowasilishwa kwa asilimia mia. Ahsante sana.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha ubunifu wa ukusanyaji mapato na usimamizi mzuri wa matumizi ya Serikali ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa miradi ya kimkakati na pia utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imesimamia kwa ufanisi ukusanyaji mapato na utekelezaji wa miradi mingi ya miundombinu ya barabara, reli, bandari na kadhalika. Napongeza Serikali kwa mwendelezo mzuri wa utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa umeme Mto Rufiji. Mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* pamoja na uboreshaji wa bandari utaimarisha kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu. Umeme, reli na bandari ni nguzo imara ya kiushindani katika uchumi wa Tanzania na nchi za maziwa makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki wakati dunia inapambana na janga la *corona virus (covid-19),* tumejifunza umuhimu wa kuwepo kwa mikakati mbadala kutokana na nchi nyingi tunazoshirikiana kibiashara na kiuchumi kukumbwa na mtikisiko wa kiuchumi. Biashara ya usafirishaji hasa wa anga imeathirika sana na napongeza mkakati wa shirika la ndege kuanza kutumia ndege zake kusafirisha mizigo. Mkakati huu ambao umetumiwa na hata mashirika makubwa ya ndege utawezesha usafirishaji wa mazao yetu ya kilimo kufikia masoko kirahisi na hapo hapo uhakika wa mapato kwa shirika la ndege hasa kipindi hiki kukiwa na upungufu wa abiria. Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Msajili wa Hazina anapaswa kuendelea kuimarisha mitaji kwa mashirika ambayo yatachochea ukuaji wa uchumi ikiwemo benki za *TADB, TIB* na *ATCL* ili iweze kusimama kibiashara ikiwa ni nguzo muhimu hata kwa sekta zingine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongezewa mitaji, benki za *TADB* na *TIB* ziwezeshwe kujenga mahusiano taasisi kubwa za kimataifa ili fedha za maendeleo zinazotolewa na taasisi hizo zipitie kwao hasa kwa miradi mikubwa ya kilimo na viwanda ikiwemo uchumi wa bluu. Kwa *ATCL* iboreshe muundo wake wa utumishi kulingana na biashara iliopo ya usafiri wa anga ili kupunguza mzigo wa gharama na kuongeza ufanisi. Pia *ATCL* ianzishe njia za safari za ndani na za nje zenye fursa ya kuongeza biashara, kama vile safari za moja kwa moja za Mbeya – Dodoma, Mbeya – Lilongwe, Mbeya Lubumbashi, na Mbeya – Lusaka.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa maboresho ya uwanja wa ndege wa Songwe na kutokana na maboresho hayo napendekeza kujengwe maghala *(cold rooms)* kwa ajili ya kuhifadhi mboga mboga, matunda, nyama na samaki kwa soko la nje. Uwanja wa ndege wa Songwe upo kimkakati kwa kuhudumia wafanyabiashara wa hapa nchini na pia nchi jirani za Zambia, DRC na Malawi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za ukopeshaji kupitia mabenki kwa wakulima kutoka kwenye Mfuko wa Tanzania Trilioni Moja zilizotolewa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napendekeza mfuko huu utumike pia kwa kutoa dhamana katika uagizaji mbolea kwa lengo la kupunguza bei za mbolea na hata kuwezesha upatikanaji wa mbolea kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iangalie upya mapendekezo kuboresha muundo wa mfuko wa asilimia 10 kwa ajili ya mikopo kwa vijana, wakina mama na makundi maalum. Napendekeza mfuko huu uboreshwe na uwe sehemu ya mpango wa kuwawezesha kiuchumi makundi lengwa kwa misingi ya huduma za kifedha shirikishi *(financial inclusion)*. Msukumo uwe kwenye elimu ya ujasiriamali na kuwasimamia kwa karibu wakopaji ili kuongeza tija na pia kuboresha uchumi wa wakopaji na Tanzania kwa ujumla.

Napendekeza pia kujumuisha huu mfuko uwe kitaifa na uendeshaji uwe katika misingi ya taasisi za kifedha, lakini kwa masharti nafuu ikiwemo bila riba na Serikali iunganishe mifuko yote ya makundi maalum na yaunde taasisi moja imara chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea hata kwa kutafuta vyanzo mbadala vya fedha kugharamia ujenzi huo, kwa vile kutakuwa na fursa kubwa za usafirishaji. Pamoja na ujenzi wa *SGR*, napendekeza kuendelea na kuboresha reli ya *TAZARA* na uboreshaji wa bandari zetu ikiwemo ujenzi wa bandari kavu ikiwemo ya Inyala, Mbeya ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki ili kupunguza gharama za kusafirisha pembejeo na mazao. Serikali ichukue hatua za haraka kuinusuru reli ya *TAZARA* hata ikibidi kurekebisha mikataba ya umiliki na uongozi ili mradi uendeshwe kwa tija. Kuna kuchukua hatua za makusudi kwa kutumia zaidi *TAZARA* kusafirisha mizigo ambayo imeelemea

hata uwezo wa barabara zetu. Usafirishaji wa mizigo kwa kutumia *TAZARA* ilenge kupunguza gharama za pembejeo kwa wakulima na wakati huo kupunguza gharama za kusafirisha mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iwekeze angalau shilingi bilioni 100 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya reli na karakana. Uwekezaji huu utawezesha *TAZARA* kujiendesha kwa faida na kuipunguzia Serikali mzigo wa kulipa zaidi ya shilingi bilioni 15 kwa mwaka ikiwa ni mishahara ya wafanyakazi wa *TAZARA*. Uwekezaji huu unahitajika haraka wakati Serikali za Tanzania na Zambia zinaendelea na jitihada za kurekebisha mikataba ikiwemo wa uendeshaji wa *TAZARA*. Pamoja na kuboresha *TAZARA*, napendekeza kukamilisha taratibu za ujenzi wa bandari kavu ya Inyala, Mbeya ambapo Mamlaka ya Bandari kwa kipindi kirefu wamewahakishia wananchi kulipa fidia ya eneo lao wanalolichukua.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za mapato kutokana na janga la *Covid-19,* kuna fursa nyingi za muda mfupi za kuongeza mapato kupitia hatua za kiutawala ikiwemo ya kuondokana na matumizi na malipo ambayo hayana tija kwa Serikali na hata walipakodi. Kutokana na mahitaji makubwa ya uwekezaji kwenye miradi ya kimkakati, uchumi wetu utaendelea kuwa na mahitaji makubwa ya mikopo ya pesa za kigeni na wakati huo huo kulipa mikopo iliyoiva. Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha mapato ya fedha za kigeni yanaongezeka kupitia mazao ya kilimo, madini na utalii. Kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yatasaidia kuimarisha Deni la Taifa kuwa himilivu na pia kuendeleza utulivu wa shilingi yetu dhidi ya sarafu kuu za kigeni na hata kuhakikisha utulivu wa mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ihakikishe kipaumbele cha kuwekeza kwenye kilimo ikiwemo pembejeo na umwagiliaji

kwa lengo la kuongeza tija na pia kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kulinda mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upotevu mkubwa wa fedha za Serikali ikiwemo miradi ya Serikali Kuu na Halmashauri, napendekeza Serikali kuimarisha kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili kuongeza ufasi na uhuru wa Wakaguzi wa Ndani. Serikali ihakikishe Mkaguzi wa Ndani wakati wote anakuwa huru kutoka kwa Afisa Masuuli. Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri wasimamiwe na Mkaguzi Mkuu wa Mkoa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Serikali iimarishe uhuru wa Mkaguzi Mkuu wa Ndani *(Internal Auditor General)* na hata kupandisha hadhi ya Ofisi kuwa na Fungu la Bajeti linalojitegemea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika maeneo yafuatayo; maji, gesi asilia na mikopo ya wanawake; na nnianze na maji; naipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga Bwawa la Kidunda ambalo litasaidia wananchi wa Dar es Salaam kuweza kupata maji hata wakati wa kiangazi. Kwa kweli Mkoa wa dar es Salaam umekuwa na ongezeko kubwa la majengo ya makazi ya watu na majengo ya biashara. Majengo mengi yaliyopo mjini yanategemea kupata maji kutoka chanzo cha Mto Ruvu. Kitendo cha Serikali kutenga fedha kwa ajili ya mradi huo ni jambo jema kwa maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, gesi asilia; naiomba Serikali iweke fedha kwenye mradi wa gesi za matumizi ya majumbani,

tunahitaji sana iende kwa wananchi mbalimbali katika Mkoa wa Dar es Salaam. Ni vizuri nchi kutumia rasirimali zake katika kujiongezea kipato. Gesi hiyo itakuwa na gharama nafuu lakini pia itaingiza mapato mengi kwa Serikali. Lakini pia kuanza kutumia gesi katika magari kutapunguza matumizi ya mafuta katika nchi yetu.

Kwa upande wa mafuta; naomba Serikali iweke fedha kwa Kampuni ya *TIPER* kujenga *storages tanks* kwa kuhifadhi mafuta ambayo yatasaidia nchi kama nchi pale tutakapopata uhaba na pale ambapo bei zinabadilika kupitia *EWURA*. Wafanyabiashara wana tabia ya kufunga *depot* zao na wateja kukosa mafuta ndani ya vituo vyao, lakini Serikali haitasimamisha biashara; na-*declare interest* kuwa mimi ni mdau katika eneo hilo. Naona changamoto hiyo ni kubwa sana. Ujenzi wa vituo vya TANOIL nashauri Serikali iangalie maeneo yaliyo pembezoni badala ya kuangalia Dar es Salaam ambapo sekta binafsi limebeba eneo kubwa sana.

Kuhusu mikopo, nashauri mikopo ya wanawake , vijana na walemavu ibaki kama zamani kwa uwiano wa asililmia nne, nne na mbili. Serikali ifanye utaratibu wa kujenga masoko kwa wajasiriamali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu kwa njia ya kuzungumza naomba kupitia maandishi niendelee kuchangia mpango wa maendeleo wa mwaka ujao na zaidi na bajeti ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ya Taifa na uhuishaji wa Dira ya Taifa 2025; kwa mipango ya muda mfupi na mrefu lakini kwa matumizi ya rasilimali adimu kwa ufanisi

na tija kubwa ipo haja kurejesha sasa Tume ya Mipango ya Taifa. Pamoja na tume hiyo, naishauri Serikali jitihada za Serikali za uhuishaji wa Dira ya Taifa ya 2025 *(Vision 2025)* zifanyike kwa kuwashirikisha wananchi walio wengi zaidi. Muhimu wananchi wapate taarifa ya nini kinafanyika hatua kwa hatua na ni katika hatua gani wananchi walio wengi watahusika.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa malengo *(targets);* ni ukweli ulio wazi kuwa uchumi wa dunia umechafuka hali inayotulazimu kila shughuli tunayofanya kwa kutumia rasilimali hizi chache tena zinazopatikana kwa shida basi inatoa matunda makubwa. Serikali ya Awamu ya Sita ni dhahiri kwa mipango na matendo yake inajielekeza kwenye sekta za kiuzalishaji ambazo kama inavyoelezwa kwenye Dira ya Taifa ya 2025 zinatuwezesha kujenga uchumi jumuishi. Muhimu hapa ni kuwekeza kwa shabaha maalum ili kila tutakapoweka rasilimali kama nilivyodokeza basi ilipe mara mbili au zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa rejea ya hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 utaona kuwa sekta ya mifugo haikuchomoza katika mazao/bidhaa zilizotuwezesha kupata fedha za kigeni. Mauzo ya nchi kwa mwaka husika ziliingiza takribani dola za Kimarekani bilioni 6.7; madini yakiwa yamechangia dola za Kimarekani bilioni 3.103.17 na utalii nje ya kiasi hicho kilichotajwa ukiwa umechangia dola za Kimarekani bilioni 1.402 ukiwa unapanda kuelekea kiwango chake cha mwaka 2019 kabla ya *Covid-19* yaani dola za Kimarekani bilioni 2604.0.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu hapa ni kuwa Serikali ikiweza kujipanga na kuwekeza kimkakati katika sekta ya mifugo hasa ng'ombe kwa mwaka wa nne toka kuanzisha mradi huu kabambe, mauzo ya wanyama hai na nyama nje ya nchi unaweza kuingiza dola za Kimarekani bilioni 3.5 kwenye uchumi wetu. Kwa dhana ya ng'ombe milioni 35

waliopo sasa nchini, ufugaji wa kisasa unawezesha ng'ombe wa nyama kuchinjwa katika umri wa miezi 18 mpaka 24 hivyo kuchinjwa na kupata angalau tani milioni 1.4 kwa mauzo ya ndani na nje ya nchi. Mauzo ya tani 800,000 kwa bei ya dola 4.4 kwa kilo yanatuingizia kadirio lililotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kufikia ndoto hiyo uwekezaji mkubwa unapaswa kufanyinka. Jambo la kwanza ni kuwashawishi na kuwawezesha wachungaji wa Tanzania kuwekeza katika ufugaji. Ufugaji unaanza kwa kuachana na tabia ya kuhama hama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kutafuta malisho, maji au kukimbia magonjwa na majanga mengineyo. Kama nilivyosema hapa, uwekezaji mkubwa unahitajika lakini haina jinsi kwani pamoja na kuleta faida ya kipato kwa mwananchi na Serikali inasaidia kupunguza migogoro ya ardhi. Kutokana na ukubwa wa gharama, kufuatia uharibifu ambao sekta hii imeishafanya kwa nchi hii, mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Rukwa, Mbeya, Morogoro, Ruvuma, Pwani, Lindi na Mtwara inaweza kuhusishwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyodokeza hapo juu, mpango wa ufugaji ni kuwa *zero grazing* na *semi free range* kwa malengo ya kufuga na kuvuna kwa kipindi kifupi tukilenga tija kubwa. Faida nyingine kubwa ni kulinda mazingira kwa ajili ya kuwezesha mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere kufanyakazi kwa tija kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuwezesha wafugaji kupata wanyama wanaoweza kufugwa na kutoa nyama na maziwa kwa wingi. Hii inaweza kufanyika kwa kuagiza wanyama wengi kama mbegu na kuwasambaza kwa wakulima kwa mpango wa kurejesha baadae wakati wa kuuza nyama/maziwa. Sambamba na mbegu ni uandaaji na upandaji wa malisho yanayoweza kuwezesha wanyama hao kukua haraka na kuwa na uzito wenye faida.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni ujenzi au uimarishaji wa viwanda ili kuongeza thamani ya mazao kuelekea sokoni. Hapa ni kulenga shabaha *(target)* katika kuongeza mapato ya fedha za kigeni. Kwa takwimu na maelezo hayo, nashauri na kusisitiza eneo hili ni mwanya wa kuongeza kipato na ustawi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni mauzo tena *(re-export)* ya bidhaa. Kwa mwaka 2021 eneo hili liliingiza dola za Kimarekani milioni 90 ukilinganisha na vipindi vya nyuma tulipofikia takribani dola za Kimarekani milioni 800. Uwepo wa mafuta katika hifadhi za mafuta chini ya uangalizi wa *TRA (customs bonded warehouse)* ni fursa ya *re-export* kwa kulenga wateja wa nchi jirani ambao hawako tayari kushiriki katika mchakato wa ununuzi wa mafufa kimataifa, kundi hili ni kubwa. Fikiria kama lita takribani bilioni nne inayokwenda nchi jirani, nusu yake kama ikiuzwa toka nchini na kila lita moja ikawekewa *mark up* ni dhahiri *re-export* itachangia pakubwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la kuwekea malengo kwa matokeo ya haraka ni sekta ambazo zinaonekana kukua kwa haraka. Kundi hili ni pamoja na mazao ya mboga na maua, mchele, viwanda, samaki na mazao ya samaki, madini na utalii. Ushauri wangu ni kuwa pamoja na kuendeleza sekta zote nguvu zaidi zielekezwe kwenye maeneo niliyotaja hapo juu na sekta zenye fursa za kukua haraka na kupata soko.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la *target* ni kulenga kujitegemea kwa bidhaa/mazao ambayo yanaweza kuzalishwa hapa nchini. Kama mipango ya Serikali inavyoonesha kuna haja ya kujitosheleza katika kuzalisha mafuta ya kula na sukari bidhaa ambazo tumekuwa tukinunua toka nje ya nchi ilhali tunaweza kuzalisha hapa nchini. Lengo hili linaweza kufanikiwa kwa kuhakikisha wawekezaji wanasimamiwa ili pale ambapo kuna vikwazo kweli viondolewe ili kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na juhudi hizo ni suala la sera au sheria kinzani. Serikali imeamua kuondoa ushuru kwenye *CPO* na kuwa asilimia sifuri, hatua hii itawezesha wananchi kupata mafuta ya bei nafuu. Hoja hapa ni kuwa je, bei ya mafuta yatokanayo na *CPO* na yale alizeti yanaweza kushindana katika soko letu la ndani? Mafuta ya alizeti yana soko kubwa na lenye bei nzuri nje, hoja hapa ni kuwa je, mafuta ya mawese yakiwa na bei nafuu na alizeti zikakosa soko wakulima watakuwa na hali gani? Jambo ambalo linaweza kutokea ni kuwa viwanda vya ndani vya kukamua alizeti vinaweza kudengua na kulazimisha bei ya alizeti ya mkulima ambayo tunategemea kuwa nyingi kushuka.

Mheshimiwa Spika, alizeti ya wakulima katika hali hiyo inaweza kuishia kuuzwa nje ya nchi au wakamuaji wa hapa nchini kununua kwa bei rahisi na kuuza mafuta nje ya nchi kutokana na ukweli kuwa soko la ndani halimudu bei hiyo. Hoja na ushauri wangu ni kuwa tuwe na shabaha mahsusi kwa kila hatua inayochukuliwa lakini pia tuwe na utabiri wa nini kama kuepuka kupata matokeo ambayo hatukutegemea.

Mheshimiwa Spika, tishio la hali ya hewa; Serikali inayo mipango ya umwagiliaji kwa ajili ya utekelezaji kwa mwaka huu na miaka inayofuatia. Nashauri kutokana na hali ya hewa kutokuwa nzuri na kufuatia uhaba wa chakula duniani Serikali haraka ipitie mipango yake. Muhimu miradi ya umwagiliaji kwenye vyanzo vya maji vyenye uhakika itekelezwe mwaka wa fedha tunaojadili bajeti yake. Serikali yenyewe na au kwa kuwahamasisha wawekezaji binafsi wapewe vivutio na kuelekezwa kwenye kilimo cha umwagiliaji. Pamoja na haja ya kupata mapato kwa ajili ya maendeleo suala la baa la njaa ni muhimu kuangaliwa, kuhemea na kuwagawia wananchi chakula ni jambo gumu na lenye karaha.

Mheshimiwa Spika, ruzuku ya pembejeo za kilimo na ufugaji; Serikali ina mipango ya kutoa ruzuku kwa wananchi ili kuweza kuzalisha kwa wingi na tija kubwa. Hili ni wazo zuri na ukweli ni kwamba nchi nyingi ulimwenguni kwa kificho au hadharani hutoa ruzuku kwa sekta za uzalishaji. Ushauri wangu ni kuwa utaratibu maalum ufanyike ili kila anayepewa ruzuku ajulikane, eneo la uzalishaji lengwa na mavuno tegemewa. Kwa hali ya sasa tunao uwezo wa kufanya zoezi hili tukitumia faida ya kiteknolojia. Utaratibu huu utasaidia matumizi mabaya ya fursa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipatia fursa hii ya kutoa mchango wangu katika kujadili hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 na mpango wa maendeleo ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Pili napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi anazozichukua kwa kuendesha Taifa hili kwa ushujaa na umahiri wa hali ya juu. Huyu ni miongoni mwa Marais wa nchi hii walioweza kuonesha dira na matumaini mazuri ya nchi yetu.

Tatu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwakilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; nikianza na masoko ya mazao kwa wakulima nchini.

Mheshimiwa Spika, wakulima wetu katika nchi hii wanafanya kazi kubwa ili kujipatia mahitaji na maendeleo ya Taifa letu. Wanafanya kazi usiku na mchana kwa kutumia nguvu kubwa sana. Lakini juhudi zao zinakatishwa tamaa kutokana na hali ya masoko nchini hasa katika maeneo yao ya wakulima. Aidha, upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati pia ni tatizo kubwa kwa wakulima wetu. Wakulima wanapokamilisha utayarishaji wa mashamba yao wanashindwa kupata pembejeo za kilimo hali inayopelekea kupata hasara kubwa na kushindwa kufikia malengo yao.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kujitahidi kutumia uwezo wake wote ili kuondosha kabisa matatizo ambayo yapo ndani ya uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mkopo wa fedha za *covid;* nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uthubutu wake huu wa kutafuta na hatimaye kuupata mkopo huu ambo ni mkombozi mkubwa kwa maendeleo ya Taifa letu. Nchi nyingi ulimwenguni zimekosa fursa hii lakini sisi kwa juhudi za Mheshimiwa Rais tumebahatika kuupata. Wajibu wetu sisi wananchi ni kuutumia mkopo huu kwa hadhari kubwa ili tufike malengo yaliyokusudiwa. Kila mwananchi wa nchi hii ana wajibu wa kuona kuwa fedha hizi ni zake, zinamhusu katika kuzitunza na kuzitumia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makundi ya uzalishaji; mpango wa maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umeyataja makundi kadhaa ya uzalishaji katika nchi yetu. Miongoni mwa makundi hayo ni pamoja na wavuvi, wakulima na wajasiriamali. Lakini katika mpango haukueleza kwa makini makundi hayo yatakavyofaidika, bado makundi haya hayaelewi namna watakavyohusishwa na mpango huu ambao umewataja.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali katika jambo hili ni kujitayarisha kushuka kwenye makundi hayo ili kuwaelimisha kwa urefu na umakini mkubwa namna watakavyofaidika na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa maandishi kuhusu hotuba ya bajeti ya mwaka 2022/2023 iliyosomwa kwa ustadi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Nchemba, utajikita katika maeneo makuu mawili; sekta kuu za uzalishaji mali hasa kilimo, uvuvi na mifugo na sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, nianze na sekta za uzalishaji mali; kwa kuwa lengo kuu la mpango wa maendeleo wa miaka mitano 2021/2026 ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu, kufikiwa kwa lengo hili kunategemea sana ukuaji endelevu wa sekta za kilimo, uvuvi na mifugo. Ni dhahiri kwamba ongezeko kubwa la bajeti ya mwaka huu wa fedha katika sekta hizi za kimkakati kwa maendeleo ya kiuchumi ya Taifa letu ni ushahidi wa wazi kwamba Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imedhamiria kwa dhati ya kujenga uchumi wa kitaifa unaowanufaisha Watanzania wengi kupitia sekta hii. Utashi huu wa kisiasa wa Mheshimiwa Rais Samia unastahili kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, kupitia hotuba za kisekta (kilimo, uvuvi na mifugo) na hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali, kuongezeka kwa bajeti ya Serikali kwenye sekta hizi za uzalishaji mali kunatarajiwa kuwa chachu ya kuongezeka kwa tija katika uzalishaji na hatimaye kutoa mchango mkubwa katika kuongeza mapato ya wananchi na Serikali, kuongeza kasi ya kupatikana kwa ajira, kuongeza kiwango cha malighafi za viwandani, kuongeza mauzo nje ya nchi na hivyo

kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kuongeza kiwango cha uhakika na usalama wa chakula hasa mazao ya nafaka (ngano, mchele na mahindi) mazao ya mafuta ya kula (alizeti, michikichi) na sukari.

Mheshimiwa Spika, kwa manufaa yatokanayo na sekta hizi, bila shaka sekta hizi ndizo roho ya uchumi, uhuru na usalama wa Taifa letu. Kwa hiyo, uamuzi wa Serikali wa kuongeza bajeti kwenye sekta hizi ni uamuzi muafaka kabisa kwa mustakabali mwema wa Taifa. Hata hivyo, nashauri, Serikali iendelee kuongeza bajeti ya sekta hizi mwaka hadi mwaka, hasa kwenye maeneo yatakayokuza tija na kuongeza thamani ya mazao kwenye sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyobainishwa kwenye hotuba za kisekta na bajeti kuu, maeneo yaliyowekewa mkazo kwa ajili ya kuongeza tija na ufanisi katika sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi ni ujenzi wa miundombinu mipya ya umwagiliaji, kupanua upeo wa utafiti na uzalishaji wa mbegu bora, Serikali kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wazalishaji, kuwawezesha wazalishaji kimtaji na kiteknolojia kupitia watu binafsi na vyama vya ushirika, kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa wazalishaji kupitia benki ya kilimo na mabenki ya biashara na kuimarisha huduma za ugani kwenye sekta za kilimo uvuvi na mifugo. Hatua hizi ni muhimu ziendelee kutekelezwa kwa kasi zaidi kwa kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya sekta hizi zinatolewa zote na zinatolewa kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Spika, kulingana na unyeti na manufaa ya kiuchumi yatokanayo na sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, napendekeza kwamba Serikali itambue kwamba mikakati ya kukuza tija na ufanisi katika miradi ya kilimo, mifugo na uvuvi itaweza kutekelezwa kwa mafanikio yaliyokusudiwa ikiwa wazalishaji wadogo na wakati watawezeshwa. Wazalishaji wadogo na wakati katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ndio chimbuko la kukuza mtaji wa kitaifa. Kwa kuwa mahitaji

mengi sana ya uzalishaji na masoko ya sekta za kilimo, uvuvi na mifuko hupatikana nchini hapana shaka uamuzi wa Serikali wa kuongeza bajeti katika sekta utakuwa na matokeo makubwa kwa manufaa ya wananchi wengi.

Aidha, ulimbikizaji wa mtaji kutoka chini *(accumulation of capital from below)* kwa kuweka mazingira bora ya uwekezaji kwa kutumia wakulima, wavuvi na wafugaji mmoja mmoja na wale waliojiunga kwenye vyama vya ushirika ndio njia pekee ya kupunguza tatizo la ajira, kupunguza pengo la wenye nacho na wasionacho na kupunguza umaskini. Vilevile, kupitia sekta za kilimo, uvuvi na mifugo upo uwezekano wa nchi kuwa na wazalishaji mahiri na matajiri watakaoweza kubadili muundo wa uchumi wetu.

Kwa maoni yangu, kwa kuwa mahitaji ya msingi ya kuongeza tija na ufanisi kwa ajili ya kukuza sekta za kilimo, uvuvi na mifugo yanapatikana hapa nchini, wawekezaji wa Tanzania wanaweza kusababisha matokeo makubwa iwapo watawekewa mazingira bora ya uwekezaji na kufanya biashara kwenye sekta kilimo, uvuvi na mifugo.

Mheshimiwa Spika, inabidi tujifunze kutokana na makosa yaliyofanywa kwenye sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na viwanda. Mojawapo ya makosa hayo ni kudhani kwamba ulimbikizaji wa mtaji kutoka juu *(accumulation from below)* kwa kutumia mashirika ya umma ilikuwa njia ya uhakika ya kujenga uchumi wa kitaifa. Hata vyama vya ushirika vilijengwa kutoka juu chini ya udhibiti wa Serikali. Makosa mengine yalifanywa wakati wa ubinafsishaji wa mashamba yaliyokuwa ya Serikali. Ili kusahihisha makosa yaliyofanyika huko nyuma, napendekeza yafuatayo:-

(a) Uchaguzi wa teknolojia itakayotumiwa kwenye miradi ya umwagiliaji uzingatie uwezo wa kifedha na kiufundi wa nchi na watumiaji ili iwe endelevu. Aidha, ujenzi na uendeshaji wa miradi mipya ya umwagiliaji ushirikishe vikundi

na vyama vya ushirika vya wazalishaji. Vilevile miradi mipya ya umwagiliaji ifungamanishwe kwenye mnyororo wa thamani kuanzia kweye hatua ya kugharamia nyenzo na teknolojia za kukuza tija kwenye shughuli za uzalishaji, nyenzo na teknolojia za uongezaji wa thamani, nyenzo na teknolojia za usafirishaji mazao ya kuelekea sokoni, maghala ya kuhifadhi mazao na mtandao wa masoko ya ndani na nje. Kutokana na mahitaji ya masoko ya ndani n nje, miradi mipya ya umwagiliaji ijikite zaidi katika uzalishaji wa mazao ya nafaka hasa mahindi, ngano na mpunga.

(b) Yafanyike mageuzi katika mfumo wa umiliki na matumizi ya ardhi yaani mfumo ambao utawapa wazalishaji uhakika wa kumiliki na kutumia ardhi kwa namna endelevu. Kifalsafa na kiitikadi, ardhi ni rasilimali nyeti na muhimu kwa ustawi na maendeleo ya nchi na watu wake. Kwa mujibu wa Azimio la Arusha; "Ardhi ni ufunguo wa maisha ya binadamu kwa hiyo Watanzania waitumie ardhi kama rasilimali yao kwa maendeleo ya baadaye. Kwa kuwa ardhi ni mali ya Taifa, Serikali ni lazima iangalie kuwa ardhi inatumiwa kwa faida ya Taifa zima na ardhi inatumiwa kwa faida ya mtu binafsi au kwa watu wachache." Msingi huu wa kifalsafa na kiitikadi umeliepusha Taifa na tishio la migogoro hatarishi baina ya tabaka linalohodhi rasilimali za ardhi na tabaka la wasiokuwa na ardhi. Hata hivyo, msingi huu umeanza kulegalega kutokana na sababu kadhaa ikiwemo mabadiliko ya kisera na kisheria yaliyofanyika tangu mwaka 1995. Katika eneo la usimamizi wa rasilimali ya ardhi na hata utatuzi wa migogoro ya ardhi, yamefanyika makosa kadhaa ambayo yanakwaza juhudi za wananchi na Serikali za kuendeleza sekta za kiuchumi zikiwemo sekta za kilimo, uvuvi na mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa ni vigumu sana mzalishaji katika sekta za kilimo na ufugaji kupata ardhi ya uhakika kutokana na ukweli kwamba maeneo mengi yanayofaa kwa mifugo na kilimo yamehodhiwa na watu wachache bila kuyaendeleza kwa tija. Kihistoria, ardhi ni mali

ya umma kwa maana kwamba kila Mtanzania anayo haki ya kumiliki na kutumia ardhi kwa ajili ya kuendesha maisha yake. Kwa msingi huo, ardhi haipaswi kuwa bidhaa yenye thamani sokoni bali ardhi ni kiini cha uhuru wa nchi na uhai wa watu wake. Hata hivyo, kisheria na kiuhalisia, ardhi ina thamani kubwa na inauzwa kama bidhaa sokoni. Hata Serikali ikitaka kutumia ardhi kwa manufaa ya umma inatakiwa kulipa fidia bila kujali kwamba ardhi hiyo imeendelezwa na mmiliki au laa.

Mheshimiwa Spika, ardhi tupu ambayo haina maendelezo yoyote hivi sasa inauzwa kwa mujibu wa sheria za ardhi hali inayochochea uuzaji wa ardhi kiholela na hivyo kutoa mwanya wa watu wachache kuhodhi ardhi kwa lengo la kuiuza. Aidha, ardhi tupu inawekwa dhamana benki na mmiliki anaweza kupewa mkopo na asiporejesha mkopo ardhi hiyo itauzwa sokoni na benki. Hata upimaji wa viwanja mijini unasukumwa na ongezeko kubwa la thamani ya ardhi na hivi sasa upimaji wa ardhi umekuwa moja ya vyanzo vikuu na vya uhakika vya mapato ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Kuipa thamani ardhi tupu kisheria kumechochea vitendo vya uporaji wa ardhi za vijiji kunakofanywa na watu na vikundi vya watu kwa nia ya kuilimbikiza ili baadae waiuze au waikodishe kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa upimaji wa viwanja katika maeneo ya pembezoni mwa miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha na Dodoma unaonesha kwamba watu wachache wamekuwa wakinunua maeneo ya ardhi kwa bei ndogo na kuyauza kama viwanja wakishirikiana na Halmashauri za Wilaya, baadhi ya maeneo hayo yalikuwa mashamba. Vilevile wananchi maskini wanashawishika kuuza ardhi tupu kiholela na hatimaye kutumbukia zaidi kwenye umaskini. Kwa ujumla lipo tishio la kuzuka tabaka la watu wengi wasio na uhakika wa kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukithiri kwa vitendo vya ulimbikizaji wa ardhi unaofanywa na watu wachache wenye lengo la kuiuza au kuikodisha baadae, lipo tatizo la uhaba bandia wa ardhi *(artificial land shortage)* katika maeneo mengi mijini na vijijini. Tatizo hili ni la muda mrefu na utatuzi wake unahitaji mabadiliko ya Sera ya Ardhi ya mwaka1995 na Sheria za Ardhi za mwaka 1999. Mabadiliko hayo yanatakiwa kuzingatia ukweli kwamba ardhi ni uhai wa nchi na watu wake. Kwa hali ilivyo sasa ni vigumu kukuza sekta za kilimo, uvuvi na mifugo kwa manufaa ya wananchi wengi ikiwa mfumo wa umilikaji ardhi hauwapi uhakika wazalishaji wadogo wa umiliki na matumizi bora ya ardhi.

Kuhusu mikakati ya kuongeza maeneo ya umwagiliaji na kuanzisha mashamba mapya ya kilimo cha kisasa *(block farms)* utekelezaji wake unategemea uhakika wa upatikanaji wa ardhi. Aidha, ufugaji wa kisasa nao unategemea upatikanaji wa uhakika wa ardhi. Hata lengo la Serikali la kuhakikisha kwamba nchi yetu inajitosheleza katika uzalishaji wa mazao ya kutengeneza sukari, ngano na mafuta ya kula litafikiwa tu iwapo upatikani wa ardhi utakuwa wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ifanye uhakiki wa ardhi inayofaa kwa shughuli za uwekezaji katika sekta za kilimo, ufugaji na matumizi mengineyo ili matokeo ya uhakiki huo yawe msingi wa kuandaa mpango wa kitaifa wa matumizi bora ya ardhi. Ipo dhana kwamba Tanzania ina ardhi tele inayofaa kwa uwekezaji wa kila aina ikiwemo kilimo na ufugaji. Dhana hii inatakiwa kuhakikiwa.

Mheshimiwa Spika, natambua juhudi za Serikali za kuimarisha mahusiano bora miongoni mwa watumiaji wa ardhi kwenye aina zote za ardhi kwa mujibu wa sheria na kwa maslahi ya Taifa. Hata hivyo, juhudi hizo zinakwamishwa na kuongezeka kwa migogoro ya ardhi hasa maeneo ambayo shughuli za kilimo na ufugaji zinapanuka kwa kasi na idadi ya watu inaongezeka kwa kasi. Kazi ni ngumu inayohitaji

kufanywa na Maafisa wa Serikali waadilifu na wabunifu. Aidha, Serikali iendelee kuhifadhi maeneo ya ardhi yaliyotengwa kisheria kwa ajili ya matumizi ya Taasisi, Idara, Wizara na Mashirika ya Umma. Ulinzi na uhifadhi wa maeneo ya ardhi yanayomilikiwa kisheria na Serikali ni suala muhimu kwani ardhi hiyo ni hazina ya Taifa kwa matumizi ya baadaye ikiwemo upanuzi wa shughuli za mafunzo, utafiti, hduma za jamii na ulinzi na usalama. Hazina hiyo ya ardhi iliyo chini ya taasisi za Serikali ikibidi kubadilishwa matumizi basi matumizi hayo yawe ya kimkakati na kwa faida ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, umekuwepo mjadala hapa Bungeni kuhusu dhamira ya Serikali ya kubadili matumizi ya maeneo ya ardhi inayomilikiwa na Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* katika mikoa ya Dodoma (Kongwa), Pwani (Ruvu) na Kagera (Mabare). Wapo Wabunge walioshauri kwamba Serikali isitishe mpango huo kwa kuwa hauna tija kwa Taifa. Naishauri Serikali kuangalia upya wazo hilo ili uamuzi utakaofanywa uwe na faida kwa Taifa. Ni muhimu tukajifunza kutokana na makosa ya nyuma wakati wa zoezi la ubinafsishaji wa mali za mashirika ya umma ikiwa ni pamoja na ubinafsishaji wa mashamba ya mkonge na viwanda vya kubangua korosho na viwanda vya nguo. Walionunua mashamba ya mkonge na viwanda vya nguo na viwanda vya kubangua korosho wengi hawakutekeleza ipasavyo mikataba husika.

(c) Yafanyike mageuzi katika uongozi na usimamizi wa vyama vya ushirika. Kwa kipindi kirefu, uongozi na usimamizi wa vyama vya ushirika vya kilimo vimegubikwa na matatizo mengi kutokana na uwezo mdogo wa watendaji na viongozi wa kuviendesha kwa weledi, ubunifu na uadilifu. Aidha, sera na sheria ya vyama vya ushirika vina udhaifu na ahadi ya Serikali ya kufanyia marekebisho sera na sheria hiyo imechukua muda mrefu kutekelezwa. Hata mtazamo wa sasa wa majukumu ya vyama vya ushirika ni finyu kwani vyama vya ushirika kwenye sekta za kilimo, uvuvi na kilimo

vimegeuzwa wakala wa wafanyabiashara. Kimsingi vyama vya ushirika vinatakiwa kushiriki kikamilifu katika shughuli zote kwenye mnyororo wa thamani kwa manufaa ya wana ushirika. Majukumu ya vyama vya ushirika hayapaswi kuanzia na kuishia kwenye utafutaji wa masoko, bali wanapaswa kufanya kazi zote ikiwemo kazi zote za kuongeza tija katika uzalishaji, kuongeza thamani ya mazao, kumiliki mabenki yatakayokuza mtaji wa vyama vya ushirika na kugharamia shughuli za uzalishaji na kutafuta masoko.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kufanya mchakato wa kupitia na kufanya marekebisho ya sera na sheria ya vyama vya ushirika ili kusahihisha makosa ya kisera na kisheria yaliyopo na kuweka mazingira bora ya kuimarisha ya vyama hivyo.

Katika kipindi hiki kigumu kiuchumi nchini na duniani kote, uhimilivu wa uchumi wetu, ukuzaji wa sekta za viwanda na biaashara na hata ufufuaji wa uchumi kwa ujumla vinategemea zaidi ukuaji wa kasi wa sekta za kilimo, uvuvi na mifugo, na ukuaji wa sekta hizi unategemea zaidi kiwango cha uwekezaji wa Serikali na sekta binafsi na pia kiwango cha ubora wa uongozi na usimamizi wa sekta hizi. Mtazamo kwamba siasa ni kilimo na kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa ni sahihi jana, leo na kesho. Hakuna njia ya mkato ya kukuza sekta hizi za uzalishaji na kazi ya kukuza sekta hizi ni kazi ya kufa na kupona. Kwa kuwa kuna utashi wa kisiasa wa kukuza sekta hizi za uzalishaji chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, hakuna sababu ya kudhani kwamba malengo yaliyowekwa kwenye sekta za kilimo, uvuvi na mifugo hatatafikiwa. Inawezekana ikiwa kila mdau wa uchumi na siasa nchini atatimiza wajibu wake.

(d) Iandaliwe mikakati shirikishi ya kuimarisha usalama na mahusiano mema miongoni mwa wadau. Ili kufikia malengo yaliyowekwa kwenye sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, pamoja na mambo mengine, ni muhimu Serikali

ishirikiane na wadau wa sekta hizi kuunda na kutekeleza mikakati ya kuimarisha usalama kwenye maeneo ya uzalishaji mali na pia kuboresha mahusiano kazini. Kumekuwepo na matukio kadhaa ya wizi wa mifugo katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, wavuvi kwenye bahari na maziwa makuu wamekuwa wakivamiwa wawapo kazini na kunyang'anywa nyenzo zao za kazi. Migogoro baina ya wakulima na wafugaji imekuwa ikihatarisha usalama wa wananchi na mali zao na hata kusababisha vifo katika baadhi ya maeneo nchini. Kumekuwepo pia malalamiko kutoka kwa wavuvi kwamba baadhi ya Maafisa wa Serikali wasio waadilifu wamekuwa wakidai rushwa au kutumia mabavu kupindukia wakati wa kuendesha operesheni dhidi ya uvuvi haramu. Yapo pia malalamiko ya wakulima, wafugaji na wavuvi kwamba nyenzo za kazi na hata pembejeo zinazouzwa au kugawiwa kupitia mpango wa ruzuku hazina ubora na zinawasababishia hasara. Kuna matukio mengi ya wanyamapori wakali na waharibifu hasa tembo kuwavamia wananchi katika makazi na mashamba yao na kufanya uharibifu wa mali na hata mauaji. Yapo pia malalamiko kwamba baadhi ya Maafisa Ugani hawawajibiki ipasavyo. Wakati wa msimu wa kuuza mazao baadhi ya wakulima hulalamikia makato holela kwenye mauzo yao na wengine hudhulumiwa pesa zao baada ya kuuza mazao yake. Upo pia utapeli na wizi kwenye vipimo wakati wa mauzo. Matatizo yote haya ya kiusalama na kimahusiano yanatakiwa kupatiwa ufumbuzi ili kufikia malengo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya elimu; kwa kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika na miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Taifa letu la Tanzania limepata mafanikio makubwa sana katika sekta ya elimu katika ngazi zote. Pamoja na changamoto zinazoikabili sekta ya elimu, Watanzania tunatakiwa kujivuna na kuona fahari kutokana na mafanikio hayo. Mpango wa bajeti ya Serikali

kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 unaendeleza juhudi za Serikali ya CCM kukabiliana na changamoto za sekta ya elimu. Naipongeza Serikali ya CCM kwa mpango wake wa kupanua wigo wa elimu bila ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato sita. Aidha, naipongeza Serikali kwa kutafuta pesa za kugharamia mpango kamambe wa maboresho katika taasisi za elimu ya juu.

Suala ambalo nitalizungumzia kwa undani ni kuhusu mchakato ulioanzishwa na Serikali wa kupitia mitaala ya elimu katika ngazi zote za elimu. Kwa kuwa Serikali imeanzisha mchakato shirikishi wa kupitia mitaala kwa lengo la kulinda na kukuza ubora wa elimu inayotolewa hapa nchini, ni matarajio yangu kwamba changamoto zinazosababisha kushuka kwa ubora wa elimu yetu zitapatiwa ufumbuzi baada ya kukamilika kwa zoezi hilo. Bila shaka, mchakato huu wa kupitia mitaala utakuwa mgumu kutokana na mgongano wa kimtazamo miongoni mwa wadau wa elimu kuhusu dhana na maana ya elimu bora. Upo pia mgongano wa kimtazamo miongoni mwa wadau wa elimu kuhusu mikakati na mbinu mwafaka za kulinda na kukuza ubora wa elimu yetu. Ikiwa mchakato wa kupitia mitaala ya elimu utakuwa shirikishi kiasi cha kutosha nina uhakika tutapata mwafaka wa kitaifa kuhusu hatima ya ubora wa elimu ya nchi yetu. Pamoja na matumaini makubwa waliyonayo wadau wa elimu kuhusu matokeo ya mchakato wa kupitia mitaala ya elimu, lengo letu lisiwe kubadilisha kila kitu kana kwamba mfumo wa elimu yetu unazaliwa upya. Naamini kwamba yapo mafunzo yanayoweza kupatikana kutokana na historia ya ukuaji na maendeleo ya sekta ya elimu nchini tangu tupate uhuru. Ni jambo jema kutamani mambo mema na mapya; ni jambo jema pia kujifunza kutoka nchi nyingine ndani na nje ya Bara la Afrika. Ni vizuri pia kujifunza kutokana na uzoefu mzuri uliolimbikizwa kwa muda mrefu kwenye sekta yetu ya elimu tangu tupate uhuru. Ni vizuri pia kuthamini mafanikio tuliyokwisha yapata na kuyalinda na kuyaendeleza. Zipo tafiti kadhaa, taarifa za tume na vikosi kazi ambazo zimewahi

kufanywa huko nyuma kuhusu mageuzi na maboresho kwenye sekta ya elimu nchini ambazo zinaweza kuwa chanzo cha fikra na mawazo ya kuboresha elimu yetu. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba mchakato wa kupitia mitaala ya elimu unaoendelea ni nyeti na unahitaji kuendeshwa kwa weledi na umakini mkubwa sana kwa maslahi ya Taifa. Ni dhahiri kwamba Watanzania wanataka mabadiliko katika sekta ya elimu hususan kwenye maeneo ya ubora wa elimu *(quality)* na manufaa ya elimu *(relevance)* na shabaha ya elimu *(purpose)*. Maeneo hayo ndiyo yanayojadiliwa zaidi humu Bungeni na ndani ya jamii. Kama njia ya kuchangia kwenye mjadala unaoendelea hasa kuhusu kusudi la elimu, napenda kumnukuu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwenye moja ya hotuba zake aliyoitoa mwaka 1970; "Kujifunza kokote kuna kusudi, kusudi hilo ni kuongeza nguvu kazi kwa ajili ya mtu na mazingira yake. Kwa maneno mengine, shabaha ya ujifunzaji ni maendeleo ya watu na utu."

Mheshimiwa Spika, mtazamo huu wa Mwalimu Nyerere kuhusu shabaha ya elimu unafaa kuwa mwongozo wetu wakati wa kujadili hatima ya elimu yetu. Ili elimu ichangie katika maendeleo ya watu na utu ni muhimu mitaala ya elimu katika ngazi zote ichochee tabia ya uthubutu, ujasiri, utaifa, udadisi, ubunifu, uwajibikaji, kujiamini, kujitegemea na uadilifu miongoni mwa wahitimu. Wahitimu bora huzalishwa na walimu bora na walimu bora wanatakiwa kupatikana kutoka kwenye kundi la wahitimu bora. Kwa hiyo, mtaala bora ndilo chimbuko la elimu bora na elimu bora huzalisha wahitimu na walimu bora.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu pia kutambua kwamba mchakato wa kujifunza ni endelevu na wala hauishii kwenye hatua ya mwanafunzi kufaulu mitihani na kutunukiwa vyeti. Kwa hiyo, mfumo wa elimu utakaotufaa ni ule unaojenga tabia ya Watanzania kupenda kujielimisha wakati wote hata baada ya kuhitimu na kutunukiwa vyeti. Hoja hii ya umuhimu

wa wananchi kuwa na tabia ya kujifunza imesisitizwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika moja ya makala zake aliyoyaandika mwaka 1962. Nanukuu; "Watu walio hatari sana ni wale ambao wanafikiri kuwa wanajua kila kitu wala hawana haja ya kujifunza zaidi. Hii ni tabia mbaya ambayo huzuia kabisa maendeleo." Zipo njia nyingi za kujenga tabia ya Watanzania kupenda kujifunza. Kupitia kazi za wasanii wabobezi, wanafasihi wabobezi, waandishi wa vitabu mashuhuri na wasifu za watu mashuhuri ni vyanzo muhimu vya wananchi kujifunza. Eneo hili nalo linapaswa kuzingatiwa katika mjadala wa kukuza ubora wa elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia hutoba ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia ukurasa wa saba ambao umezungumzia Dhima ya Serikali ya Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kwanza kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Sambamba na hilo dhima kuu ya bajeti kama ilivyokubaliwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Pili, ni kuongeza kasi ya kufufua uchumi na kuimarisha sekta za uzalishaji kwa ajili ya kuboresha maisha. Sambamba na hilo dhamira ya Serikali ni kujenga uchumi na kukabiliana na umasikini pamoja na ukosefu wa ajira hasa kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, maana yangu ni nini; awali ilkuwa zikitolewa asilimia 10 ambazo zikigaiwa kwa nne, nne na mbili ambazo zilikuwa zikisaidia sana makundi ya vijana, wanawake na ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli na sisi kwa macho yetu tuliona kwamba ilikuwa ikiwasaidia sana makundi haya. Ni jambo la kushangaza kusikia Serikali inadhamira ya kupunguza mikopo hii kutoka asilimia 10 na kwenda asilimia tano. Maana yake makundi haya yanaweza kupata mkopo huu kwa asilimia mbili, mbili na moja.

Mheshimiwa Spika, hapa kweli kuna uhalisia wa kufanya biashara na kuweza kujikwamua kiuchumi na kupunguza umasikini. Kwa vile Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 inatamka kuwa Tanzania itakuwa imefuta umasikini na tunafikia uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwanza ufanyike utafiti wa kisayansi, kwa kuwahusisha makundi yaliyokuwa yakifaidika na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili ifanyike tathmini ya mafanikio na changamoto tangu utaratibu wa mikopo hii ilipoanza kutolewa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba changamoto zipatiwe majibu na fursa ziendelezwe.

Mheshimiwa Spika, bado Serikali tunaiomba itoe mikopo ya asilimia 10 au 15 ili kama kweli tunataka makundi haya kujikwamua kiuchumi badala ya kupunguza hizi asilimia.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali iangalie namna ya kuona kuwa wanafunzi wote wenye sifa za kupata mkopo ni haki yao kwani wale waliotoka *private schools* wengi wao wanakosa mkopo kwa *formula* ambayo bodi inatumia.

Mheshimiwa Spika, ada ya sekondari ni mkataba kati ya mzazi na shule; na chuoni ni kati ya mwanafunzi na Serikali, huyo mwanafunzi atalipa mwenyewe. Wakati mwingine mzazi anakuwa na uwezo wa kulipa ada kwa kipindi fulani na anaweza kupoteza kazi yake au kustaafu hivyo kushindwa kulipa ada ya chuo kikuu. Niiombe Serikali itoe ada kwa wanafunzi wote bila kujali uwezo wa wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, pili, kilimo cha tumbaku kina hasara zaidi kuliko faida. Maeneo yanayolima tumbaku yanaweza kubadili kilimo hicho na kulima mazao mbadala. Baadhi ya magonjwa mengi hutokana na tumbaku kama kansa ya ubongo, mapafu, moyo, figo, tezi dume na ovari.

Mheshimiwa Spika, hata ukulima huo hauna faida kwa wakulima hao wengi wamebaki maskini huko Namtumbo na Tabora hakuna faida. Faida inabaki kwa wanunuzi na wakulima wakubwa ambao hukopeshwa mbegu na mbolea kama chama cha msingi, ni unyonyaji wa hali ya juu. Serikali iamue kusitisha hata viwanda vya tumbaku. Tumbaku *is killing our people healthy wise and economically*. Wakulima wadogo hawapati kabisa zile *grade* za kwanza hata kama watafuata taratibu zote.

Mheshimiwa Spika, hebu tujikite kwenye alizeti kwenye sehemu hizo kwa ku-*replace* hilo zao la tumbaku.

Mheshimiwa Spika, ukatili wa kijinsia ni suala linaloendelea sana kwenye jamii yetu. Eneo hili la ukeketaji linaendelea na bado juhudi za kutokomeza zimepungua sana. Sasa hivi watoto wanakeketwa wakiwa wamezaliwa kabla hawajafika nyumbani. Nashauri ulinzi uwepo sehemu watoto wanakozaliwa hasa mikoa inayoongoza kwa ukeketaji.

Mheshimiwa Spika, wakati watu wenye ulemavu wa ngozi walipokuwa wanakatwa viungo Serikali ilikuwa makini

kwa kuwakamata na kuwaonesha hadharani, pia kuwafunga. Kwa nini kwenye ukeketaji Serikali inalegalega?

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri Gwajima anampeleka gerezani ngariba mmoja hiyo haitoshi, maghariba wako wengi na ukeketaji unaendelea katika mikoa ya Mara, Singida, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Manyara na baadhi ya maeneo ya Morogoro na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, madhara ya ukeketaji ni mengi kama ulemavu, maumivu, saikolojia kubadilika, anemia, maambukizi ya magonjwa na hatimaye kifo.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kifo kikitokea kwa wale wasichana huko porini inakuwa ni siri kubwa, halisemwi jambo hilo Serikalini hasa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, wanawake wanaokeketwa huwa hawana furaha kwenye ndoa zao, huwa kama wanabakwa kwani hawafurahii tendo la ndoa. Hii hupelekea ndoa nyingi kuvunjika familia kukosa amani na furaha.

Mheshimiwa Spika, Wizara hizo tatu ziongezewe fedha ili kuweza kupambana na ukatili huo wa kijinsia kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa nyongeza ya mchango wangu kwa hotuba ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa juhudi zake kwa njia ya kistaarabu kupitia *TRA* na kaulimbiu yake ya ukiuza toa risiti na ukinunua dai risiti. Lakini kumekuwa

dosari kidogo katika maelekezo ya kutoa risiti hasa pale mtoa huduma anapotakiwa kuambatanisha madai yake ya huduma aliyotoa yaambatanishwe na risiti ya *EFD,* ukitilia maanani kuwa mara unapotoa risiti ya *EFD* unatakiwa ulipe pia *VAT* kwa *TRA* ndani ya kipindi cha mwezi vinginevyo usipolipa unadaiwa pamoja *penalty.*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naiomba Serikali iangalie changamoto wanazozipata wafanyabiashara. Inapotokea mtoa huduma wanacheleweshwa sana kulipwa huduma wanazotoa hasa kwa taasisi za Serikali. Je, Serikali haioni iko haja ya kurekebisha sheria hii kudai *VAT* na kodi kwa biashara ambayo imekopwa? Vinginevyo wajasiriamali wetu watafilisika kwa riba za benki walizokopa mikopo ya biashara na kodi za *TRA,* pia Serikali ije na maelekezo kwa taasisi za Serikali kulipa wazabuni kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ni vyema wafanyabiashara wangepewa kipindi cha miezi miwili au mitatu ya kuwasilisha risiti za malipo badala ya kuwasilisha madai kuambatanisha risiti ya *EFD* sababu malipo yanakuwa hajafanyika.

Kuhusu Sheria ya Manunuzi; utaratibu wa kutafuta wazabuni wa kutoa huduma inayotarajiwa kutolewa hivyo kupelekea kupatikana kwa huduma kwa taasisi za Serikali imekuwa na tatizo la kutoa *tender* kwa huduma bila kuzingatia kiwango cha huduma inayotarajiwa kutolewa hivyo kupelekea kupatikana kwa huduma zilizo chini ya kiwango na kuwaacha watoa huduma bora walioweka fedha halali kwa huduma bora, hatujui ni woga wa watu wa *procument.*

Mheshimiwa Spika, ninavyojua mimi anayetakiwa kupewa *tender* ni *lowest evaluated bidder* na sio *lowest bidder,* utaratibu wa kumpata *tenderer* (mtoa huduma)

aliyeweka fedha kidogo umepelekea huduma zenye kiwango cha chini kwenye taasisi nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mimi nianze kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuletea bajeti nzuri na iliyokamilika na inayoleta matumaini makubwa kwa Watanzania. Pia niipongeze Wizara ya Fedha, Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa walioifanya katika kutuletea hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, sekta ya elimu; naipongeza Serikali kwa kutuletea mradi wa kuboresha elimu ya juu kwa mabadiliko ya kiuchumi, kwa sababu mradi huu utawawezesha wahitimu wa vyuo vikuu kuacha utegemezi baada ya kumaliza masomo yao.

Pia naipongeza Serikali katika mradi huu ambao unalenga kuboresha miundombinu za vyuo vikuu vyetu, vya Lindi, Kagera, Rukwa, Katavi, Manyara na kukamilisha ujenzi wa *Institute of Marine Science* ya Zanzibar na chuo kipya cha TEHAMA Dodoma.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuipongeza Serikali ya Mama Simia Suluhu Hassan kwa hatua yake nzuri ya kuendelea kugharimia programu ya elimu ya msingi kwa kuondoa ada jambo ambalo linawawezesha watoto wetu hasa kutoka kwenye familia masikini kuweza kupata haki yao ya msingi ya kielimu na kuwaepusha na matendo maovu yakiwemo masuala ya udhalilishaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kama mama na sisi kwa pamoja tumeguswa na kusikitishwa sana kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo umasikini, mimba za utotoni ambazo zimekuwa zinarejesha nyuma na kusambazwa suala la elimu kwa watoto hususan wa kike kwa kukatishwa masomo, lakini jambo zuri na la kumpongeza ni kuona kwamba Serikali yetu inaenda kulipatia mwarubaini suala hilo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya; kwa namna ya kipekee napenda pia kupongeza Serikali ya CCM inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan inafanya kuboresha sekta ya afya, ni faraja kubwa kwa jamii yote, lakini hasa kwa sisi wanawake ambao huwa tunateseka hasa katika huduma ya mama na mtoto. Kupitia hotuba hii ya bajeti tumeona jinsi Serikali ilivyopanga kujenga hospitali maalum ya mama na mtoto Dodoma na Hospitali ya Kanda ya Magharibi, kukamilisha ujenzi wa hospitali tano za Rufaa za Mikoa katika mikoa mpya ya Katavi, Geita, Njombe na Simiyu, pamoja na kukamilisha hospitali nane za rufaa za mikoa. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu nyingine za kuimarisha sekta ya afya ambazo ninazipongeza kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi; mwaka 2021 sekta ya uvuvi ilikua sana mpaka asilimia 2.5 na ilichangia asilimia 1.8 kwenye pato la Taifa kwa hivyo pia Serikali imeweza kuchangia kwa kutoa ajira nyingi kwa Watanzania na pia Serikali imeamua kujenga bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa pamoja na kununua meli mbili za uvuvi katika ukanda wa uchumi wa bahari na ununuzi wa boti za kisasa kwa wavuvi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali yetu kwa kununua vifaa vya kuvutia samaki na kuendelea na jitihada za kutafuta ufufuaji wa Shirika la Uvuvi wa Tanzania na kuwajengea uwezo wataalamu kwa kuwapatia elimu na

mafunzo ya uvuvi na tafiti mbalimbali na kukamilisha mialo ya kupokea Samaki, vilevile na kujenga masoko yenye maeneo ya kimkakati na kukarabati vituo vya ulinzi na rasilimali ili kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, napongeza sana juhudi ya Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia kwa kazi nzuri inaendelea kufanyika. Tanzania inakwenda kupaa kwa maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu nzima wamejitahidi kutenda haki na kuwa ubunifu wa hali ya juu kujenga uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuoanisha mchango wangu huu wa kuinua uchumi kwenye sekta muhimu ya kilimo. Uchumi wa dunia kupitia kilimo hai umekuwa ukiongezeka kwa kasi sana kufikia *Euro* milioni 124 kwa mwaka 2020 ikiwa ni ongezeko la *Euro* bilioni 14 kutokea mwaka 2019. Ukiacha maeneo yaliyozoeleka ya chakula kumekuwa na ongezeko kwenye bidhaa za vipodozi, mavazi na madawa asili ya binadamu na viatilifu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunayo nafasi kubwa ya kuongeza kipato chetu kupitia mfumo wa kilimohai ambao hauna gharama kubwa kwa Serikali na mzalishaji, nikitolea mfano zao la pamba na tunayo mengi kama hilo. Miaka miwili iliyopita Tanzania tayari ilikuwa nchi ya tano kwa uzalishaji mkubwa wa pamba ya kilimohai duniani na katika msimu wa mwaka 2021/2022, zaidi ya wakulima wa pamba 40,000 nchini Tanzania wamethibitishwa kimataifa. Kwa sasa mahitaji ya pamba ya kilimohai duniani yamezidi uzalishaji. Inakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 84 katika mwaka 2020 na 2030.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya kampuni 36 za kimataifa zinazotengeneza nguo na wauzaji wameahidi kutumia pamba ya kilimohai pekee tu ifikapo mwaka 2025. Mzalishaji mkuu wa pamba duniani nchi ya India ana matatizo ya kuongeza uzalishaji wake kutokana na kutumia mbegu zenye vinasaba vya viini tete *(GMO)*. Tanzania, kinyume chake, inakataza matumizi ya *GMO* na kwa kawaida hutumia viatilifu vyenye asili ya kemikali kidogo kuliko nchi nyingine. Hii inaipa Tanzania fursa ya kimkakati ya kujiweka kama mzalishaji mkuu wa pamba hai duniani.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iweze kuzingatia na kuona kwamba sasa ni wakati muafaka wa kutoa kipaumbele kwa mfumo huu wa kilimohai sio tu kwa pamba bali hata mazao mbalimbali kwa mfumo wa kilimohai ikiwa pamoja na pamba.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu na kukithiri kwa ongezeko la maradhi yasiyoambukiza. Maradhi hayo mengi ni kutokana na ongezeko la matumizi ya kemikali kwenye kilimo chetu, sambamba na uchafuzi wa mazingira na kuangamiza vimelea muhimu kwa afya na uhai wa udongo. Serikali haioni haja ya kujipunguzia gharama kwenye matibabu mfano kansa kwa kuondoa matumizi ya kemikali sumu kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, nafasi ya kilimohai katika kuongeza ajira kwa vijana wetu ni tunzo yetu tuliyopewa na muumba tusiiache kwa kuendelea kuwa soko la biashara za kemikali na kukubali kuharibiwa uoto wetu wa asili kwa neno la kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Spika, tukiwawezesha vijana wetu kwenye uzalishaji wa mbolea za asili kama walivyoanza ndugu zetu wa Ghana tayari wamepunguza kwa kiasi matumizi ya mbolea za kemikali na kutumia mbolea inayozalishwa na taka. Pia vijana wana nafasi ya kutengeneza viatilifu vya

kibaiolojia kutumia malighafi zinazopatikana. Niiombe Serikali ifikirie kutoa ruzuku ya mbolea za kemikali na tutumie ruzuku kuwasaidia vijana kuzalisha. Mifano ipo kama ilivyo kwa Kikundi cha *Hakika Fertilizer.*

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu, pia nakupongeza wewe Spika kwa kazi nzuri, nawapongeza Waziri Mwigulu na Naibu Waziri wake na watendaji wote wa Wizara nzima.

Mheshimiwa Spika, natoa pongeze kwa Rais Mheshimiwa Samia kwa kazi ya kuhakikisha Watanzania tunakuwa kiuchumi na kusimamia sera na mpango wa maendeleo kwa manufaa ya Taifa. Pia natoa pongezi kwa Rais kwa kuifungua nchi, hakika Watanzania tunajivunia maana hata vivutio vya kitalii vimejulikana kimataifa.

Mheshimiw Spika, natoa pongezi kwa Serikali kwa kuondoa ada ya kidato cha tano na sita; ni imani yangu hatua hii itampa fursa mtoto wa kike kuendelea na masomo na kuepuka ndoa za utotoni. Niishauri Serikali iweke miundombinu rafiki kwenye shule hizi kwa watoto walemavu.

Mheshimiwa Spika, ninaamini Serikali yangu ni sikivu sana, niiombe sana asilimia 10 ya wanawake, vijana na walemavu isipunguzwe bali ndugu zetu wamachinga nao ni muhimu sana wakatafutiwa fedha za miundombinu kwenye vyanzo vingine. Nishauri fedha zinazopunguzwa kwenye magari ya Serikali basi ziangaliwe na kutoa *percent* kiasi na kuwapatia wamachinga.

Mheshimiwa Spika, niongelee Jimbo la Temeke hasa kuhusiana na wafanyabiashara ndogo ndogo, niiombe Serikali iimarishe mifumo ya TEHAMA katika kufanya makadirio ya kodi kwani itasaidia sana wafanyabiashara wadogo wadogo kupenda kulipa kodi badala ya kukwepa na pia

itasaidia sana katika kuongeza mapato ktaika Halmashauri zetu hata kufanya Serikali pia kuongezeka kwa mapato.

Mheshimiwa Spika, nauga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuwasilisha vizuri taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa miaka mitano wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026 na bajeti kuu ya Serikali ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuipongeza Serikali ya CCM inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa jinsi wanavyotekeleza kwa umakini Ilani ya CCM. Miradi mingi ya maendeleo inatekelezwa Tanzania nzima katika kila jimbo la uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye umuhimu wa kuboresha miundombinu ya barabara kwenye vivutio vya utalii katika maeneo ya Mlima Kilimanjaro na ushauri kwa Serikali kujenga shule maalumu za sayansi kila mkoa.

Mheshimiwa Spika, mbali na Mlima Kilimanjaro, Mkoa wa Kilimanjaro una vivutio kadhaa vya utalii ambavyo vikitumika kikamilifu vitatuongeza idadi ya watalii na kuliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni. Kwa mfano, Mkoa wa Kilimanjaro una mti uitwao Mkukusu. Mti huu uko katika Kijiji cha Tema, kata ya Mbokomu ndani ya hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Huu ndiyo mti mrefu kuliko miti yote Barani Afrika kwani una urefu wa mita 81.5 na umri wa miaka 600. Tangu ugunduliwe, watalii wamekuwa na shauku kubwa ya kutembelea eneo hili.

Pili, Kanisa Katoliki kibosho na taasisi zake; eneo hili liko katika Kijiji cha Singa katika Kata ya Kibosho Mashariki. Hii ni Parokia ya pili ya Kikatoliki Kilimanjaro baada ya ile ya Kilema.

Ukifika eneo hili ndio utaelewa kwa nini limekuwa likitembelewa na watalii. Eneo hili lina jengo la kuvutia sana la Kanisa lililojengwa kwa mawe ya kuchonga karne ya 18 na lina mazingira mazuri ya kijani na ni sehemu unayoweza kuuona vizuri Mlima Kilimanjaro na kupiga picha.

Tatu, kivutio kingine ni maporomoko ya maji Materuni. Maporomoko haya ni moja ya maporomoko ya maji katika Mto Mware, Kata ya Uru Mashariki, Jimbo la Moshi Vijijini, Mkoa wa Kilimanjaro. Maporomoko haya yanapatikana katika Kijiji cha Materuni pembezoni mwa hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Maporomoko haya yana urefu wa zaidi ya mita 100.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vivutio katika maeneo haya, changamoto kubwa inayokabili maeneo niliyotaja hapo juu ni ubovu wa miundombinu ya barabara. Kutokana na ubovu wa barabara, watalii hupata shida kufika katika maeneo haya na hii imepelekea kupunguza idadi ya watalii.

Mheshimiwa Spika, changamoto za barabara katika maeneo yanayopeleka watalii kwenye vivutio vya Mlima Kilimanjaro zinatakiwa zipewe kipaumbele cha pekee na Wizara ya Maliasili na Utalii kwani wao ni wanufaika wakuu. Ninaishauri Serikali iachane na kuzitegemea *TARURA* na *TANROADS* kwani mitandao yao ya barabara ni mingi na hawajatoa kipaumbele kikubwa kwa barabara za jimbo langu zinazopeleka watalii kwenye hivi vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali, huu ni wakati wa kutumia michango ya *Corporate Social Responsibility (CSR)* unaotokana na mapato ya Mlima Kilimanjaro kutengeneza miundombinu ya barabara katika jimbo langu la Moshi Vijijini. Fedha hizi zipelekwe halmashauri husika ili wasimamie ujenzi wa barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini Tanzania mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetoa fedha za kujenga shule moja maalumu ya sayansi kwa ajili ya wasichana katika kila mkoa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upendeleo nilioeleza hapo juu, hapa nchini kuna uwekezaji mkubwa sana kwenye shule bora za wasichana. Mfano wa shule bora binafsi zenye ufaulu mkubwa ni pamoja na *St. Francis Girls* - Mbeya, *Barbo Johansson Model Girls* - Dar es Salaam, *St. Christian Girls* - Tanga, *Loretto Girls* - Mwanza, *Samaritan Girls Secondary School* - Shinyanga, *Anwarite Girls Secondary*- Kilimanjaro, *Precious Blood* - Arusha, *Bethel Sabbs Girls Secondary School, St. Theresa of Avila Girls Secondary, Hekima Girls Secondary School* - Kagera, *Visitation Girls School* - Kilimanjaro, *Kandoto Science Girls Secondary* - Kilimanjaro, *Marian Girls* - Pwani, *Feza Girls* - Dar es Salaam, *Kibosho Girls Secondary* - Kilimanjaro, *Mazinde Girls* - Tanga, *Kifungilo Girls* - Tanga, *St. Mary's High School* - Dar es Salaam, *John the Baptist Girls Secondary School* - Dar es Salaam, *Kunduchi Girls Islamic High School* - Dar es Salaam, *Bethsaida Girl's Secondary School* - Dar es Salaam, *St. Marie Eugenie Girls Secondary School* - Kilimanjaro, *Joyland Girls Secondary School* - Kilimanjaro, *St. Christina Girls Secondary School* - Tanga na *St. Clara Girls Secondary School* - Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, idadi kubwa ya wasichana wanaosoma katika shule nilizotaja hapo juu hufaulu vizuri na wengi wao hufanikiwa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu hapa nchini. Kwa kifupi, mazingira ya kuwasaidia wasichana kujiendeleza zaidi ni mazuri kuliko ya wavulana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine uwekezaji kwenye shule za wavulana ni kidogo sana ukilinganisha na ule wa wasichana. Shule chache za binafsi ninazoweza kuzitaja ni kama *Marian Boys, Feza Boys, Tengeru Boys* na nyingine chache ambazo sijazitaja.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na changamoto hii ninapendekeza kwa Serikali iwekeze kila mkoa na kujenga shule ya vipaji maalumu ya sayansi kwa ajili ya wavulana.

Mheshimiwa Spika, tusipochukua hatua za kimakusudi kusaidia watoto wa kiume kwa kuwajengea shule maalumu, huko mbele ya safari uwepo wao katika vyuo vya elimu ya juu utakuwa na walakini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna bora anavyoingoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa katika maeneo yote muhimu ya ustawi wa nchi yetu eneo la siasa, eneo la *diplomatic*, eneo la uchumi na eneo la utamaduni na maeneo mengineo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye eneo la uchumi pekee; katika eneo hili Mheshimiwa Rais ameitendelea haki sana kwa kuhakikisha vichocheo vya uchumi vyote vimeimarika. Sekta muhimu za kilimo, biashara, uwekezaji, viwanda, nishati na usafirishaji ambazo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa nchi vinaboreshwa. Kwenye kilimo kuna mipango mizuri ya uendeshaji kilimo inayoendana na rasilimali fedha na ushahidi wa hilo ni ongezeko la bajeti ya kilimo kwa asilimia kubwa ambayo haijawahi kutokea kutoka shilingi bilioni 294 hadi kufikia shilingi bilioni 954.

Kwa upande wa eneo la biashara; eneo hili pia kazi kubwa ya kuondoa vikwazo vya biashara imefanyika, *blue print* ni kielelezo cha kazi hii nzuri, tozo 232 zimeondolewa ndani ya siku 100.

Mheshimiwa Spika, eneo la uwekezaji Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amefanya makubwa katika kipindi kifupi sana cha uongozi wake. Mheshimiwa Rais ameweza kushawishi kiasi cha dola bilioni 1.6 hiki ni kiasi kikubwa kuwahi kutokea.

Eneo la usafirishaji ukamilishaji wa reli ya kisasa kutoka Isaka kwenda Mwanza, ujenzi wa meli mpya nne na ukarabati wa meli kubwa moja, meli hizi zitasafirisha zaidi ya tani 3000 za mizigo kwenda nchi jirani, ujenzi wa viwanja vya ndege na eneo la nishati kuna kazi kubwa pia ya kuhakikisha nishati inapatikana na inatosheleza mahitaji yetu ya ndani na kuuza nje ya nchi, ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere litakalotoa *megawatt* 2115 na uwekezaji mkubwa wa *LNG* wa dola bilioni 30 katika mikoa ya Lindi na Mtwara ni mafanikio makubwa kupata kutokea. Uwekezaji huu unaongezekana zaid ya nusu ya uchumi wote wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kuhusu kupanda kwa bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 234 hadi shilingi bilioni 954. Tunaipongeza sana Serikali iliyoundwa na Chama cha Mapinduzi kwa nia njema ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 hadi 2025 kwa kuongeza fedha za Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kutoka shilingi bilioni 234 hadi shilingi bilioni 954. Hii ni hatua nzuri itakayoongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini na kuifanya nchi kuwa na chakula cha kutosha ndani na kingine kuuzwa nje ya nchi. Pamoja na mafanikio yanayoweza kujitokeza kutokana na uzalishaji wa mazao kuongezeka, zipo changamoto zinazoweza kutokea ambazo Wizara wanatakiwa kujipanga nayo yakiwemo masoko ya mazao ya biashara. Naishauri Serikali ijipange mapema iwezekanavyo kutafuta masoko ya mazao ili uzalishashaji ulete tija kwa Taifa.

Pili ni kuhusu miundombinu ya kusafirisha/kupitisha mazao yanayovunwa; barabara za wilaya na mikoa ya pembezoni sio rafiki kwa usafirishaji wa mazao ya wakulima. Serikali ijitahidi kutengeneza barabara ili mazao yatakayozalishwa yaweze kusafirishwa bila kuharibika. Mfano mikoa ya Lindi na Mtwara barabara zake sio rafiki mazao yanaweza kuharibika.

Pia Bandari ya Mtwara kutotumika ipasavyo inazorotesha uchumi wa wana Mtwara na Lindi na Taifa kwa ujumla; viwanda vya kubangua korosho viwili vya Newala na 10 vya maeneo mengine havifanyi kazi badala yake vinatumiwa kama maghala jambo ambalo halileti tija kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, ushauri kwa Serikali; kwanza Serikali ijikite sasa kutafuta masoko ya mazao ya kilimo yatakayozalishwa ili yasiishie kuharibika na kukatisha tamaa wakulima. Pia masoko yakipatikana yataleta faida ya kiuchumi kwa nchi yetu.

Pia barabara zenye hadhi ya kuchongwa huko vijijini zichongwe ili zipitike muda wote ili kurahisisha wafanyabiashara na wakulima kusafirisha mazao yao kwa urahisi. Vilevile barabara zenye hadhi ya lami nashauri ziwekwe lami mfano barabara ya kiuchumi ya Mtwara – Nanyamba - Tandahimba -Newala hadi Masasi kwa kiwango cha lami. Vilevile barabara ya Amkeni - Kitangari - Mtama zijengwe kwa kiwango cha lami ili wananchi warahisishiwe usafiri.

Kuhusu Bandari ya Mtwara iweze kufanya kazi yenye tija inatakiwa sasa; kwanza ni kwa kufufua mradi wa *Mtwara Development Corridor* ili bidhaa zetu za kilimo zitoke na kusafirishwa nchi jirani kupitia bandari yetu ya Mtwara

Pili, kujenga reli ya kisasa ya Mtwara hadi Mbambabay na Malawi ya Liganga na Mchuchuma ili makaa ya mawe

toka yanakozalishwa kufikishwa bandari ya kupitia njia ya reli kwani kwa kutumia barabara, barabara zetu zitaharibika haraka sana.

Naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha hoja yake atueleze yafuatayo; moja, mpango wa *Mtwara Development Corridor* umefikia wapi?

Pili, mpango wa ujenzi wa reli ya Mtwara - Mbambabay umefikia wapi? Na tatu, mpango wa ujenzi wa barabara ya kiuchumi ya Mtwara - Newala - Masasi kilometa 160 zilizobakia utaanza rasmi lini?

Kuhusu ukusanyaji wa mapato ya Serikali; katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango imeeleza maeneo ya kupata fedha za bajeti kuu ya mwaka wa fedha 2022/2023 ikiwemo mapato kutoka *TRA,* mikopo toka kwa wahisani wa maendeleo na mapato toka vyanzo visivyo vya kikodi vya Wizara/Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu naulenga kwenye makusanyo toka Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ipo changamoto kubwa kwenye matumizi yanayopatikana katika Halmshauri zetu. Ukusanyaji wa mapato kupitia *PoS* wapo wakusanyaji mapato ambao sio waaminifu. Tunashukuru ipo *improvement* toka ripoti ya *CAG* ya mwaka 2019/2020 ambako halmashauri nyingi zilikuwa na changamoto ya makusanyo kupitia *PoS* ukilingahisha na ripoti ya *CAG* kama hiyo ya mwaka 2020/2021. Kati ya ukurasa 194 hadi 205 ya ripoti ya *CAG* ya mwaka 2020/2021 imeeleza upotevu wa fedha kupitia *PoS*. Lakini pia ripoti hiyo imeonesha matumizi mabaya ya fedha za mamlaka ya Serikali za Mitaa yafanywayo na watumishi wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwachukulie hatua za kinidhamu watu wote waliojihusisha na upotevu wa fedha za Serikali kupitia *PoS* na

matumizi mengine yasiyo halali waliobainishwa katika ripoti ya CAG ya mwaka 2020/2021 ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya uchumi wa Taifa mwaka 2021; Sura ya 6 ihusuyo rasilimali watu; katika hotuba wa Hali ya Uchumi ya Taifa kwa mwaka 2021 kipengele cha mgawanyiko kimkoa na pamoja na msongamano wa watu Tanzania Bara. Mheshimiwa Waziri kuna wimbi kubwa la Watanzania kutoka mikoani kukimbilia mkoa wa Dar es Salaam ambako sasa idadi ya Watanzania yapata 5,526,638 sawa na asilimia 9.6 ya Watanzania wote huku mkoa wa Katavi idadi ni ndogo ipatayo watu 842,200 ya Watanzania wote sawa na asilimia 1.5.

Vilevile msongamano wa watu katika mkoa wa Dar es Salaam wastani wao yapata watu 3,967 kwa kila kilometa ya mraba wakati Lindi msongamano ni wastani wa watu 16 kwa kila kilometa ya mraba. Sababu kubwa ya watu wengi kukimbilia mkoa wa Dar es Salaam imeelezwa katika hotuba ya hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021 kuwa ni upatikanaji wa huduma za kijamii na fursa za kiuchumi ambazo maeneo mengi hasa ya pembezoni zinakosa fursa hizo. Mfano katika Halmashauri ya Wilaya Mtwara Vijijini yenye kata 22 na vijiji 107 kunakosekana huduma za kijamii zifuatazo; vituo vya afya viko vinne tu kati ya 22 vinavyohitajika; zahanati zipo 29 kati ya 107 zinazohitajika; umeme upo kwenye vijiji 33 tu kati ya vijiji 107 hali inayowafanya vijana na akina mama kukosa fursa za kujiajiri kwenye viwanda vidogo vidogo na shughuli za kuuza biashara za maji baridi, soda baridi na kadhalika.

Pia barabara yake kuu kutoka Mtama - Kitangari - Amkeni lami ipo kilometa 20 tu kati ya kilometa 74 zilizopo hali ambayo magari yanayopita sio rafiki, hayamalizi safari kutokana na ubovu. Sababu ni kuwa wafanyabiashara hawapeleki magari yao mazima; bei ndogo za mazao mfano korosho na ukosefu wa bei kwenye mazao mchanganyiko

mfano njugu, mbaazi, mihogo husababisha watu wake kuhamia Dar es Salaam kwa wingi kufuata huduma bora.

Ushauri wangu; imefika wakati sasa Serikali ihakikishe inazipeleka fursa za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Newala ili kuwafanya watulie kwenye maeneo yao na kufanya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri; nashauri ibakie kwenye uwiano wa zamani wa 4:4:2 ili zilete tija kwa wananchi kwani kwenye halmashauri zenye mapato kidogo watapata kiasi kidogo kisicholeta tija kwa wanufaika.

Kwa kuwa fedha za 10% ya mapato ya ndani hutolewa kama *revolving fund,* basi kiasi cha kwenda kwa Wamachinga (miundombinu) basi zichukuliwe huko ingawa ipo changamoto kubwa ya kutokusanywa kwa fedha hizo kutoka kwa wale waliokopeshwa. Nashauri pia usimamizi uwe imara kwenye marejesho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vitambulisho vya Taifa *(NIDA);* wapo Watanzania hawajapata vitambulisho vya *NIDA* hadi sasa. Wapo ambao wametengenezewa viitambulisho hivyo lakini hawajavipokea kutokana na kupelekwa maeneo tofauti na wanakoishi/kusiko kata zao. Hali hii imesababisha upotevu wa vitambulisho hivyo kwa kuwa ni vigumu kuvipata kwa kuwa havina namba za simu za mhusika.

Ushauri wangu; vitambulisho viharakishwe utengenezaji wake kwani ni kitambulisho muhimu kinachohitajika kila eneo la huduma; vipo vitambulisho vinaisha muda wake mwaka Disemba 2023 na 2024. Serikali ijipange na ongezeko la watu ambao watakuwa hawana vitambulisho ifikapo mwaka 2023/2024.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nipomngeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanayoifanya, Mwenyezi Mungu amjaalie siha na afya njema ili azidi kutumikia wananchi. Pia nimpongeze Waziri wa Fedha pamoja na timu yake yote kwa kuleta bajeti ya kihistoria ambayo Watanzania wameielewa sana.

Mheshimiwa Spika, shukrani; nianze kwa kumshukuru Rais wetu Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kutupa fedha nyingi za miradi ya maendeleo katika Jimbo la Lushoto, tunamshukuru mno Rais wetu, kwani katika miradi ya maji tumepata zaidi ya shilingi bilioni tatu kwa kipindi cha mwaka mmoja tu. Tumepata pesa zaidi ya shilingi bilioni tano kwa ajili ya barabara. Pia tumepata shilingi bilioni moja kwa ajili ya vituo vya afya viwili. Tumepata zaidi ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya maboma ya madarasa ya shule za msingi pamoja na sekondari.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumepata zaidi ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuongeza mabweni pamoja na madarasa katika sekondari ya Shambalai na pia tumepewa shilingi milioni 470 kwa ajili ya kujenga sekondari kwenye kata ambazo hakuna sekondari na kadhalika, Mwenyezi Mungu amjaze majazo mema na ampe afya njema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu asilimia kumi; naomba kuishauri Serikali kutotoa hii asilimia tano kutoka kwenye asilimia kumi, kwani hii itakuwa sio sawa kwa sababu asilimia hii yenyewe haitoshi. Ushauri wangu kwa Serikali iongeze asilimia tano kwenye asilimia kumi, hiyo ndiyo ipewe wamachinga, pamoja kwamba bado hakujafanyika uchambuzi wa kina wa kumjua mmachinga ana tabia gani katika kufanya kazi zake. Niiombe Serikali iwachunguze wamachinga hasa kwa kile ambacho Serikali inachotaka kuwapa, kwa sababu leo hii tukija na suala la kuwajengea sehemu za kufanyia biashara huoni ya kwamba Serikali

itakuwa inapata hasara, kwani hakuna mtu asiyejua tabia za wamachinga kuwa ni ya kutembea mitaani au kuweka biashara yake kwenye mzunguko wenye watu wengi.

Mheshimiwa Spika, afya; wananchi walio wengi hasa wanaoishi vijijini hawapati huduma bora ya afya na maeneo mengine hakuna kabisa huduma hiyo ya afya, niiombe Serikali kwa kuishauri ijenge vituo vya afya tena vyenye hadhi ili kunusuru maisha ya wananchi wetu waishio vijijini, mfano kwenye Jimbo la Lushoto kuna uhaba wa vituo vya afya kama ifuatavyo; Kituo cha Afya Gare, Kituo cha Afya Kwai, Kituo cha Afya Makanya na Kituo cha Afya Malibwi.

Pamoja ya kwamba zipo kata nyingi ambazo hazina vituo vya afya, nimeona nianze kata hizo hapo juu, kwa hiyo niiombe Serikali katika kuchambua bajeti hii, Serikali itenge fedha kwa ajili ya vituo hivi vya afya nilivyoorodhesha hapo juu.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya barabara; katika Jimbo la Lushoto lina changamoto ya barabara kama inavyojulikana Lushoto ni ya milima na mabonde makubwa, hivyo kusababisha wananchi wengi kupata hasara ya kutoa mazao yao shambani kwa sababu ya miundombinu ya barabara kuharibika kila wakati na ukizingatia baadhi ya barabara zinatengewa pesa kiduchu (kidogo) ambazo fedha hizo hazikidhi utengenezaji wa barabara hizo hasa barabara ya Dochi - Mombo kilometa 16; barabara ya Dochi - Gare kilometa 10; barabara ya Kwefingo - Kwesine kilometa 14; barabara ya Migambo - Kifungilo kilometa 9; barabara ya Kwekanga - Mlola kilometa 11 na barabara ya Kwemakame – Ntambwe - Ng'aloi - Mzizima. Hizi ndiyo barabara ambazo ndizo zenye changamoto kubwa na ndiyo barabara zenye kuingiza mapato mengi Serikalini. Kwa hiyo naomba hizi nazo zitengewe fedha za kutosha hasa kwa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu pia Jimbo la Lushoto kuna upungufu wa vyumba vya madarasa ya sekondari na shule za msingi kama ifuatavyo; Shule ya msingi Gare A na B; Shule ya Sekondari Kwemashai na Kwemahai; Ngulu; Kilangwi; Mshizii; Handei Gare; Makanka; Shule ya Sekondari Masange, Masange; Milungui; Kwezinga; Shule ya Sekondari Mkuzi, Migambo; Kwaboi; Kwai; Shule ya Sekondari Kireti, Kireti; Kwemakame; Shule ya Sekondari Ntambwe, Ntambwe; Ngindoi; Shule ya Sekondari Malimbwi, Malimbwi; Mategho; Kweboma; Shule ya Sekondari Makole, Makole; Ungo; Hondelo; Shule ya Sekondari Mazashai, Mlongwema; Mgambo; Kwemshazi; Shule ya Sekondari Mdando, Mdando; Shule ya Sekondari Kwetango, Kweulasi; na Lunguza. Hizi ndiyo shule za msingi pamoja na sekondari ambazo ndiyo zenye uhitaji wa maboma kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kikokotoo; yapo malalamiko makubwa kwa watumishi hasa wale wenye mshahara wa chini ya milioni moja kuwa kikokotoo kinawaumiza sana maana wanapostaafu huwa wanapata mafao yao kidogo mno kiasi kwamba pesa hizo kidogo wanazopewa hawawezi kuwekeza kwenye jambo lolote la kuongeza kipato. Kwa hiyo naomba kuishauri Serikali itoe kikokotoo hiki ili watumishi waweze kutimiza malengo yao wanapostaafu.

Mheshimiwa Spika, suala la uchumi; ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 73 imeandika kuwa Serikali itajenga kiwanda kikubwa cha dawa kwa kutumia miti dawa yetu na mimea dawa yetu, lakini mpaka leo bado hakuna dalili ya kujenga kiwanda hicho wakati nchi yetu ina miti dawa na mimea dawa ya kutosha.

Naomba niishauri Serikali yangu tukufu; kwanza kuharakisha kujenga kiwanda hicho dawa; kuwatafuta wataalam wote wa tiba asili ili waweze kupeleka malighafi kiwandani; kuwawezesha vifaa vya kazi waganga wa tiba

asili; na kuwawezesha kwa kuwapa maeneo ili waweze kupanda zao hilo kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, yakifanyika yote hayo ni imani yangu nchi itaongeza pato la Taifa kwa asilimia 20 kwa kupitia dawa zetu za asili na asilimia 20 tutaipata hasa kwa kuziongezea thamani dawa zetu hasa kwa kuzitengeneza kwa vidonge na kwa sindano, tukifanya hivyo kwanza tutakuwa tumekidhi mahitaji ya dawa kwa wananchi wetu na *MSD* watakuwa wamepunguza kwa kiasi kikubwa kuagiza dawa nje badala ya kuagiza dawa nje sisi ndiyo tutauza nje.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaaliwa miti dawa ambayo inatibu magonjwa mengi na hasa yale ambayo sio ya kuambukizwa kama kansa, tezi dume, figo, kisukari, *pressure,* bawasili, uvimbe na vidonda vya tumbo na gesi na kadhalika. Magonjwa yote haya dawa zake zimeshafanyiwa utafiti na kuonekana zinasaidia kwa asilimia 95 pamoja na dawa ya UVIKO-19, zimefanya vizuri sana kwenye janga la UVIKO-19.

Niendelee kusisitiza kuwa wataalamu wetu wawashirikishe waganga wa tiba mbadala ili miti dawa yetu iweze kuongeza pato la Taifa, na uzuri wa dawa zetu za asili ni *organic* hazina *side effect* yoyote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na niendelee kusisitiza Serikali iwawezeshe waganga wa tiba asili kwa kuwapa ruzuku kama secka nyingine zinazopewa ruzuku.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kuhusu kodi ya *flat rate* ya shilingi 3,500,000 kwamba ipunguzwe lakini pia izingatie ukubwa au *capacity* ya gari au *tonnage*. Kodi hii itozwe kwenye magari ya abiria na mizigo, na magari makubwa tu. Hawa wenye magari madogo kama *canter* na *hiace* na *coaster* kuwekwe

viwango vingine kutokana na kukubwa wake; "(xi)Kutoza kiwango cha mfuto *(flat rate)* cha shilingi 3,500,000 ikiwa ni kodi ya mapato inayopaswa kulipwa kwa kila magari ya mizigo na mabasi ya abiria kwa mwaka. Lengo la hatua hii ni kuongeza uwazi katika makadirio ya kodi baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na walipakodi, kuweka mfumo wa kodi unaotabirika na kuongeza mapato ya Serikali. Hatua hii inatarajiwa kuiongezea Serikali mapato yanayokadiriwa kuwa shilingi milioni 141,052."

"(iii) Kutoza ushuru wa bidhaa wa shilingi 700 kwa kilo ya bidhaa za sukari *(sugar confectionery)* zinazoingizwa kutoka nje ya nchi na shilingi 500 kwa kilo ya bidhaa za sukari zinazozalishwa hapa nchini zinazotambuliwa kwa HS Code 1806.31.00, 1806.32.00, 1806.90.00, (chokoleti); 1905.31 (biskuti); na 1704 (chingamu). Viwango tofauti vinapendekezwa ili kulinda viwanda vya ndani. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 34,453.87; kwa kuwa nia ni kulinda viwanda vya ndani basi na kama ambavyo umepunguza makali kwa viwanda vingine kutokana athari za UVIKO na kwa kuwa bidhaa hizi zinatumiwa zaidi na watoto wetu, basi naomba hiyo kodi uiondoe kabisa. Ni muhimu sana!

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 72(90) ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini, Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kuimarisha miundombinu wezeshi ya usafirishaji na nishati; kuhakikisha uhimilivu wa viashiria vya uchumi jumla; na kuwianisha tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na Wizara na Mamlaka za Udhibiti kwa lengo la kupunguza na kurahisisha ulipaji wake na kuzifuta baadhi ya tozo na ada za kero. Aidha, mwaka 2022/2023, Serikali itaendelea kufanya marekebisho ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya sheria mbalimbali. Marekebisho hayo yanalenga kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, hususan katika sekta ya

viwanda, uwekezaji na biashara pamoja na kuongeza ajira, mauzo nje, mapato na akiba ya fedha za kigeni.

Mapendekezo ni kuomba kufutwa kwa kodi ya pango la ardhi kwa shule/vyuo binafsi na za taasisi za dini kwa kuwa zinatoa huduma na kusaidia na Serikali katika kuboresha elimu nchini. Pia watoto hawa ni Watanzania ambao wenzao wanasomeshwa bure kuanzia shule ya msingi mpaka kidato cha sita. Muhimu!

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia Bungeni kwa kuzungumza tarehe 22/6/2022 napenda kutoa mchango katika maeneo yafuatayo; ukusanyaji wa kodi, mapendekezo ya matumizi sahihi ya mali na rasilimali za Taifa na barabara ya Kibena/Stop Lupembe - Madeke hadi Morogoro/Ifakara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi, mosi, napendekeza kuwa Serikali iongeze rasilimali watu katika kutatua migogoro nchini. Bodi na Tume za Kodi zilizopo kwa mujibu wa sheria ni ndogo na zinazunguka nchi nzima kutatua migogoro ya kodi. Hii ndiyo sababu kesi nyingi za kodi haziishi. Napendekeza turekebishe sheria ili kuongeza wigo wa taasisi hizi ili ziwepo kila mkoa nchini.

Pili, kuhusu ushuru na kodi kwa biashara za misitu hasa mbao, nguzo na magogo, napendekeza kuwa ushuru ujulikane *(flat rate)* kwa kuweka kiwango ili kila mfanyabiashara ajue kodi anayopaswa kulipa kutokana na ukubwa wa gari au mzigo aliyobeba yaani kwa mfano, gari aina ya fuso shilingi 500,000; *canter* shilingi 300,000 na kadhalika. Hii siyo itaondoa usumbufu kwa wafanyabiashara kwa kusumbuliwa sana barabara, bali pia itaongeza sana mapato ya Serikali yetu. Hivi sasa pesa nyingi zinachukuliwa na Maafisa wa Kodi wasio waaminifu. Serikali inapoteza mapato mengi sana.

Kuhusu matumizi sahihi ya rasilimali za Taifa; Halmashauri ya *Njombe DC* Serikali imejenga Hospitali ya Halmashauri katika Kata ya Matembwe kwa thamani ya zaidi ya bilioni nne hadi sasa lakini majengo haya mengi hayapokei wagonjwa wengi maana kila kijiji kuna zahanati na kila kata tunajenga kituo cha afya. Nashauri hospitali hii itumie baadhi ya majengo yake kama chuo cha afya au wauguzi ili majengo haya ya thamani yasiachwe na kubaki kuwa pango la popo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara; napendekeza Serikali ianze ujenzi kwa awamu yaani angalau kilometa 10 kila mwaka maana hii ni ahadi ya Serikali na hasa Mheshimiwa Rais wetu na ni ahadi ya muda mrefu tangu Awamu ya Tatu na wananchi wamekuwa na manung'uniko makubwa sana kwa Serikali jambo ambalo siyo zuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavvyo na nikianza na pongezi; kwa moyo wa dhati kabisa nampongeza na kumshukuru Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake mahiri ambao ameuthibitisha kwa kutekeleza miradi ya maendeleo mingi na mikubwa tena ya kihistoria nchi nzima ndani ya mwaka mmoja.

Nampongeza sana Waziri wa Fedha na Mpango Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Naibu wake pamoja na watendaji wake wote Wizarani wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri sana wanayoifanya lakini pia kwa hotuba nzuri iliyosheheni taarifa zote muhimu, hakika hotuba imeweka wazi nchi ilikotoka na tunakoelekea katika kutafuta maendeleo kwenye sekta zote.

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukurani kwa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa jimboni Arumeru Mashariki; barabara za Malula Kibaoni kupitia Kingori Madukani, Maruvango, Leguruki hadi Ngarenanyuki shilingi 1,000,000,000; na Akheri kwenda Nkoanrua hadi Ulonga pamoja na kivuko cha Poli/Seela shilingi 500,000.

Kwa upande wa sekta ya afya; Kituo cha Afya Mareu shilingi 500,000; na Hospitali ya Wilaya EMB na nyumba ya mtumishi shilingi 390,000. Aidha kwa upande wa elimu; madarasa 70 shilingi 1,400,000,000; na kwa upande wa wa sekta ya maji; Mradi wa Maji Patandi na Nkoarisambu shilingi 2,700,000,000 Mkandarasi yuko *site;* Kijiji cha Nshupu shilingi 269,000,000; Ngongongare Kiwawa shilingi 1,600,000,000; Imbaseny, Maji ya Chai, Kikatiti shilingi 4,300,000,000; na Kijiji cha Nkure shilingi 502,000,000.

Mheshimiwa Spika, changamoto kwanza ni barabara ya Mbuguni kuanzia Tengeru Sokoni hadi Mererani ikipitia Kikwe inaunganisha mikoa miwili ya Arusha na Manyara lakini pia ni muhimu biashara ya madini ya Tanzanite yanayochimbwa Mererani kwa maana ya kuipeleka sokoni.

Kuhusu ahadi za viongozi wakuu; barabara ya Akheri kuanzia Sangis hadi Ndoombo iliahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami na Rais wa Awamu ya Nne Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Januari, 2012 wakati wa mazishi ya aliyekuwa Mbunge wetu Marehemu Jeremiah Solomon Sumari. Pia barabara ya Kingori kuanzia Malula Kibaoni hadi Ngarenanyuki nayo iliahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Barabara hii ni muhimu kwa shughuli za utalii kwa sababu iko upande wa Mashariki ya Hifadhi ya Arusha *(ANAPA)* na inazunguka Mlima Meru kwa upande wa Mashariki na Kaskazini na kuungani barabara kuu ya Moshi/Arusha na Arusha/Namanga. Kwa hiyo, itakuwa barabara ya mchepuo upande wa Mashariki ya Jiji la Arusha

lakini pia unapunguza umbali kutoka Moshi kwenda Namanga kwa kilometa 33.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kwa heshima na taadhima Serikali itekeleze ahadi hizi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza wewe binafsi kwa kazi nzuri unayofanya ya kuliongoza Bunge letu na pia nampongeza Waziri wa Fedha na Naibu wake.

Naomba kuchangia kwenye eneo la ajira kipengele cha uzoefu; eneo hili liunganishwe kwenye mafunzo vyuoni, mwanafunzi apate muda wa miezi sita au mwaka mmoja kadri itakavyoonekana inafaa aweze kupata uzoefu ili akiingia kwenye soko la ajira kusiwe tena na kipengele cha uzoefu kwani waombaji wengi wa ajira wanakuwa *fresh from school* hivyo kipengele cha uzoefu kuwa kikwazo kwao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya, pia kwa bajeti nzuri ambayo inaenda kugusa maisha ya Watanzania hasa katika sekta ya elimu kwa kufuta ada mpaka kidato cha tano na sita. Pili kwa kutoa ruzuku kwenye mbolea na mafuta pamoja na kufuta kodi ya *VAT* kwenye mafuta ya kula, hiyo ni habari njema sana kwa Watanzania.

Pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya hasa kwa maandalizi ya bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, mimi leo mchango wangu kwenye bajeti kuu utajikita sana kwenye mambo yafuatayo; kwanza ni kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato ili kuweka kiwango cha asilimia 3.5 kwa walipakodi wenye mauzo yanayozidi shilingi 11,000,000 lakini yasiyozidi shilingi 100,000,000 kwa mwaka *(presumptive regime)*. Lengo ni jema sana la kuweka uwazi na kurahisisha makadirio na ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba kuishauri Serikali kwamba kutokana na changamoto za kiuchumi ambazo dunia inapitia kama vile athari za UVIKO-19 na vita ya Ukraine na Russia uendeshaji ya biashara hasa kwa wafanyabiashara wadogo umekuwa mgumu sana. Kwa hiyo Serikali ione namna ya kupunguza *rate* hiyo walau ifikie asimia mbili, hii itapanua wigo wa wawalipa kodi wa kati na pia kuzifanya biashara ndogo kushamiri zaidi na zaidi.

Pia tuone uwezakano wa kuanza kutoa *EFD machine* bure kwa wafanyabiashara waliopo kwenye bandi hii ambao wengi wao ni wadogo.

Niipongeze Serikali kwa kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 10 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ili kumpa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha mamlaka ya kusamehe kodi ya mapato kwa wawekezaji mahiri maalumu baada ya kuidhinishwa na *National Investment Steering Committee (NISC)* kwa mujibu wa kifungu cha 20(8) cha Sheria ya Uwekezaji Sura ya 38, pamoja na kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo ni jema kuondoa urasimu unaoweza kuwakatisha tamaa wawekezaji.

Nitakuomba Mheshimiwa Waziri unapofanya hitimisho, utoe ufafanuzi kama marekebisho haya yanahusisha na ile miradi ya kimkakati ambayo jumla ya kodi yake haifiki bilioni moja kwa muda wote wa mradi kwani kwa utaratibu wa sasa na sheria iliyopo msamaha wa kodi kwenye miradi ya *nature* hiyo haihitaji *approval* ya Baraza ya Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana pia sana Serikali kwa kutoza Kodi ya Mapato ya asilimia mbili kwenye malipo yanayofanywa kwa watoa huduma za kidijitali wa kigeni. Lengo la hatua hii ni kuongeza wigo wa kodi na kuzingatia kanuni za usawa za kodi na hii tu itaweza kuliingizia Taifa zaidi ya bilioni 4.8 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, nimuombe tena Waziri unapo-*wind up* atoe ufafanuzi juu ya kodi hii ya mapato kwa watoa huduma wa ndani na wenye makazi ya kudumu hapa nchini. Je, nao watahusika na kodi hii au itakuwa *offsetted* kutoka kwenye kodi yao ya mapato ya mwaka wanayoitoa?

Pia Serikali imeamua kutoza kiwango cha mfuto *(flat rate)* cha shilingi 3,500,000 ikiwa ni kodi ya mapato inayopaswa kulipwa kwa kila magari ya mizigo na mabasi ya abiria kwa mwaka. Ni kweli lengo la hatua hii ni kuongeza uwazi katika makadirio ya kodi baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na walipakodi, kuweka mfumo wa kodi unaotabirika na kuongeza mapato ya Serikali.

Katika hili naomba atakapokuwa ana-*wind up* Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi je, mabasi yanayolengwa hapa ni namna gani? Je, ni yale yanayofanya safari za mikoani tu au hata daladala *(in town bus services)?* Hata hivyo naomba kuishauri Serikali pia kutathmini kwa kina sana athari za kodi hii hasa kwenye kipindi hiki ambapo Taifa linajitahidi katika kupambana na athari za kiuchumi za UVIKO-19 na vita ya Urusi na Ukraine. Sekta hii imeathirika sana na upandaji wa bei ya vipuri *(spare parts),* kwa hiyo ongezeko la

kodi hiyo kwa kiwango hicho inaweza kuleta athari ya mfumuko wa bei kwa mlaji wa mwisho.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia nikianza na sera za kikodi zinahitaji kulinda viwanda vyetu. Bado pamoja na bajeti kulifanya hili, kwenye viwanda vyetu vya chuma na mabati vinaendelea kupata ushindani usio sawa. Wawekezaji kutoka China wanaofanya shughuli za kutengeneza mabati wana *take advantage* ya kutokuwa na kodi kwa kiwango cha 35%. Bado *import duty* ipo kwenye 25%.

Pili wawekezaji bado wana *under declared* thamani ya *imports* zao. Hivyo nina *suggest* kuwe na *Minimum Import Price (MPI)* kwa *materials* zote.

Mheshimiwa Spika, kwenye *flat materials* za *Pre Engineered Buildings* ambazoni muhimu kwa ujenzi wa maghala, *green houses, show rooms,* bado zimewekewa *rate* ambayo inafanya watengenezaji wa vifaa hivyo nchini wanashindwa kushindana na waagizaji wa *finished product*. Ili kuleta usawa Serikali ingetoa *remission* kwenye *code* namba 7210.49.00.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, ajiandae.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani nyingi kwa fursa hii. Natangulia kusema, naunga mkono hoja. Naomba kutoa pongezi nyingi sana kwa Waziri wetu wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa mapendekezo mazuri sana aliyoyaleta kupitia hotuba yake ya bajeti ambayo tunaijadili, na ninaomba sote tuiunge mkono leo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Naibu Waziri Mheshimiwa Hamad Chande pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Emmanuel Tutuba na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi nzuri na mapendekezo mazuri sana ambayo yapo mezani kwetu.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri anawasilisha hotuba yake hapa alituambia mara kadhaa kwamba anayoyapendekeza hapa ni maelekezo mahususi ya Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo, kupitia maelezo yangu haya, nampenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa mapendekezo mazuri sana yaliyopo kwenye bajeti mengine ambayo nitajaribu kuyainisha hapa ambayo kwa kweli yatatuvusha na kutupeleka vizuri sana mbele ya safari. Hongera sana Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imetajwa kwamba ni bajeti ya uzalishaji na utaiona tu katika kiwango cha fedha ambacho kimepelekwa katika Wizara ya Kilimo pamoja na mambo mengine. Pia ni bajeti ya kuainisha matumizi mazuri ya fedha za Serikali. Kwa mfano, hatua ambazo zimechukuliwa kuongeza ukaguzi wa fedha za Serikali kuhakikisha kwamba matumizi yanatumika kwa namna ambayo inaleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, juu ya yote, hii ni bajeti ya elimu. Yapo mapendekezo mahususi na makubwa sana ambayo yameletwa kupitia bajeti hii kwa ajili ya kuendeleza elimu hapa nchini. La kwanza kabisa ni hili la kuhakikisha kwamba sasa nchi yetu inatoa elimu bila ada kuanzia Darasa la Kwanza mpaka Kidato cha Sita.

Mhewshimwia Spika, napenda sana kuipongeza Wizara na kumpongeza sana Rais wetu, kwa sababu tuliambiwa ni maelekezo mahsusi ya Rais wetu. Najua ada ilikuwa shilingi 70,000. Wapo watu wanadhani hicho ni kiwango kidogo

sana, lakini wapo Wabunge wengi hapa wanafahamu kwamba wapo wazazi walikuwa wanashindwa kutoa hizo Shilingi 70,000/= kwa ajili ya kuwapeleka watoto wao kwenda kusoma Kidato cha Tano na cha Sita. Wapo Wabunge wengi humu tayari walishalipia vijana wengi kwa ajili ya kwenda kusoma. Kwa hiyo, huu ni mzigo tumepunguza kwa wazazi ili Watanzania waweze kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua vilevile hii ni sehemu ya gharama ya kusoma Kidato cha Tano na Kidato cha Sita. Tutapitia miongozo yote tukishirikiana na wenzetu Mheshimiwa Bashungwa, TAMISEMI na wenzetu wa Hazina kuangalia ile miongozo ili kusiwe na mzigo mkubwa ambao unakinzana na azma ya Rais wetu ya kutoa elimu bila ada mpaka Kidato cha Tano na cha Sita.

Mheshimiwa Spika, tutafanya haraka kupitia tunapitia *joining instructions* zote na kuangalia ni mizigo ipi ambayo imewekwa na Wabunge wengi wamezungumza huku kwamba sasa tumeondoa Shilingi 70,000/=, lakini gharama nyingi zipo sehemu nyingine. Tutafanyia kazi maelekezo ya Rais wetu kuhakikisha kwamba tunapunguza michango yote ambayo haina maana na haina tija katika shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima niseme vilevile, katika gharama za kusoma, hasa sisi tunaopitia vijijini, wazazi wengi sana wanapata shida. Kuna wazazi wakati mwingine wakiona mtoto amefaulu, wanaona kama ni mzigo kwa sababu ya gharama. Kuna mambo ya sare nakadhilika. Nashukuru sana Wizara ya Fedha na Mipango kwa kutenga fedha kupitia dirisha la *TASAF* kuweza kusaidia juhudi za elimu kwa familia ambao uchumi wake ni duni kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa *TASAF* unatusaidia sana kuanisha ni familia gani zinahitaji msaada katika vijiji. Kwa kutumia ubunifu huu wa Wizara yetu ya Fedha, itatupunguzia

ile adha ya kujaribu kujua ni nani kweli anastahili kusaidiwa na Serikali na nani anaweza akachangia. Hii kwa kweli itaenda kupunguza sana mzigo kwa familia nyingi na tunaamini baada ya *experiment* ya bajeti hii, tunaweza tukaongeza pia mwaka unaofuata kupanua wigo wa kusaidia familia nyingi ili kila mtoto wa Kitanzania aweze kusoma bila kujali uwezo wa mzazi wake, asiache kusoma kwa sababu tu mzazi wake hana uwezo wa kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila Mbunge amezungumzia umuhimu wa elimu ya kati, kwa sababu tunafahamu kwa sehemu kubwa sana elimu ya kati inatoa ujuzi na ufundi ambao unamwandaa mhitimu kuajirika na kuajiriwa kwa urahisi zaidi. Ndiyo maana kilio kikubwa cha Wabunge wote ni kuhakikisha kwamba kila wilaya inapata *VETA*. Tunashukuru sana kupitia bajeti hii, tumetengewa fedha sasa za kujenga vyuo vya *VETA* ili azma ya Rais wetu ya kuhakikisha kwamba kila wilaya inapata Chuo cha *VETA,* tuianze sasa na kuikamilisha.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri wa Fedha na Mipango kwa kututengea fedha na sisi Wizara ya Elimu tutasimamia kwa makini ujenzi huo. Natoa wito kwa Wabunge tusaidiane, wakati wa kuanza kugawa fursa hizi mwenye ardhi anapata kipaumbele cha kwanza. Kwa hiyo, tuanze kutatufa ardhi tusije tukapata matatizo.

Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi, ngoja niseme lingine. Tunajenga chuo kikubwa cha TEHAMA kwa maelekezo ya Rais wetu hapa Dodoma kupitia bajeti hii, tunashirikiana na wenzangu, Mheshimiwa Nape Nauye kwa ajili ya yale aliyokuwa anasema msemaji aliyepita hapa sasa hivi. Kwa mara ya kwanza tunapeleka *campus* za vyuo vikuu kwa ajili ya kutoa *degree* za ujuzi, siyo *academic degree,* za ujuzi katika mikoa kadhaa kupitia mradi wa *HEET* ambao Mheshimiwa Waziri ameusema.

Mheshimiwa Spika, tutajenga *campus* Lindi, Kagera, Katavi, Rukwa, Mwanza, Tanga, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Simiyu, Manyara, Ruvuma, Singida na Dodoma hapa kwenye TEHAMA. Kwa upande wa Zanzibar kwa ajili ya kusaidia uchumi wa bluu kwa sababu elimu ya juu ni suala la Muungano, *SUZA* wametengewa fedha lakini *Institute of Marine Science* ambayo ni *campus* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na yenyewe tunaenda kukamilisha ujenzi kule ili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kisaidiane na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuendeleza uchumi wa bluu katika ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, *degree* au diploma ambazo tutazitoa huko zote zitakuwa za ujuzi, siyo za *academic*. Kwa kila chuo ambacho kitakuwa kinashikilia hizi *campus* tumewaambia watafanya mpango wataleta tutaidhinisha, mtu akisoma kule anafanya kama ni suala la *leather technology* inakuwa ndiyo *degree* ya *Leather Technology* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu nasema ukweli haya ni maagizo mahsusi ya Rais wetu. Alisema mkopo ambao tumechukua *World Bank* usiishie kwenye vyuo ambavyo tayari vipo, tutawanye fursa hizi mikoa yote na tuhakikishe kwamba tunakopeleka kule tunaenda kuleta ujuzi ambao unaongeza uwajirikaji na kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kueleza vyuo vile pamoja na hizi *campus,* vyuo vingine vyote vya Serikali 14, tunaenda kuendeleza miundombinu yake na kuna fedha za kupeleka wahadhiri kwenda kusoma. Tutapenda wengi wakasome kwa ajili ya maandalizi ya kuendeleza hizi *campus* mpya kwa ajili ya kutoa elimu ya ujuzi. Kwa mfano, kwa Kigoma kwa Mheshimiwa Ndalichako, ambako kinapelekwa *campus* kwa ajili ya mambo ya tiba na Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema tiba inaweza ikatumika kwa ajili ya kuleta watalii kwa nchi jirani. Tutahakikisha kwamba tunapeleka

Wahadhiri kwenda kusoma kwa ajili ya kuja kutoa taaluma hiyo katika Mkoa wa Kigoma. Tutafanya hivyo pamoja na chuo cha Mloganzila ambacho kiko Pwani na vyuo vingine vyote.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga, Mheshimiwa.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, ajiandae.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kupata fursa hii kuchangia katika bajeti hii kubwa ya Serikali, lakini pia nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nianze pia kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na niwapongeze na timu yake yote bila kuwataja mmoja, mmoja kwa kutuletea bajeti nzuri, bajeti ambayo tukiisimamia vizuri inakwenda kutekelezeka vizuri na tutaondoa changamoto kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi tunatambua kwamba ni Wizara wezeshi na katika mipango yote ya Serikali ilivyopangwa tegemeo kubwa pia ni kuhakikisha kwamba Wizara ya Ardhi tunasimamia shughuli ambazo tumepewa

kuzifanya ili kuwezesha kazi zote ziweze kufanyika. Tunatambua kama ni kilimo watahitaji ardhi, kama ni watu wa madini pia ardhi itatakiwa, watu wa mifugo vilevile lakini na changamoto ambazo zipo katika Sekta ya Ardhi tumejiandaa vizuri kuweza kuzipatia ufumbuzi. Tunatambua wazi Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, katika kipindi kifupi ameweza kuitangaza nchi kwa upana wake katika maeneo mbalimbali. Wabunge hapa wamechangia maeneo mengi wakizungumzia habari ya utayari pia wa Serikali katika suala zima la kupokea wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa tu kwamba tumejiandaa katika kuona hatma ya kutekeleza yale yote yaliyopangwa inafanyika. Nichukulie mfano mmoja kwenye kilimo ambapo walisaini mikataba zaidi ya 36 kuhakikisha kwamba kilimo kinawekezwa. Tumeshazungumza na Wizara ya Kilimo wenye sekta yao, kuhakikisha kwamba suala la utambuzi wa maeneo ambayo yatafaa kwa kilimo yanatambuliwa mapema, yanapimwa na yanakuwa *gazetted* ili kuwa tayari kupokea uwekezaji mkubwa. Tunafanya hivyo kwa sababu tunajua tusipofanya hivyo tunaweza tukaleta changamoto ambazo ni za migogoro ambayo haina tija.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo pia tunakwenda kulifanya katika suala zima, tayari tumekwishatenga eneo ambalo lina ukubwa wa ekari zaidi ya laki 247 kwa ajili ya uwekezaji wowote utakaokuwa umekuja. Kwa hiyo, kwa upande huo tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa sababu ilikuwa ni moja ya maagizo yake kuhakikisha tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Wabunge 14 wamechangia, lakini ilikuwa ni pamoja na Kamati ya Bajeti katika kututaka tupanue wigo wa kukusanya kodi, lakini na kuondoa migogoro ambayo ipo. Napenda nilithibitishie Bunge lako

kwamba Wizara ya Ardhi katika suala zima la kuhakikisha haya yote yanafikiwa, tumeendelea kuelekeza nini cha kufanyika katika maeneo ambayo yamekuwa na changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala zima la migogoro ile ya vijiji 975 ambavyo vilivyotajwa tayari kama Wizara tumeshaifikia mikoa, ile timu ya Mawaziri nane ambayo ilikuwa inaongelewa tumefikia mikoa 12 kati ya 26 iliyowekwa. Tayari katika maeneo hayo Serikali kupitia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan waliridhia katika kipande hicho kuweza kufuta mapori 12 ambayo yanakwenda kufanyiwa kazi ya kuwapa wananchi. Katika vijiji vyote ambavyo vimefikiwa katika hilo, kwenye hatma ya kuondoa migogoro tumefikia vijiji 412 kati ya 920 ambavyo wananchi wanaenda kukaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika suala zima la uwekezaji pia tunajua watu watakwenda katika maeneo ya utalii. Kama kuna migogoro ya mipaka katika maeneo hayo ni wazi mazingira hayatakuwa mazuri katika kupokea. Kwa hiyo, Serikali kupitia Mawaziri Nane wa Kisekta, tumefanya kazi hiyo ambayo tunajua ni chanzo kilichokuwa na migogoro mikubwa katika suala zima la kukuza utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Wabunge pia kama watatu walizungumzia suala la Mipango Miji. Kwamba tunahitaji kupanga Miji yetu vizuri ili tuweze kuona kwamba inafikika na inakuwa salama kwa makazi, lakini pia katika kuvutia uwekezaji. Najikita kwenye uwekezaji kwa sababu ni Sekta ya Ardhi ambayo inaweka wigo mpana wa kupokea hayo yote yanayozungumzwa.

Mheshimiwa Spika, suala la Mipango Miji ni takwa la Kisheria na limetajwa katika kifungu cha 7(1) ambayo inazitaka Halmashauri zetu kutenga maeneo hayo na kuweka kufanya Mipango Miji katika maeneo yao. Sasa kama hili takwa la kisheria Mamlaka hazifanyi utekelezaji wa hilo, ni

wazi migogoro itakuwepo. Kwa hiyo Serikali kwa kushirikiana, Wizara yangu na TAMISEMI, tutahakikisha tunafuatilia kwa karibu halmashauri zetu kuhakikisha zimeweka mipango kabambe, zimetenga maeneo ya uwekezaji. Pia katika yale maeneo ambayo yanahitaji kupangwa, kupimwa na kumilikisha, Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan, imetoa zaidi ya bilioni 50 kwa ajili ya kufanya kazi hiyo, tumekopesha kwenye halmashauri. Vile vile tumesaini Mkataba na wenzetu wa *World Bank,* bilioni 345 zimekwenda pia kuwekezwa katika suala zima la kuboresha mifumo ili kurahisisha suala la upimaji.

Mheshimiwa Spika, mambo haya yote lazima yaende kwa pamoja kwa sababu unapotaka kupanga lazima pia uweze kupima halafu umilikishe. Sasa na Serikali imewekeza pesa nyingi pale kuhakikisha kwamba mifumo yetu kwanza ya kuweka kumbukumbu inatatuliwa vizuri na inasomana. Sasa tunaelekea kwenye suala la Sensa ya Watu na Makazi, mifumo isiposomana ni wazi sisi tutakuwa kikwazo katika Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumesha-*harmonize* mifumo yote inasomeka na pesa tunazozipata tunaenda kuongeza zile *point* za upimaji ili kuweza kuwa na wigo mpana wa kupima ambao utarahisisha zaidi kuifikia nchi kwa wakati mfupi zaidi, kwa sababu mashine tunazozipa za kupimia ni zile zinazokwenda wigo mpana wa *radius* kama *square kilometer* 100 kwa wakati mmoja na hizo zinaweza kuwekwa katika kila mikoa, lakini bado mikoa yote inakwenda kuimarishwa. Kwa hiyo mfumo wa ukusanyaji mapato ambapo Kamati ya Bajeti pia imeongelea, utakwenda kuboresha tu pale ambapo tayari tutakuwa tumehama kutoka kwenye analogia na kuingia kwenye digitali. Kwa hiyo haya yote yakifanyika katika wakati ambao tumepangiwa wakati huu wa fedha tuna imani itakwenda kukamilika na tutakwenda kuondoa vikwazo vingi ambavyo vipo.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwetu sisi kama Wabunge, ambao ni Madiwani katika maeneo yetu, tuwe na ushiriki wa pamoja katika kuhakikisha halmashauri zetu zinatimiza matakwa ya kisheria katika kuweka mipango yake, ikiwa ni pamoja na ile ya mpango wa matumizi ya ardhi. Hapa naishukuru sana Serikali kwamba, imeiongezea Tume ya Matumizi ya Ardhi bilioni nne na kufanya ziwe bilioni 5.4, suala ambalo lilipigiwa kelele sana na Wabunge. Hilo tumeliona kama Serikali na tayari tumeongezewa pesa hiyo, kwa hiyo tutaenda kupanua wigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai yangu tena kwa halmashauri, bado narudi kulekule kwa sababu ufanisi wa Sekta ya Ardhi, inategemea na ufanisi katika halmashauri zetu kutekeleza matakwa ya kisheria ambayo yanatutaka kupanga, kupima na kumilikisha. Yanatatutaka kuweka mpango wa matumizi ya ardhi, Wizara ni wezeshi, Wizara inasimamia. Tutashirikiana vizuri na wenzetu wa TAMISEMI kuona hili takwa la kisheria linatimizwa. Niwaombe sana Wabunge, kwa sababu hii imekuwa ni kelele kila mara migogoro inakuwepo, lakini hatujaweza kukaa sawa katika halmashauri zetu ambazo ni Madiwani ili tusaidie Bajeti Kuu ya Serikali kuondokana na hii changamoto ambayo sasa tunatumia pesa nyingi kwenda kutatua migogoro ambayo tungekuwa tumejipanga katika suala zima tungekuwa tumemaliza. Niombe sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili tayari, Mheshimiwa.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimeweza kudodosa hayo machache, lakini niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Wachangiaji niwakumbushe wakati mkichangia mtazame huku mbele ili muweze kuona hii *mic*

nikishawasha, maana yake muda wako umekwisha umalizie sentensi.

Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo, atafuatiwa Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa na Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, ajiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja ya Bajeti Kuu ya Serikali. La pili, nitumie nafasi hii kushukuru Serikali, na kukishukuru Chama cha Mapinduzi na kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa niaba ya wakulima wa nchi yetu, kwa kuweka utashi wa kisiasa lakini na ku-*allocate* sehemu kubwa ya bajeti katika eneo la kilimo.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge Serikali imejipanga na Wizara imejipanga kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa zinatumika kuweza kufikia malengo yaliyokuwa yamewekwa. Hatua ambazo Serikali imechukua na niishukuru sana Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha kwa ujumla. Utaangalia kwenye Bajeti ya Wizara ya Fedha na Bajeti Kuu ya Serikali kuna mabadiliko ya kikodi mengi sana ambayo yamesoma na Waziri wa Fedha, pamoja na ku-*allocate* fedha lakini *tax measure* zilizowekwa na Wizara ya Fedha zimeonesha utayari wa kikodi wa kufanya mabadiliko katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni eneo ambalo tunaenda kwenye uzalishaji wa mafuta. Utaona kwamba kuna *tax measures* zimewekwa za kutoa *incentive* kwa wazalishaji na *processors* wa mafuta ya kula ya ndani ili hatua tunazochukua za kuzalisha mbegu za ruzuku na kuwapelekea wakulima, ziendane na mnunuzi anayechakata siku ya mwisho aweze kuchakata na awe *competitive* sokoni. Utaona kwamba kumetolewa *exemptions* kwenye eneo la

*VAT* za vifaa vinavyotumika kwenye uzalishaji wa alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile imetolewa *exemptions* za *VAT* kwenye *equipment* ambazo zinatumika kwa ajili ya kuchakata *single refinery* na *double refinery* ya mafuta ya kula. Hii ni hatua nzuri sana ambayo Serikali imechukua na Wizara ya Fedha na Kamati ya Bajeti. Kwa niaba ya wakulima na Watanzania ambao tuko kwenye Sekta ya Kilimo, tunawashukuru sana na nadhani Waheshimiwa Wabunge hiki kimekuwa kilio cha Bunge hili kwa muda mrefu kwamba hatua za kibajeti za kutenga fedha ziendane na hatua za kikodi kuweza kusaidia eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ambalo nataka niliseme kwa ufupi, Wabunge zaidi ya asilimia 80 wamechangia Sekta ya Kilimo, nataka niwahakikishie ushauri wa Wabunge na mawazo yao, sisi kama Serikali tunayachukua na tutaendelea kuyafanyia kazi katika kila hatua ambazo wamekuwa wakishauri.

Mheshimiwa Spika, nataka niende kwenye *specifics*, baadhi ya Wabunge wamechangia sana kwenye eneo la mbolea. La kwanza, Ndugu yangu Sanga, Mheshimiwa Aida na wengine wamechangia kwenye eneo la mbolea. Nataka niwaambie *reforms* tunazofanya kwenye *subsector* ya mbolea, hakuna mtu ataweza kutuzuia. Hili ni jambo ambalo nina uhakika nalo. Hakuna mtu ataweza kutuzuia kwa sababu *reforms* tunazozifanya ni kwa maslahi ya nchi yetu na ni maslahi ya wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme jambo moja, bei ya mbolea, mbolea ni bidhaa ambayo bei yake inakuwa *determined* na *forces* kwenye soko la dunia. Ni bidhaa inazalishwa *locally,* hata kama Tanzania leo tungezalisha *urea,* bado *pricing* yake ingeathirika na mwenendo wa hali

ya dunia, ukiacha hatua ambazo nchi zinachukua zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia nzima leo inatoa ruzuku ya mbolea, dunia nzima na nilisema wakati na-*wind up* bajeti yangu kama Waziri wa Kilimo. Nikasema kwamba nchi kama Malawi bajeti ya Sekta ya Kilimo ya Malawi asilimia 44, dola milioni 133 inatumika kama ruzuku ya mbolea. Nchi kama Rwanda asilimia 11.7, dola milioni 15 ya bajeti ya kilimo ya sekta ya Serikali ya Rwanda inatumika kama ruzuku ya mbolea. Nchi kama ya Zambia inatoa asilimia 30 ya ruzuku ya bei ya mbolea iliyoko sokoni. Tunapotaja bei za mbolea ni vizuri Waheshimiwa Wabunge tukaelewa na hii ni elimu ya msingi kabisa ya mtu yoyote aliyesoma *form five* na six. Mtu yoyote aliyesoma *form five* na *six* akajaaliwa kusoma somo la *Commerce* kuna elimu tunafundishwa *International Trade* na *International Pricing*. Tunapotaja bei ya mbolea tuna uwezo wa kutumia *ex-factory price*, tunatumia *FoB rate*, tunatumia *CIF rate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapokuja Bungeni hapa na hii nataka niiseme, *specifically* Mheshimiwa Mpina alisema kwamba nimetaja bei mbili tofauti. Ni hivi ninapotaja bei ambayo imetangazwa na *World Bank, IMF, IFC, African Development Bank,* hawa watu wanatumia *average rate* zilizoko kwenye *Global Commodity Exchange*, siyo bei ya Tanzania. Hili linakubalika duniani. Ninaposema *CIF rate* natumia *landed rate* ya Tanzania, ninaposema *FoB rate* natumia bei ya *origin*. Kwa hiyo hii ni jambo ndogo sana ambalo mtu unatakiwa kujifunza tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bei ya bidhaa yoyote...

**SPIKA:** Wewe ulikuwa umepewa dakika tano Mheshimiwa na kengele imegonga. Dakika moja malizia hoja yako.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, sawa. Nimalizie tu kusema kwamba, tatizo la upandaji wa bei ya mbolea dunia siyo tatizo la Tanzania na Serikali ya Awamu ya Sita imeamua kutoa ruzuku na sisi kama Wizara tumeshajiandaa, tunaanza mchakato wa utoaji wa ruzuku kwenye msimu ujao wa kilimo na tutavipa vipaumbele viwanda vya ndani. Tutavipa ruzuku na wakati huohuo mbolea kutoka nje tutaipa ruzuku. Kwa hiyo ni vizuri tusi-*mislead* umma.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako na Mheshimiwa Daktari Selemani Saidi Jafo, ajiandae.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye Bajeti ya Serikali iliyoko mbele yetu. Kabla sijaendelea naomba kwanza kabisa niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kutuletea Hotuba ya Bajeti ambayo ni nzuri na tunaamini itaweza kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili nchi yetu. Pia napenda niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia hasa kwenye maeneo ya barabara. Naomba niwahakikishe kwamba michango yao yote tumeichukua na sisi kama Wizara tunakwenda kuifanyia kazi vizuri kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye maeneo mawili, eneo la kwanza ni ujenzi wa reli ya kisasa ya *standard gauge* na eneo la pili ni eneo la barabara. Kama tunavyojua nchi yetu inaendelea na ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es

Salaam mpaka Mwanza yenye urefu wa kilomita 1,219 ambayo imegawika katika loti tano. Mradi huu kwa loti ya kwanza kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro ulianza mwaka 2016, mwaka huo tulianza kwa kutangaza tenda kwa ajili ya kupata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kipande hicho.

Mheshimiwa Spika, wakati huo makampuni 23 yalichukua *tender document* lakini mwisho wa safari kampuni moja tu ilirejesha *tender document* hizo ambayo ni Kampuni ya Yapi Merkezi. Wakati tunaendelea na mchakato huo, kulikuwa na maneno mengi sana kwa watu mbalimbali ambao walisema kwamba tuifute tenda hiyo kwa sababu haikuwa na mwitikio mzuri au *non responsive*. Baada ya kutafakari kwa kina sheria na maslahi mapana ya nchi yetu tuliamua tuendelee na mchakato, kuendelea na kumpa mkataba Mkandarasi Yapi Merkezi ambaye anafanyakazi hiyo kwa Dola za Kimarekani Bilioni 1.215 na mpaka sasa Mkandarasi huyo amefikia asilimia 96.5.

Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2016 tulitangaza tenda kwa kipande cha pili, cha tatu, cha nne na cha tano, lakini kwa bahati mbaya tena hakuna Mkandarasi yoyote aliyoomba. Tulitoa muda tena wa ziada lakini mpaka kufikia tarehe 31 Mei, 2017 kampuni moja tu ndiyo iliyoomba tenda kwa kipande cha *Lot* Nne; kampuni hiyo ilikuwa ni Kampuni ya Afrika Kusini *Transnet* ambayo iliungana na Kampuni ya *Mota-Engil* ya huko Ureno.

Mheshimiwa Spika, kampuni hiyo iliwasilisha gharama za Dola za Kimarekani Bilioni 1.498 kwa kipande chenye urefu wa kilometa 165, hii ina maana gharama za ujenzi kwa kila kilomita moja ilikuwa iwe dola milioni tisa. Bei hii ilikuwa kubwa sana ukilinganisha na *engineering estimation* ambayo tuliweka. Baada ya hapo tukaona mchakato wa kwenda kwa tenda ya wazi yaani *open tender* hauwezi kutusaidia wala hatuwezi kutupa faida yoyote ya msingi na tukaamua

kuanzia hapo tuenda kwa utaratibu wa *Single Source*. Utaratibu wa *single source* kikawaida unakubalika kisheria, lakini kuna vigezo muhimu ambavyo vinatakiwa kwanza tuangalie kwenye utaratibu wa *single source*.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha kwanza je, tunajiuliza Mkandarasi ana uwezo au ana uzoefu wa kufanyakazi inayotakiwa, kigezo cha pili je, Mkandarasi yupo kwenye *site* ya eneo la kazi, swali la tatu je, Mkandarasi anayo teknolojia inayotumika kwenye kazi husika.

Mheshimiwa Spika, kuna taratibu mahsusi ambazo tunazitumia kumpata Mkandarasi wa *single source*. Hatua ya kwanza kabisa Mkandarasi anapewa *tender document*s na yeye mwenyewe anatakiwa ajaze vigezo mbalimbali yaani *technical parameter* pamoja na bei. Hii hatuna maana kwamba tunampa kazi, mnampa *tender document*s yeye anajaza bei mwenyewe. Hatua ya pili inayofuata ni wataalam kufanya *evaluation, technical evaluation* na *financially evaluation*, hatua ya tatu inayofuata ni *negotiation* ni makubaliano au mapatano baina ya Mkandarasi na Mamlaka ya Shirika la Reli Tanzania na hatua ya nne ni utayarishaji wa mkataba na kuupeleka mkataba ufanyiwe uhakiki Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nitachukua mfano mdogo tu wa *Lot No*.4 jinsi gani tulifanya kupitia utaratibu huu. Kama nilivyosema *Lot No*. 4 tulitangaza lakini Mkandarasi alikuja na bei kubwa, bei ambayo ilikuwa ni Dola Bilioni 1.498 ambayo ni sawa na Dola Milioni Tisa kwa kila kilomita moja. Tukaamua kwenda kwenye *single source*, hatua ya mwanzo tulimpa Mkandarasi na Mkandarasi mwenyewe alikuwa ni Yapi Merkezi, tulimpa *tender document* na alijaza bei ya kuanzia Shilingi Trilioni 2.3 kwa kilometa 160.

Mheshimiwa Spika, hatua iliyofuata baada ya hapo wataalam wetu walikaa na wakaangalia *tender document*

zake kwanza tukaona je zimekidhi vigezo vya *technical evaluation* na *financially evaluation,* tukaona vimekidhi. Hatua ya tatu ilikuwa ni *negotiation* baina ya Mkandarasi ya *TRC* na hatua hii tulitumia karibuni miezi mitano kumpata huyu Mkandarasi. Baada ya *negotiation* bei ilishuka kutoka bei iliyowasilishwa na Mkandarasi ambayo ni Trilioni 2.33 mpaka kufikia Shilingi Trilion 1.93. Hapa utaona kuna punguzo la takriban Bilioni 406 sawa na asilimia 22.

Mheshimiwa Spika, ukilinganisha tena kama tungelikwenda kwenye *open tender* yaani tukatoa tenda ya wazi, punguzo tulilopata lilikuwa ni dola milioni 657.84 sawa na shilingi trilioni 1.513. yaani kama tungelikwenda *open tender* tungeliweza kupoteza shilingi trilioni 1.513. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu tumefanya *Lot No*. 2, *Lot No*. 3, kwa utaratibu huu tunakwenda kufanya *Lot No*. 6. *Lot No*. 6 hatujampa Mkandarasi tulilofanya tulimpa Mkandarasi *tender document* na kumpa *tender document*s siyo kwamba umempa kazi, kuna vitu viwili tofauti, watu wengi hawajui utaratibu unavyokwenda, watu wengi wanafikiria ukipewa *tender document* ndiyo umepewa kazi hapana. Hatua inayofuata sasa ni kuangalia je, Mkandarasi yule amekidhi vigezo, baada ya hapo kutakuwa na *negotiation* kubwa sana ambayo tunaamini sisi hiyo bei itashuka kwa takribani asilimia 30 mpaka 25. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana muda wako umeshakwisha Mheshimiwa.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Jafo, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kujenga uchumi wa nchi yetu na kuendelea kuimarisha sekta mbalimbali ikiwemo sekta za huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naompongeza Waziri wa Fedha na Mipango Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba pamoja na timu yake yote, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kutuletea bajeti nzuri ambayo inakwenda kubana matumizi, kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha ili kuhakikisha kwamba fedha za walipa kodi zinatumika katika kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo naomba nielekeze mchango wangu kuhusiana na Kanuni ya Mafao ambayo itaanza kutumika kuanzia Tarehe Mosi Julai, 2022. Utakumbuka kwamba mnano mwaka 2018, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Sheria hiyo iliunganisha mifuko ya *GEPF, LAPF, PPF* na *PSPF* na kuja na Mfuko mmoja wa Mafao kwa Watumishi wa Umma. Kabla ya kuunganisha mifuko hiyo, kulikuwa na Kanuni tofauti za mafao ambazo zinatumika kwa mifuko mbalimbali. Mfuko wa *GEPF, PPF*, *NSSF* na Wafanyakazi wote ambao wameajiriwa baada ya Julai, 2014 walikuwa wanatumia Kanuni ya Mafao ambayo ilikuwa inawapa mafao ya mkupuo kwa asilimia 25 na wastani wa umri wa kuishi ilikuwa ni miaka 12.5, lakini wanachama waliokuwa wa Mfuko wa *PSPF* na wanachama wa *LAPF* walikuwa wanalipwa mafao kwa mkupuo wa asilimia 50 na wastani wa umri wa kuishi wa miaka 15.5.

Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha Sheria ya Mafao mwaka 2018 zilitengenezwa Kanuni za kuwezesha utekelezaji wa sheria hiyo. Sheria hiyo pia ililenga katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwiano wa mafao kwa watumishi wote, kama nilivyoeleza kwamba baadhi ya watumishi mpaka leo wanalipwa mkupuo wa asilimia 25 na wengine wanalipwa mkupuo wa asilimia 50. Kanuni za Mafao za mwaka 2018 ziliwekwa mafao ya mkupuo ya asilimia 25 kwa watumishi wote, sekta ya umma, sekta binafsi na bila kujali ametoka katika mfuko gani. Kwa hiyo, baada ya Kanuni hizo kuanza kutumika, watumishi waliokuwa wa *PSPF* na *LAPF* kwa sababu wao walikuwa wanashuka kutoka asilimia 50 mpaka 25 kulikuwa na kutokukubali ile Kanuni iliyokuwa imetungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ni sikivu, kutokana na malalamiko ya watumishi Serikali ilisitisha matumizi ya kikokotoo na Serikali ikaagiza iundwe Kamati ambayo inashirikisha wadau, wafanyakazi, waajiri na Serikali ili kuchambua uwezo wa mifuko, kuchambua hali ya uendelevu na uhimilivu wa mifuko na kuja na kanuni ambayo itakubalika. Kazi hiyo imeanza kufanyika tangu mwaka 2019 na kwa kweli haikuwa kazi nyepesi. Lakini nafurahi kukufahamisha kwamba, makubaliano yamefikiwa na kwamba kuanzia Tarehe Mosi Julai, 2022 Kanuni ya Mafao kwa watumishi wote itakuwa inatoa mafao ya mkupuo wa asilimia 33. Kwa hiyo, wale waliokuwa wanapata asilimia 25 ambao ni watumishi wote wanaofanya katika Mashirika ya Umma, wale watumishi wote katika Sekta Binafsi, Serikali kuanzia Julai Mosi, 2022 imewapandishia mafao yao ya mkupuo kutoka asilimia 25 mpaka asilimia 33. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze athari zilizokuwa zinajitokeza kutokana na Kanuni ya Mafao ya mkupuo ya asilimia 50. Nitatoa mfano halisi kwamba kuna mfano wa mchangiaji katika mafao ambaye amechangia katika mfuko kwa miezi 467 na michango yake kwa muda wote wa

utumishi ni Milioni 36. Kanuni ya zamani ilikuwa inampa mafao ya mkupuo ya milioni 129, yaani yeye amechangia Milioni 36, naomba Wabunge tusikilizane vizuri katika eneo hili. Amechangia milioni 36 katika kipindi chote cha utumishi lakini anapata mafao ya mkupuo ya milioni 129, lakini wafanyakazi walioko *NSSF* na wafanyakazi katika Mashirika ya Umma, mfanyakazi ambaye amechangia michango ambayo ina thamani ya milioni 86, amefanyakazi miezi 350 kwa kutumia mkupuo wa asilimia 25 yeye anapata mafano ya mkupuo ya shilingi milioni 54. Huyu amechangia milioni 36 analipwa milioni 129, huyu amechangia milioni 86 analipwa milioni 54. Kwa hiyo, Kanuni hii inakwenda kuweka usawa kwa mafao miongoni mwa wafanyakazi, wale waliokuwa wanalipwa kidogo na wenyewe wapande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia kanuni hii mpya, watumishi wa umma kama mfano wa huyu ambaye alikuwa amechangia Milioni 86 lakini anapata Milioni 54 atakwenda kupata Milioni 71 kwa kutumia kanuni mpya.

Mheshimiwa Spika, wanapopata mafao ya mkupuo wanaendelea kulipwa pensheni, kwa hiyo, huyu akilipwa milioni 71 kutokana na Kanuni hii itakayoanza kutumika mwezi Julai ataendelea kulipwa shilingi 1,084,000 mpaka Mwenyezi Mungu atakapomuita. Kwa hiyo, ile inakuwa ni ya mkupuo lakini anaendelea kulipwa pensheni kila mwezi. Kwa hiyo, utaona kwamba ile *formula* ambayo ilikuwa inampa mkupuo wa asilimia 50 ilikuwa haina uhalisia, unachangia milioni 36 unalipwa kwa mkupuo milioni 129. Hii imesababisha kwamba mifuko imekuwa hali yake ya uhimilivu na ukwasi imekuwa ikiendelea kupungua mwaka hadi mwaka hii inajidhihirisha hata katika ripoti ya CAG. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ripoti ya CAG ya Machi, 2022 nikiangalia ukurasa wa 144, CAG anatuambia kwamba gharama za mafao zinazidi mapato ya michango hivyo kuhatarisha uwezo wa mifuko kulipa mafao. CAG ametuamia

kwamba katika miaka mitatu ameona kwamba kila mwaka makusanyo kwa wanachama yanakuwa ni madogo ukilinganisha na mafao yanayolipwa na ametoa mfano CAG katika ukurasa 144, anasema katika mwaka wa fedha 2020/2021 tofauti kati ya michango na mafao ilikuwa ni Bilioni 767, yaani nakisi ya michango unayokusanya na kile unacholipa unakuwa na nakisi ya bilioni 767.

Mheshimiwa Spika, hili ni shimo ambalo tunalichimba na kwa kutumia Kanuni hii ndiyo tunakwenda kurekebisha na kama nilivyosema inakwenda kuongeza mafao kwa wafanyakazi 1,350,000 na inakwenda kuongeza mafao.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tamisemi, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumshukuru sana Mwenyezi Mungu lakini nikushukuru wewe kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 2 Novemba, 2021 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan tulipokuwa Glasgow - Scotland aliutangazia ulimwengu, kwamba Tanzania tunakwenda

kujipanga kuwafikisha kwenye zile *NDC - National Determiners Contribution* kupunguza suala zima la hewa ya ukaa au gesi joto duniani kwa asilimia 30 mpaka 35. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Waziri wa Fedha, umemtendea haki Mheshimiwa Rais kwa kuja na mambo mahsusi Sita ya kimazingira. Jambo la kwanza, Mheshimiwa Rais alisema Tanzania tunakwenda kuiunganisha Bandari ya Dar es Salaam na *Landlocked Country* ya Rwanda and Burundi kwa *Standard Gauge* ambayo itapunguza gesi ya ukaa duniani. Amesema tutatumia Dola za Kimarekani zaidi ya Bilioni 7.5, leo hii namshukuru Profesa Mbarawa amesema hapa, katika bajeti yake ya kutimiza hii *mission* zaidi ya Shilingi Trilioni 1.5, dunia inashuhudia alichosema Mheshimiwa Rais bajeti yake mwaka huu inazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa pili Bwawa la Nyerere, alisema tunaenda kuzalisha umeme wa maji ambao utapunguza hii *emission* na utachangia *four times* katika *energy mix* nchini mwetu, ambayo mwaka huu tunaona bajeti yam waka huu zaidi ya Shilingi Trilioni 1.44 imeitendea haki dunia inasema: "Rais wa Tanzania alichokisema ndiyo kinachotekelezwa katika bajeti ya Tanzania". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, tumeshuhudia kwamba Rais alisema Jiji la Dar es Salaam kuna mradi wa mabasi yaendayo kasi ambayo inapunguza hiyo *emission*, leo hii tunashuhudia mradi mkubwa bajeti ya mwaka huu imetengwa bajeti kupunguza *emission*, mradi unaendelea vizuri katika ile awamu ya pili ya kutoka katikati ya Mji mpaka Mbagala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la nne, ni eneo la mradi wa kilimo. Tumeshuhudia bajeti ya kilimo imepanda na dunia inashuhudia kwamba, bajeti ya Tanzania alichosema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda kuhakikisha anafanya *smart agriculture* ni kweli bajeti imeongezeka mara

tatu. Pia alisema suala la uhifadhi, Tanzania zaidi ya asilimia 32 ardhi yake imehifadhiwa, na kampeni ya upandaji miti zaidi ya milioni 276 kwa mwaka kwa kila halmashauri kupata miti milioni 1.5, leo hii dunia inashuhudia. Bajeti aliyowakilisha Mheshimiwa Mwigulu hapa inashuhudia wazi kwamba alichosema Rais Mama Samia Suluhu Hassan, ambayo ilikuwa ni miongoni mwa *best speech* mwaka huu kweli kimefanyika katika bajeti ya Tanzania. Haya yote ni mambo makubwa sana ambayo tunayo kila sababu ya kujivunia nchi yetu na bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja imesema hoja *carbon credit* hapa, jambo hili ni kweli tulikuwa hatuaanza vizuri lakini bahati nzuri sasa hivi tumekwenda katika kutengeneza miongozo, lengo kubwa ni kwamba miongozo hii itakuja na kanuni. Leo hii tuna halmashauri chache zinapata suala zima la fedha ya hewa ya ukaa na ndiyo maana kama Serikali tumeamua kulichukua hili kuliweka katika mipango mizuri zaidi, Halmashauri ya Tanganyika na Halmashauri chache tu.

Mheshimiwa Spika, katika hili unaona zaidi ya tani Milioni 1.4 mpaka mwaka 2022 zitakuwa zimehesabika kama hii ni hewa ya ukaa. Kwa hiyo, imani yetu kubwa sana, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na wadau wote wakiwemo wadau wa Bunge tutaangalia jinsi gani tutafanya, mwongozo huu ukitoka itakwenda sambamba na suala utekelezaji wa kanuni, lengo kubwa ni kwamba mchango wa bajeti wa uchangiwe vilevile na suala zima la hewa ya ukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lilikuwa ni suala zima la mahusiano ya Taasisi za Muungano za Bara na Visiwani. Naomba nikuhakikishie, mpaka mwaka 2021/2022 Taasisi zetu za Muungano chini ya Serikali ya Awamu ya Sita na Serikali ya Awamu ya Nane ya Dkt. Hussein Mwinyi tulishafanya vikao 19.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache sana na muda wangu naona umekwisha, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Joakim, Simbachawene ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Mimi pia niungane na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Waheshimiwa Mawaziri kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Naibu Waziri Hamad Chande pamoja na timu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuleta bajeti kuu ya Serikali ambayo tunaipongeza; lakini pia tumeona imepokelewa vyema na Watanzania. Hongereni sana Mheshimiwa Waziri na timu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na mimi niseme naunga mkono hoja. Nishukuru Bunge lako Tukufu katika bajeti ambayo tunapitisha baadaye, naamini itapita kwa asilimia 100 kwa sababu imesheheni mambo mazuri; nikushukuru wewe pamoja na Bunge lako Tukufu Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwenye bajeti hii mlitupitisha shilingi trilioni 8.7 tuwashukuru sana. Katika shilingi trilioni 8.7 hizi, mambo ni mengi kabambe ambayo pamoja na Bunge lako Tukufu mlitupitishia; lakini *ni-highlight* tu machache. Mtakapopitisha Bajeti Kuu ya Serikali inamaana ukiangalia watumishi Ofisi ya Rais TAMISEMI tuna watumishi takriban asilimia 70 ya watumishi wote wa umma. Hata zile asilimia 23.3 ambazo Mheshimiwa Rais alipandisha mishahara kwa watumishi wa umma Ofisi ya Rais, TAMISEMI watumishi wetu ni wanufaika wakubwa Kwa sababu asilimia karibia 70 ya watumishi wote wako chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea kumshukuru sana Rais wetu kwa kuwajali watumishi. Vilevile miji 45 mradi wa *TACTIC* zile fedha trilioni ziko humu kwenye Bajeti Kuu ya Serikali. Kwa hiyo, baada ya kupitisha bajeti kuu hii Waheshimiwa Wabunge kutoka kwenye hii miji 45 tunakwenda kuchapa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti hii zipo trilioni za fedha kwa ajili ya kumalizia miradi ya sekta ya elimu, afya, maboma yale ambayo yalikuwa hayajakamilika, Waheshimiwa Wabunge mmetupitishia twende tukapige kazi kukamilisha maboma sekta ya elimu na sekta ya afya. Kwenye bajeti hii pia Mheshimiwa Rais kwenye maelekezo yake na bajeti ambayo Ofisi ya Rais TAMISEMI mlitupitishia ya shilingi trilioni 8.7 pia, kwa kutambua kazi nzuri ya Waheshimiwa Wabunge ambayo mnaifanya Mfuko wa Jimbo tuliongeza kutoka bilioni 11 kwenda bilioni 16. Kwa hiyo, tutakapopitisha Bajeti Kuu ya Serikali pia tunakwenda kuchagiza maendeleo kupitia huu Mfuko wa Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nimalizie kwa kutambua kazi nzuri ambayo Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya katika kusimamia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pia Bajeti hii Kuu ya Serikali, tumeongeza *OC* kwenye Tawala za Mikoa na Ofisi za Wakuu wa Wilaya ili wakasimamie vyema fedha nyingi ambazo Mheshimiwa Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan anatuwezesha katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, na nitumie nafasi hii, katika mchango wa mtani wangu Mheshimiwa Waitara amechangia vizuri na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumemsikia. Changamoto ambazo ziko Mkoa wa Mara tunazifanyia kazi. Ningependa kuwatoa wasiwasi wananchi wa Mkoa wa Mara Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan ni Sikivu. Changamoto zilizoko Tarime Vijijini, changamoto

zilizoko Rorya na maeneo mengine ya nchi yanayofanana na changamoto hizo tunakwenda kuzipatia dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuwaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge; tunaendelea kuimarisha nidhamu katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Chama chetu cha Mapinduzi kwenye *Party Caucus* walitoa maelekezo kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI lazima tuwape ushirikiano Wabunge kwa sababu ndio watetezi wa bajeti ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Baada ya hapo nilitoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi kuhakikisha wanawapa ushirikiano asilimia 100 Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaheshimu na kuthamini sana Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.  Baada ya maelekezo ambayo Chama cha Mapinduzi kilitupatia Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri Mkuu akatoa maagizo nilishatoa maagizo haya na ndiyo maana hata Profesa Shemdoe Katibu Mkuu Ofis ya Rais, TAMISEMI tumeanza utaratibu wa kuwajulisha Wabunge miradi kabla haijaenda kwenye halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama mimi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ninawasikiliza Wabunge na kutii maagizo ya Chama na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni Mkuu wa Mkoa gani, Mkuu wa Wilaya gani ambaye hatasikiliza maelekezo ya Serikali na Chama? Kwa hiyo ningependa kuwatoa wasiwasi na Bunge lako Tukufu; mchango wa mtani wangu Mheshimiwa Waitara ni mzuri, lakini nilitaka nitoe *clarification* maana yeye *ame-generalize* kwamba Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya kana kwamba wote wanazo changamoto kama zilizoko Mkoa wa Mara. Wakuu wa Mikoa wanafanya kazi nzuri sehemu nyingi, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi. tuendelee kuwapa ushirikiano. Hata hivyo, maeneo ambayo ni mahususi yana changamoto kama kule Tarime na Rorya tutayapatia dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sera ya elimu bila malipo; tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan sera hii katika Serikali anayoiongoza ya Awamu ya Sita tumeiendeleza; na utekelezaji wa sera hii umepelekea watoto ambao walikuwa hawawezi kwenda shuleni kwa sababu ya gharama kuweza kwenda shule. Hii imepelekea kuongezeka uhitaji wa walimu kwenye shule zetu na kuongezeka kwa uhitaji wa miundombinu katika shule zetu. Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan kwenye upande wa walimu, tumekwisha ajiri walimu 26,598 na kwenye bajeti hii Waheshimiwa Wabunge mtakapotupitishia tunakwenda kuajiri walimu 9,800 ili kuendelea kupunguza uhitaji wa walimu katika shule zzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, kwenye upande wa miundombinu ambayo imeongezeka uhitaji wa madarasa kwa sababu ya elimu bila malipo, tayari bilioni 304; mataifa mengine tulikuwa tunaona wanachukua fedha za *IMF* wanakwenda kununua vitakasa mikono, wananunua barakoa lakini kwa dira nzuri ya Mheshimiwa Rais wetu fedha hizi tumezitumia kwenye kujenga miundombinu ambayo kizazi cha sasa na vizazi vijavyo vitatumia. Kwa hiyo, tayari tumeshabainisha uhitaji wa madarasa… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, niliomba dakika za shemeji yangu Dkt. Ashatu ziwe 10.

**SPIKA:** Ndio zimeshafika 10 hiyo ni ya pili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, zimeshafika 10?

**SPIKA:** Dakika moja malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa suala la asilimia 10 za vikundi. Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Waziri wa Fedha na Mipango atalihitimisha vizuri lakini mimi ningependa kuwaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge. Kwenye suala la asilimia 10 pamoja na hitimisho ambalo Mheshimiwa Waziri atalitoa sisi tunakwenda kuimarisha usimamizi kwa kutumia TEHAMA kwenye fedha hizi za asilimia 10. Pia tunakwenda kusimamia sheria, kwamba Wakurugenzi katika kutoa asilimia 10 si hiyari bali ni takwa la kisheria. Sambamba na hilo nimeshaweka vigezo vya kuwapima Wakurugenzi; moja ya kigezo ni kuangalia wanasimamiaje asilimia 10, kuzitoa kwa wakati kwenye asilimia 40 au asilimia 60, kusimamia marejesho yake na kuzingatia utawala bora katika usimamizi wa asilimia 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda ninaunga mkono hoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha atatoa ufafanuzi zaidi kwenye hii asilimia 10. ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora atafuatiwa na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nimshukuru pia Mwenyezi Mungu. Pia na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri wenzangu walionitangulia kumpongeza sana Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa bajeti hii. Bajeti hii ya kwanza ya Mheshimiwa Rais imeweza kubeba maono na muelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwahudumia Watanzania. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono hayo, na kwa kweli bajeti hii imejieleza wazi ni namna gani inajenga imani kwa Watanzania, hasa baada ya kuona Watanzania wengi wanamuamini na wanamuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kwenye hoja ambazo zilijitokeza wakati wa mijadala. Nianze na hoja ya utoshelevu wa watumishi wa umma na mifumo ya ajira nchini. Waheshimiwa Wabunge wametushauri lakini na Serikali imeendelea kufanya tathmini ya maeneo hayo makubwa mawili niliyoyasema. Jambo la kwanza Waheshimiwa Wabunge wameomba kwa haraka iwezekanavyo miundombinu iliyojengwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wangependa kuona watumishi wanapelekwa haraka na miundombinu hiyo inaanza kufanya kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda naiagiza Sekretarieti ya Ajira na Mamlaka zote zilizokasimiwa utaratibu na mchakato wa ajira kwa vijana wa Tanzania kuhakikisha haraka iwezekanavyo wanatangaza vijana wote waliofaulu usaili ambao wanastahili kwenda kuhudumia kwenye miundombinu iliyojengwa; na mwezi wa Julai ajira hizo mpya zote zianze kufanya kazi na vijana wote wawepo katika maeneo yao waliyopangiwa ili kazi ya Serikali hii iweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshiimiwa Spika, eneo la pili Waheshimiwa Wabunge na sisi Serikali, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais,

tumepokea kilio cha vijana wengi na kilio cha Waheshimiwa Wabunge katika mfumo mzima wa mchakato wa ajira. Tumekuwa tukishuhudia makundi ya vijana yanasafiri kutoka katika mikoa mbalimbali kila mara, wanakusanyika hapa Dodoma kwa ajili ya kufanya usaili. Ninaomba kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge tumesikia kilio hicho. Tumeshafanya maamuzi na mara baada ya bajeti hii kupita naiagiza Sekretarieti ya Ajira kutekeleza maagizo ya Serikali na Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha mfumo wa usaili sasa unakwenda katika mikoa yote nchini; na tunapoupeleka mfumo huu wa usaili katika mikoa nchini hatua ya awali ya usaili inayojumuisha watoto wengi wa wakulima watoto wengi ambao hawana uwezo wa kusafiri kila siku ifanyike huko mikoani. Hatua zinazofuata zinaweza kuendelea kwenye ngazi ya Kanda na zinaweza kuhitimishwa kwenye ngazi ya Taifa. Hiyo itawasaidia sana vijana hawa kutokuhangaika kila siku kusafiri kwenda kwenye usaili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge mmetushauri sana, Mheshimiwa Rais ameamua kutuagiza tulisimamie kwa nguvu zetu zote, ni kuangalia ni namna gani watoto wa Kitanzania wanapata fursa ya kufanya usaili katika Sekretarieti ya Ajira na mamlaka nyingine zilizokasimiwa madaraka. Kwa kuwa nafasi ni chache, wanaofaulu wanakuwa ni wengi, kuna kila haja ya kuwa na *database* ili kuondoa usumbufu mkubwa. Naiagiza Sekretarieti ya Ajira na mamlaka zote tulizozikasimia utaratibu wa usaili wa ajira Sekretarieti ya Ajira ibadilishe kanuni ya usimamizi wa *database* ndani ya mwezi mmoja. *Database* itoke katika kuhifadhi taarifa miezi sita mpaka mwaka mmoja ili kutusaidia kuangalia watoto waliofanya i*nterview* katika kada zinazofanana wasijirudie rudie kuhangaika kuendelea kufanya *interview*. *Database* itumike kuweza kuajiri watoto wa Tanzania. Kwa hiyo, ninaiomba Sekretarieti ya Ajira maagizo haya ya Serikali yasimamiwe ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia mfumo wa tathmini ya hali ya watumishi Waheshimiwa Wabunge mmetuambia, kuna tatizo kubwa la mgawanyo na uwiano sawa wa watumishi katika maeneo mbalimbali nchini. Tumefanya utafiti, lakini si utafiti tu tumetengeneza mfumo wa tathmini ya hali ya utumishi, tumegundua liko tatizo la uwiano wa watumishi kutoka eneo moja kwenda lingine. Kwa mfano mdogo tu, baada ya kutengeneza na kujenga huo mfumo na taarifa kuanza kuingizwa na waajiri kwenye mfumo tumegundua, nitatoa mfano, lakini sitataja ni shule gani na ni eneo gani. Kuna shule moja katika manispaa moja walimu 21 wanafundisha somo moja la Kiswahili kwenye shule hiyo. Kupitia mfumo huu wa tathmini wa hali ya utumishi nchini tumegundua pia katika shule hiyo hiyo, walimu wengine 21 wanafundisha somo moja la Historia kwenye shule hiyo hiyo. Tumegundua kuwa walimu 16 wanafundisha somo moja la Jiografia katika shule hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kupitia mfumo huu ambao Mheshimiwa Rais aliagiza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iangalie hali ya usawa wa mgao wa watumishi, tumegundua kwa mfano, shule hizi nitazitaja, na ninazitaja kwa maana yangu halisi ninataka kuagiza kwamba ajira mpya zitakazotokea Mamlaka zote zitupie macho katika shule hizi nitakazozisema na nyingine zinazofanana na hizi. Shule ya Msingi Kitula iliyoko Wilaya ya Muleba *(DC)* Mwalimu Dickson anafundisha masomo saba yeye peke yake, na Mwalimu Fadhila anafundisha masomo saba peke yake. Tumeangalia Shule ya Msingi Ihema ambayo iko Wilaya ya Mbarali Mwalimu Azalia anafundisha masomo 10 pekeyake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuziagiza mamlaka zote za ajira zitakazopanga watumishi hawa wapya kuzingatia mgao sawa wa watumishi katika maeneo mbalimbali nchini. Ni lazima mamlaka hizo zizingatie usawa huu. Haitakuwa vyema kama watumishi hawatagawiwa kwa usawa ilhali kila sehemu ya Tanzania inahitaji jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize na suala la nidhamu. Imeongelewa sana, naungana mkono na Waziri wa Fedha kwamba tunatakiwa kuangalia nidhamu ya watumishi nchini. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawapenda sana watumishi wa umma katika nchi nzima ya Tanzania; na ndiyo maana amefanya yale aliyoyafanya, *arrears*, madaraja, kima cha chini cha mshahara hiyo yote anataka kuonesha anasimamia haki kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, haki ni pamoja na haki ya mtumishi kuadhibiwa anapofanya makosa hatutaweza kuangalia fedha hizi zote zinazotolewa na Serikali zinapokwenda kwenye halmashauri, hawa watumishi waliokasimiwa madaraka ya kusimamia rasilimali fedha hawasimamii rasilimali fedha vizuri ambayo inatakiwa iende kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kanuni ya 42 kwenye kanuni za mwaka 2003 zinazosimamia utumishi wa umma imesema na kueleza wazi, aina za adhabu zinazotakiwa kupelekwa kwa watumishi wa umma wanapokiuka maadili ya utumishi wa umma. Ninaomba kuziagiza Mamlaka zote za Ajira nchini itakapofika tarehe 30 mwezi Julai waniletee taarifa za mashauri ya nidhamu ambayo yanaendelea katika mamlaka zote za ajira, ili tuweze kuona kama kweli hao tuliwakasimia shughuli za kusimamia rasilimali watu wanachukua hatua za nidhamu kwa watumishi wachache ambao wanaharibu sifa ya watumishi wengi wanaolitumikia Taifa hili na kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba niliambie Bunge lako Tukufu, baada ya kuingia kwenye hii ofisi nimegundua, katika eneo linapoteza fedha nyingi za Serikali ni mchakato wa mashauri ya nidhamu. Mtumishi anakuwa na shauri la nidhamu lisiloisha kwa miaka mitano na anaendelea kupokea mshahara. Lakini unajiuliza, Kamati za Nidhamu zinafanya nini

katika eneo hilo ili kuhakikisha kwamba mashauri haya yanaisha kwa haraka?

Mheshimiwa Spika, eneo hilo linamfanya mtumishi, na wakati mwingine watumishi wengi wamekuwa wakionewa tu katika mashitaka hayo. Wakati mwingine waliopewa nafasi ya kusimamia mashauri ya nidhamu wanafanya maksudi, wale watumishi ambao wamekiuka maadili wanafunguliwa mashitaka ya nidhamu bila utaratibu kusudi mashitaka hayo yasiishe na wasikutwe na hatia.

Mheshimiwa Spika, hatutakubali, tutasimamea eneo hilo. Msingi wa eneo hilo tunataka kwenye kila mwaji ri Kamati za Nidhamu zizingatie sheria na utaratibu na zitoe haki kwa watumishi. Mtumishi anatakiwa kupata haki katika mashauri ya nidhamu na kupata haki katika maeneo mengine yoyote yanayotakiwa. Tumekubaliana kuunda mifumo ya usimamizi wa rasilimaliwatu nchini. Tutasimamia watumishi, tutasimamia taasisi zote za umma, ndani yam waka mmoja tutakuwa tunaipima taasisi moja baada ya nyingine kama imetekeleza vyema wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, mtumishi anakuwa na shauri la nidhamu lisiloisha kwa miaka mitano na anaendelea kupokea mshahara. Unajiuliza, Kamati za Nidhamu zinafanya nini katika eneo hilo ili kuhakikisha kwamba mashauri yao yanaisha kwa haraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hilo linamfanya mtumishi na wakati mwingine watumishi wengi wamekuwa wakionewa tu katika mashitaka hayo ya nidhamu. Wakati mwingine waliopewa nafasi ya kusimamia mashauri ya nidhamu, wanafanya makusudi. Wale watumishi ambao wanakiuka maadili wanafunguliwa mashitaka ya nidhamu bila utaratibu kusudi mashitaka hayo yasiishe na wasikamatike wana hatia. Hatutakubali, tutasimamia eneo hilo. Msingi wa eneo hilo tunataka kila mwajiri, Kamati za Nidhamu zizingatie sheria na

utaratibu na zitoe haki kwa watumishi. Mtumishi anatakiwa kupata haki katika mashauri ya Nidhamu na kupata haki katika maeneo mengine yoyote yanayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tumekubaliana kuunda mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu nchini. Tutasimamia watumishi, tutasimamia taasisi zote za umma. Ndani ya mwaka mmoja tutakuwa tunaipima taasisi moja baada ya nyingine kama imetekeleza vYema wajibu wake. Tumetoa waraka kuhakikisha waajiri wote watakuwa wanawasilisha vielelezo kwenye Tume ya Utumishi wa Umma ili kusaidia kusimamia nidhamu ya watumishi na ili watumishi wanaofanya vizuri waweze kuwa *rewarded* kwa kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja, naendelea kuipongeza Serikali na Wizara kwa ujumla. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora umetoa hapo maelekezo na maagizo mengi, ila naomba ulirudie lile agizo la watumishi, hasa walimu kupelekwa kwenye maeneo ziliko shule kwa usawa. Hebu lirudie kidogo hili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nirudie agizo hili kama lifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumetengeneza mfumo wa tathmini ya hali ya utumishi nchini. Mfumo huo umetusaidia kugundua mgawanyo sawa na uwiano sawa wa ajira na kuwapeleka watumishi katika maeneo mbalimbali nchini ili wakatoe huduma kwa Watanzania wote. Tunahangaika kwamba idadi ya watumishi haiendani na mahitaji ya nchi, lakini kama tukiwagawa vizuri watumishi tulionao, wakapata fursa ya

kutekeleza majukumu yao katika maeneo mbalimbali nchini, tatizo la upungufu wa ajira tutakuwa tumelipunguza kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kutoa agizo kwa heshima ya Kiti chako, mamlaka zote zilizokasimiwa kutengeneza taratibu za ajira nchini, zihakikishe zitakapoanza kupeleka watumishi wa ajira mpya katika kutoa huduma kwenye maeneo mbalimbali, na hasa kwenye sekta ya afya na sekta ya elimu, wahakikishe maeneo ambayo hayana watumishi yapate kipaumbele cha kugawiwa watumishi katika mgawo huu ambao tunaenda kuutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani ya Mheshimiwa Rais kwamba Watanzania wote wafikiwe na huduma zinazofanana bila kupendelea, bila kujali maeneo ambayo Watanzania hao wanaishi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa agizo hilo, Waheshimiwa Wabunge ni muhimu kipindi hiki ambacho tutarejea Bunge lile lingine kwa sababu, ajira hizi zinaanza mwezi wa Saba, yale maeneo yetu ni muhimu sana kufuatilia shule zipi zimepata nani na nani ili Serikali ipate taarifa. Hiyo ndiyo kazi yetu Waheshimiwa Wabunge kama wawakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Mchemba Madelu, ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu

pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Hamad, nawapongeza sana. Pia nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Sillo, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa kwa pamoja ambayo wamefanya katika kipindi hiki cha bajeti kwa Bunge letu hili toka tulipoanza na sasa tuko ukingoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shabaha ya Sera za CCM kwa mwaka 2020/2025 ni kujenga uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani na unaojengwa katika msingi wa viwanda, huduma za kiuchumi na miundombinu wezeshi. Shabaha nyingine ya pili ni kuingia kwenye uchumi wa kidijitali kwa kuimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu *(digital economy)*. Ni katika muktadha huu wa utekelezaji wa shabaha hii ndiyo maana Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema, hataki kodi zinazowaweka Watanzania katika mazingira magumu, hataki kodi ya dhuluma, hataki kodi inayowafanya watu waishi maisha ya hofu, anataka kodi halali na ya haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona matokeo kwamba wakati huu wa uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, makusanyo ya kodi yameongezeka kwa wastani wa Shilingi trilioni 1.8 hadi tisa kwa mwezi. Hii inaonesha kwamba uchumi jumuishi na shirikishi kama sera na shabaha za Sera za CCM zinavyosema, ukitekelezwa, hauna matatizo. Kweli, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa msimamo huu, nasi ambao tumewekwa kwa ajili ya kumsaidia tutahakikisha kwamba tunafanya kila linalowezekana kutimiza malengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kujenga uchumi huu tulionao sasa ambapo tuko katika uchumi wa kipato cha kati, yako malengo ambayo ni lazima twendenayo kulingana na hali ya uchumi wa sasa ili tusishuke kwenda uchumi wa chini. Sasa hivi tuko katika uchumi wa kati, ndiyo maana Serikali

inatekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema, iko miradi ambayo inaendelea na hakuna mradi hata mmoja ambao hautekelezwi. Yote inatekelezwa, na Kamati zako za Bunge zinaitembelea miradi hii na zinaona maendeleo yake, na zinatoa matokeo yake. Tunawashukuru sana Kamati zote kwa kushirikiana na Serikali kwa kupita na kuangalia miradi yote ile ya kimkakati inavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema, kwa mfano, utekelezaji wa Mradi wa *Standard Gauge* unaendelea vizuri na kwa sasa kutoka Dar es Salaam mpaka Makutupora umefikia wastani wa asilimia 92, lakini yupo Mtanzania mwingine amekaa amejifungia chumbani kwake, ana simu yake, anasema hamna kinachoendelea. Nami nafikiri ndugu zangu hii *republic* ya *social media* tuisikilize kwa makini, tuifuate kwa makini, lakini imefikia hatua hata Bunge lako likifanya maamuzi ya mambo hapa, hata Bunge lako likitoa taarifa ya manbo hapa ni kama vile haliaminiki, yaani uzushi wa kwenye mitandao ndiyo unaoonekana wa maana zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwasihi Watanzania kwamba tukifanya hivi tutakuwa hatuitendei haki Serikali, hatuitendei haki nchi yetu, na hatujitendei haki wenyewe. Kwa sababu tunapiga hatua kubwa sana ya maendeleo. Tukijifanyia tathmini katika miaka hii michache, na umesikia hapa, kila Mbunge anayesimama anasema kwake kuna vitu vinafanyika; kuna vituo vya afya, kuna maeneo ya shule zinajengwa, mambo yanayofanyika ni makubwa. Sasa hivi tunaanza kugombania barabara za lami kwenye majimbo yetu. Tumeshamaliza kuunganisha mikoa, bado maeneo kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yanayofanyika katika nchi yetu ni makubwa, lakini bado *we don't appreciate ourself* kile tunachokifanya. Ulinganifu tunaoufanya ni wa kufikirika.

Nawaomba Watanzania tujaribu kufuatilia mambo yanayotuhusu. Kwa sasa hivi niseme tu, miradi mbalimbali ya kimkakati, Mradi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa megawati 2,115 unaendelea, uliachwa na Awamu ya Tano ukiwa katika asilimia chini ya 30, lakini sasa hivi uko asilimia 60.22 na Kamati yako imesema. Pia Shirika la Ndege, juzi tulipokea ndege tatu na uongozi wa Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan umeagiza ndege nyingine tano. Haya yote ni mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile bomba la mafuta ghafi la Uganda na Tanzania ambalo linaendelea na Serikali imetoa shilingi bilioni 465.96 ambazo tunaendelea kutoa kama *share* yetu ya Tanzania; na ujenzi wa bandari za maziwa makuu Victoria, Tanganyika na Nyasa pamoja na meli zinaendelea kujengwa. Hapa sijazungumzia mambo mbalimbali yanayofanyika na fedha kwenye Halmshauri zetu zinzenda za kutosha sana. Haya ni mambo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yuko mtu mwingine anasema, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu (nilisema hapa jana kwamba), ni kama hapendi kuhamishia Makao Makuu Dodoma. Niseme tu, Serikali hii ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwanza yenyewe imehamia Dodoma yote. Rais yuko Dodoma na Waziri Mkuu yuko Dodoma. Pengine Waheshimiwa Wabunge, wananchi wetu pengine hawafiki, lakini sisi tunaofika tuseme. Rais yuko hapa, Ikulu inajengwa hapa, tunajua; Makao Makuu ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania yanajengwa hapa, ni kubwa kama ilivyo Pentagon; tumefika, tunajua na mnatoa taarifa, lakini vyombo vya ulinzi na usalama vyote viko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja kati ya vitu vya muhimu katika kuhamisha Makao Makuu ya nchi yoyote ni pamoja na mihimili yote kuwepo hapa. Inajengwa Mahakama kubwa kweli kweli, jengo lake ni kubwa sana, mhimili wa Mahakama. Pia tumetenga bajeti ya fedha hapa kwa ajili ya ujenzi wa

*International Airport,* kwa sababu Makao Makuu lazima yawe *international destination.* Kwa hiyo, lazima *airport* iwe ya Kimataifa, inajengwa, na Serikali imetenga Shilingi bilioni 394. Fedha hizi zote zinaimarisha uhamiaji wa Makao Makuu Dodoma. Ila anakaa mtu mwingine anasema Rais hapendi, amesikia wapi? Sisi tunaamini Serikali inafanya mambo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga Shilingi bilioni 250 kwa mwaka 2021/2022 kwa ajili ya majengo ya Serikali na mwaka huu imetenga Shilingi bilioni 300 kwa ajili ya majengo ya Serikali peke yake. Iko barabara ya mzunguko ya Dodoma, imetengwa Shilingi bilioni 221, barabara za *TARURA* Shilingi bilioni 102, *airport* kama nilivyosema Shilingi bilioni 394, miradi ya maji kwa Dodoma Shilingi bilioni 296, na miradi ya umeme Shilingi bilioni 216. Unasemaje hakuna nia ya dhati ya Serikali kuhamia Dodoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ndio mratibu mkuu, anasaidiwa na sisi Mawaziri wake, shughuli inaenda vizuri, na Dodoma inabadilika. Wale wanaochelewachelewa kufikiri kutakuwa kuna maamuzi mengineyo, hayapo, mnachelewa kupata fursa ya Dodoma ambayo inakwenda kuwa Mji Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana walipa kodi wa nchi hii. Nachukua nafasi hii kuwashukuru sana viongozi wetu wanaotuongoza katika maono ya kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele. Kama kuna mambo ambayo ni muhimu sana ni pale ambapo Bunge lako lilitusaidia katika kutoa maoni ya wadau katika ujenzi wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, *blueprint* inaendelea, wamechangia Waheshimiwa Wabunge hapa. Tumeendelea kukubaliana katika michango mingi waliyoisema, nami kama mratibu wa Serikali nimehakikisha kwamba tunajadiliana na Mheshimiwa

Spika yale yote Waheshimiwa Wabunge waliyoyasema kwamba taasisi za *regulatory authorities* ziachwe zifanye kazi yake ya ku-*regulate,* na *TBS* ifanye kazi yake ya ku-*set standard.* Tumekubaliana, na yote haya yatasemwa tukishafikia wakati wa *Finance Bill. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Haya, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge ambao hawakupata nafasi ya kutangazwa ile asubuhi, sasa wasimame wote kwa pamoja. Karibuni sana wageni wetu, tunaamini mmewaona Wabunge wenu humu ndani wakifanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo Watendaji Kata, Vijiji na Mitaa 58 kutoka maeneo mbalimbali nchini wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndg. Robert Maziku. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, aweze kuchangia hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia kuwa hapa leo katika mwendelezo wa kujadili Bajeti Kuu ya Serikali. Hii yote ni uwezo wake Mungu, tumshukuru sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Makamu wa Kwanza na wa Pili wa kule Zanzibar; nawashukuru Mawaziri wote;

namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelekezo yake na ulezi wake; nawashukuru Mawaziri wetu na Manaibu Mawaziri wenzangu; pia, naomba nimshukuru sana *mentor* wangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ambaye yeye ni kocha wangu kwa maelekezo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, kipekee sasa naomba kumshukuru na kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Huyu ni mama. Mungu alivyojalia mama ndiye mtu peke yake ulimwenguni ambaye ana uwezo mkubwa sana wa kutafsiri kilio au chozi la mtoto wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano. Mama mtoto wake wa wiki moja tu anapolia anaweza kutafsiri. Yaani akilia tu, anajua aah, mtoto wangu sasa hivi anahisi kiu, hebu naomba maji tumlambishe kidogo. Huu ni uwezo mkubwa wa kutafsiri. Akilia tena kwa mara nyingine, anasema mmh, sasa anahisi usingizi huyu, hebu mlaze kidogo. Akilia tena anasema, kwa kilio hiki sasa, ama chozi hili sasa, anaumwa na tumbo au homa. Kwa hiyo, mama ana uwezo mkubwa sana wa kutafsiri kilio cha watoto wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana bajeti yetu hii ambayo tumeiwasilisha kwenu Waheshimiwa, imetafsiri vilio vya wananchi wake. Huyo ndiye mama. Kama ungeniruhusu nikasema, nani kama mama? Ningesema, lakini eeh! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze kwenye hoja chache ambazo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezitoa na kujadili. Hoja ya kwanza ambayo nitaanza leo, Wabunge wengi walisema kwamba, sasa Serikali iweze kutoa bure mashine za *EFD*. Walipa kodi; wananchi, wafanyabiashara wadogo na wakubwa bado wataendelea kujirejeshea gharama kupitia makato yale ya kila mwaka. Wahenga wanasema, penye taabu na mashaka hapakosi badiliko.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TRA* imeanzisha mfumo mpya sasa ambao hautalazimika mfanyabiashara mdogo au mwingine kununua mashine hizi. Kinacholazimika kuwanacho mfanyabiashara hapa sasa ni simu tu ya mkononi. Kuwa na *smart phone,* awe na *computer* au kishkwambi, basi ataunganishwa na *internet,* anaweza kutumia huduma hiyo. Itatusaidia sana kupunguza gharama za matumizi ya makaratasi; itasaidia sana *smart phone* yako hii hata risiti zitakuwa hazina upotevu kwa sababu ziko ndani ya simu yako; pia itasaidia tatizo la kufutikafutika, kama swali ambalo limeulizwa juzi hapa, risiti haitakuwa na kufutikafutika. Mfumo huu utaanza Julai mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo hoja nyingine ambayo imezungumzwa kuhusu mwingiliano wa majukumu kati ya *ZRB* na *TRA*. Hili tayari tumeshalifanyia kazi na *weekend* hii inayofuata, kesho, tutakuwa na wenzetu kutoka Zanzibar, tutakaa kwa pamoja tuweke sawa ili kurahisisha na kuondoa mzigo mkubwa kwa wafanyabiashara au wawekezaji kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iko hoja baadhi ya Wabunge wamesema kwenye mfumo wa manunuzi ule wa *TANePS* tutumie lugha zote Kifaransa, Kiingereza, Kireno, Kiswahili, lakini kwa matumizi ya Serikali lugha zinazotumika leo ndani ya Serikali yetu lugha za mawasiliano ni mbili; Kiswahili na Kiingereza, basi tutahakikisha kwamba mfumo huu umetumia lugha hizi mbili za Kiswahili na Kiingereza ili tusiweze kumwacha mtu nyuma, anayejua Kiingereza, anayejua Kiswahili wote watatumia mfumo huu kwa sababu tutahakikisha kwamba tumeweka lugha hii ili kuwarahisishia wafanyabiashara wetu ambao ndio walipa kodi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo suala ambalo limezungumzwa kuhusu *TIN* kwa vijana kuanzia vijana wenye umri wa miaka 18. Ushauri wa Wabunge ambao wametoa kwamba

tuendelee kutoa taaluma, basi tumechukua ushauri huu na tutaendelea kutoa taaluma kwenye *program* ya *TRA* taaluma juu ya walipa kodi, lakini niwaombe Wabunge wenzangu pia tuendelee kutoa taaluma kwa wananchi wetu. Hii itatusaidia sana kutambua vijana ambao wana uwezo gani, unamtambua kijana uwezo wake ni upi, siyo kwamba lazima alipe kodi kwa sababu ana *TIN* hapana, inatusadia pia kujua uwezo wao, lakini inawezekana hata kutambulika kwamba wewe unaponunua vocha, basi unalipia kodi, inawezekana siku moja ukawa *appreciated* na wewe kwamba wewe ni mlipa kodi mzuri.

Mheshimiwa Spika, wako baadhi ya Wabunge kama vile Mheshimiwa Twaha, Mheshimiwa Msukuma walisema tupunguze ule mzigo. Unapokuwa una *TIN,* leo kijana anatoka kijijini huko anahitaji leseni ya pikipiki au gari, lazima aende mkoa, akifika pale anaambiwa tafuta *TIN* kwanza, hakuna haja ya kwenda huko tunataka tuwe na kitu kimoja tu. Ukiingiza namba za *NIDA* basi kila kitu chako kinapatikana pale, siyo lazima uzunguke huku na kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mengi ambayo yamezungumzwa na Wabunge wamechangia vizuri kabisa katika ujenzi wa Taifa lao. Amezungumza ndugu yangu hapa kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa kuhusu asilimia 10 ambayo imezungumzwa na wengi na Mheshimiwa King anasema mtemewa mate na wengi, basi lazima hulowa. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wangu ataeleza vizuri kabisa katika suala hilo.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa hayo machache, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Siku ya Jumanne tarehe 14 Juni, 2022, niliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/2023 na mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Katika hotuba zangu nilieleza masuala mbalimbali yaliyotekelezwa na Serikali katika kipindi cha mwaka 2021/2022 na matokeo ya utekelezaji wa changamoto zilizojitokeza na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo. Aidha, nilieleza pia vipaumbele ambavyo Serikali inakusudia kutekeleza na mapendekezo ya bajeti kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kulishukuru Bunge lako Tukufu na uongozi wako wewe mwenyewe pamoja na Naibu wako na Wenyeviti wako kwa jinsi ambavyo mmeendesha kwa weledi mkubwa mjadala huu wenye manufaa makubwa kwa Taifa letu. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wamedhihirisha wazi kwamba wao ni wawakilishi wa wananchi, tena wawakilishi sahihi kwa hoja ambazo wamezitoa kupitia hotuba hii, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali, napenda kutambua michango adhimu iliyotolewa na Kamati yangu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi. Serikali inaahidi kuendelea kushirikiana na Kamati katika utekelezaji wa majukumu haya. Nawashukuru na Wajumbe wote wa Kamati kwa michango yao mizuri hata wakati tunajadili uandaaji wa *Finance Bill* ambayo tutaiwasilisha wiki ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, Wabunge waliochangia kwa idadi yao ni 225 na wengine wamechangia kwa maandishi. Michango na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote imeridhisha na tutaifanyia kazi, mengine tutayajibu kwa maandishi na mengine tutaendelea kuifafanua tutakapokuwa tunajadili *Finance Bill* kwa sababu yanahusisha *Finance Bill*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake thabiti ambao umeonesha dira na matumaini mapya kwa Taifa letu. Baadhi ya masuala ya msingi yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais kwa kifupi ni kuendeleza kuweka mitaji, kuendeleza utekelezaji wa miradi ya maendeleo, utoaji wa huduma za kijamii, kuendeleza kuimarisha amani, umoja na mshikamano wa Taifa letu, kuendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi na kuendelea kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine, Jumuiya za Kikanda, Mashirika ya Kimataifa. Natoa rai kwa wananchi wote tuzidi kumwombea Mheshimiwa Rais, Mungu azidi kumjaalia afya njema, hekima na busara katika kuliongoza Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa hoja na michango mbalimbali iliyotolewa na Wabunge kwa siku saba hatuwezi tukaifafanua yote katika muda mfupi, kama nilivyosema mengine tutajibu kwa maandishi na mengine tutaendelea kufafanua katika mjadala utakaofuata wa *Finance Bill*. Nitumie fursa hii kuwashukuru Viongozi Wakuu wanaomsaidia Mheshimiwa Rais akiwepo Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu na niwashukuru Mawaziri wenzangu ambao tumesaidiana katika kuandaa ufafanuzi wa hoja hizi na zingine kama ambavyo mmetoka kusikia, wameshazitoa za kisekta na zingine za Mawaziri ambao hawajasimama kutoa ufafanuzi kwa ajili ya muda, tumeshirikiana na tumezijumuisha katika majibu tutakayoyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia Naibu Mawaziri wakiongozwa na Naibu Waziri mashuhuri sana Ndugu yangu Chande kama ambavyo mmeona alivyotoka kuhitimisha hoja yake hapa kwa ushirikiano mkubwa anaonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kujibu hoja ambazo zilitolewa nitambue maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa katika baadhi ya maeneo, nikianza na maeneo mahsusi ambayo aliyasema ambayo yalichangiwa kwa kiwango kikubwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, suala la asilimia 10 sisi tulikaa pamoja na Wizara ya Kisekta, mimi pamoja na ndugu yangu Bashungwa pamoja na timu zetu za wataalam, tukalileta jambo hili na tulichokusudia ilikuwa namna ya kukabiliana na changamoto za kibajeti ili tuweze hapo hapo kuendeleza ujenzi wa miundombinu ambayo imeonekana ni hitaji la msingi na wakati huo huo tusiathiri sana shughuli za ukopeshaji ambazo zilikuwa zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, niwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba wazo hili lilikuwa tu na nia njema na sisi tuliliibua katika namna ya kuwaza tuna-*balance* vipi masuala ya kibajeti. Nilipita kwenye *corridor* baadhi ya maeneo nikakuta wengine wanasema hili wazo kashinikiza Waziri Mkuu, wengine wanasema hivi, halikuwa na maelekezo mahsusi ya aina hiyo. Sisi tuliibua na mwenzangu tena tulikuwa na timu zote za wataalam, tukawa tunahangaika tufanyeje...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba ukiwa unazungumza utazame kisemeo kwa sababu ukigeuka, wale watu wa Taarifa Rasmi za Bunge watakosa maneno.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa hiyo, tulikuwa tumekaa tukawa tunahangaika hizi namba tuzichezeshe namna gani na tulipopeleka kupata

*clearance* kwa viongozi wetu walilitilia mashaka kwamba litapokelewaje hili lilivyo hivi. Mheshimiwa Rais alikuwa na mashaka nalo sana kwamba litapokelewaji hivi, lakini mimi pamoja na mwenzangu tulijenga hoja tukiwa na matumaini kwamba kwa sababu tunaleta fedha nyingine ya kukopesha, kwa hiyo, tulikuwa tunajua tutapunguza hii ya kukopesha iende kwenye miundombinu, halafu tulete nyingine ya kukopesha kufidia hapo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo baada ya michango mingi ya Wabunge na niwahakikishie Mheshimiwa Rais amefuatilia michango yenu, maelekezo aliyotupatia tulipopeleka mrejesho wa mjadala alisema Wizara pamoja na wataalam wasikilizeni wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo, tumepokea maelekezo ya Mheshimiwa Rais pamoja na kuridhika na ushauri tuliopewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, utakubaliana nami kwamba kwenye jambo hili karibu kila Mbunge aliyesimama pamoja na michango mingine aliyokuwa nayo hakuacha kusema jambo hili na sisi kama Wizara tumekubaliana kuwasikiliza wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo jambo hili la asilimia litabaki vilevile kama lilivyokuwa likitumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mama yangu mlezi wa Mkoa wa Singida mstaafu, mama yangu Khadija Taya, jambo hili uwaambie na unaowawakilisha tumesikiliza, limebaki vilevile na tunazingatia pia hoja mpya zilizotolewa zilizokuwa zikihusisha kuangalia uwezekano wa kuiongeza hii asilimia. Kwa hiyo, kadri Mfuko utakavyokuwa unaruhusu tutaendelea kuliangalia. Nilimsikia Mheshimiwa Shonza, nilimsikia nani mama yangu yule wa Mkoa wa Kusini kule akisemea ifike asilimia 20, tutaendelea kuangalia kufuatana na hali inavyoruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Kisekta kwa yale majiji au manispaa

ambao wana uhitaji mkubwa sana wa kuweka hiyo miundombinu na wana fursa ya kuweza kuchukua katika sehemu ya fedha za maendeleo hawatazuiwa kufanya hivyo kama ambavyo wale wa Dodoma walivyofanya, walichukua kutoka fedha za ndani, wakaongeza katika ujenzi wa soko kama walivyofanya na Serikali Kuu ikaweza kuwasaidia. Kwa hiyo, kwa jambo hili tumepokea na tutafanya kama ambavyo tumeliweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja zingine zilizojitokeza ilikuwa ni upande wa utekelezaji wa mabadiliko tuliyotaka kufanya kuweza ku-*accommodate* ile *blueprint*. Nia ilikuwa njema, tulikuwa tunataka tupunguze utitiri wa *agencies* zinazoenda kukusanya kwa mtu mmoja, nia yetu ilikuwa hiyo kwamba tupunguze, kama nilivyowaambia siku nilipokuwa nasoma bajeti hii kwamba, Mheshimiwa Rais ameshatoa maelekezo ambayo yanalenga namna ya kuboresha utendaji kazi katika nchi hii. Niliwaambia siku ile kwamba katika sisi wasaidizi wake kutafsiri kuna maeneo tunaweza tukakosea kwenye kutafsiri, nia ilikuwa njema inayolenga kuwapunguzia wananchi kwa kweli, hilo sisi Wabunge wanakumbuka tumekuwa tukililia siku nyingi, utitiri wa watu mtu mmoja mmoja kila mmoja kwenda kwa mtu yule yule kwenda kukusanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hivyo hivyo na kwenye usimamizi, tulikuwa tunalenga kuangalia uwezekano wa kupunguza utitiri wa kila mtu kwenda kusimamia eneo lile lile. Kwa hiyo nia ilikuwa hivyo. Hata hivyo, baada ya kusikiliza sana ushauri wa Wabunge ulivyotolewa Mheshimiwa Rais alisema tuwasikilize wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo lile jambo ambalo lililokuwa linahusisha kwenye pamba, lililokuwa linahusisha kwenye *TMDA,* lililokuwa linahusisha kwenye *EWURA,* lililokuwa linahusisha kwenye ubora wa mawasiliano la *TCRA,* yale ambayo tulisema sasa yafanywe na *TBS* yatabaki kama ilivyokuwa kwa kuzingatia aina ya majukumu yenyewe kwamba yanakuwa na ufanisi zaidi yakifanywa na

maeneo husika, yale ambayo yana uzoefu na yana utaalam, lakini pia na majukumu yale yanaendana na eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililoongelewa zaidi lilikuwa jambo linalohusisha asilimia mbili ile *withholding* kwa wachimbaji wadogo wadogo. Hili na lenyewe Mheshimiwa Rais amefuatilia mjadala, lakini pia kafuatilia na maoni yaliyokuwa yanatolewa na wachimbaji wadogo kote nchini na yeye akasema yeye ni mama wa wachimbaji wadogo, akasema tuwasikilize wawakilishi wa wananchi. Sisi kama Wizara tumewasiliana na Wizara ya Kisekta ya Mheshimiwa Doto pamoja na timu yake na jambo hilo limezingatiwa litabaki kama lilivyokuwa mwanzoni kabla ya kuleta mapendekezo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wakati huwa tunachanganya Kinyiramba na Kiswahili maana yake naahirisha lile pendekezo nililoliteta, kwa hiyo tunarudi kwenye hali iliyokuwa ya awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo liliongelewa kwa upana na lilikuwa na maelekezo na lilikuwa linajitokeza kwenye Kamati kama ambavyo Waziri wa kisekta amesema ni lile lililokuwa linahusisha *TASAC* kufanya majukumu yake kama *regulator* na kupunguza majukumu yale ya upande wa kibiashara. Hili na lenyewe tumesikiliza maoni ya wawakilishi wa wananchi litafanyiwa kazi na utaratibu na usimamizi wake namna gani lifanyike na katika kiwango gani, litatekelezwa kwa kupitia kanuni na Wizara ya Kisekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo liliongelewa kwa kirefu lilikuwa linahusisha Tume ya Upimaji ile ya Ardhi; Waheshimiwa Wabunge waliongea wakati wa Wizara ya Kisekta, lakini hata tulipokuja kwenye mjadala huu liliongelewa sana na kama nilivyosema ni ngumu kutaja mtu mmoja, lakini liliongelewa kwa kiwango cha juu sana na

tuliahidi kwamba tutakuja kusema siku tutakapokuja kwenye kuhitimisha Bajeti Kuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amewasikiliza wawakilishi wa wananchi na kama ambavyo kiwango cha kuanzia kiliombwa, tumeridhia Wizara ya Fedha, maoni ambayo yalitolewa tutaongeza shilingi bilioni nne ili kuweza kufikisha nusu kwa maana ya bilioni tano za kuanzia ili tuendelee kusubiria fedha zile zingine za mkopo ambazo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wamependekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasemea yale ambayo yalikuwa yamesemwa, yapo na mengine ambayo yanahusisha *Finance Bill,* tutaendelea kuyafafanua kwa sababu tutaleta *Finance Bill,* ni ngumu kutaja kila kitu ambacho kilitajwa kwa sababu muda hautatosha kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye ufafanuzi; kuna jambo liliongelewa linalohusisha maduka ya kubadilishia fedha, nilimsikia Mbunge wa Arusha, Mbunge wa Moshi Mjini, nilimsikia Mbunge Balozi wa afya ya akili ambaye ni Mbunge wa Iringa Mjini; jambo hili limeshafanyiwa kazi. Nililiahidi Bunge lako Tukufu kwamba mpaka ifikapo wiki ya kwanza ya Julai, tathmini inayofanyika itakuwa imeshakamilika na baada ya hapo tutakwenda kwenye utekelezaji kufuatana na tathmini hiyo. Pamoja na maoni yaliyotolewa yanayoendana na jambo hilo yakiwepo ufanyaji kazi wa maeneo yale pamoja na utendaji kazi katika masuala yatakayofuata yale mengine.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka hata mtani wangu Mheshimiwa Cecilia Paresso, alilisema kwa umakini mkubwa na kwa kweli kambi ya wachache wameshiriki vizuri tu katika kutoa maoni na Mungu awape utulivu wa mawazo, wamechangia vizuri. Hayo yote tutakwenda kuyajumuisha

baada ya tarehe 4 tunaenda kwenye utekelezaji wa jambo hilo. Tathmini inakamilika, limeshafanyiwa kazi kwa kina na tunaamini tutaangalia kwenye yale malalamiko yaliyokuwepo na tutaangalia katika yale mazingira ya ufanyaji kazi kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamelisemea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo lilisemewa lilikuwa jambo linalohusisha Deni la Taifa. Naomba tuelewane vizuri sana kwenye hili jambo la Deni la Taifa; kwanza duniani kote nchi zote zinazotekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, nchi zote ambazo zina uchumi mkubwa na nchi zote zinazotoka kwenye umaskini zinakwenda kwenye uchumi mkubwa ndizo zenye madeni makubwa. Hiyo *equation* iko hivyo, Wabunge waende wakaangalie kwenye kumbukumbu zao, ndivyo zilivyo, huwezi ukalinganisha deni la Tanzania na deni la Marekani kwa sababu uchumi wetu haulingani, hivyo ndivyo ilivyo. Wao wana uchumi mkubwa zaidi na wana deni kubwa zaidi hivyo hivyo ukienda Japan, nchi zote ambazo zina uchumi mkubwa ndizo ambazo zina madeni makubwa hivyo ndivyo ilivyo. Si vizuri kutaja nchi zingine unapotoka kutolea mfano ulio mbaya, lakini Wabunge waende kwenye nchi maskini watakuta zingine hata hazikopesheki, hazina hata deni, hivyo ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili nilidhani tuelewane kwanza, watu wajue kwamba kadri unavyoenda kwenye kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo ndivyo deni lako linavyokua. Hivyo ndivyo ilivyo! Kwa hiyo, ni uchaguzi wako tu unaweza ukaamua usitekeleza kabisa miradi ya maendeleo kwa njia hiyo halafu ukawa na *clean sheet,* huna deni kabisa. Kwa mfano, Tanzania kabla haijaunganisha barabara za lami Mikoa yote deni lake lilikuwa chini ya Bilioni Kumi ndivyo ilivyo. Ilikuwa ukitaka kutoka Kagera ama ukitaka kutoka Mara kwenda Dar es Salaam inabidi upite Kenya, ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ukitoka Mbeya ukitaka kuja Dodoma tena Mbeya mbali, kutoka Iringa kuja hapa Dodoma ilikuwa lazima upitie Morogoro, tukaunganisha hapa kwa mkopo, kwa hiyo tukapata barabara ila tukatengeneza deni, ndivyo ilivyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ukitaka kutoka Iringa kwenda Bahati ni lazima upite Morogoro upite Chalinze, upite Korogwe, upite Arusha ndiyo uende Babati. Tukatengeneza deni kwa kuchukua mkopo tukaunganisha hapo, ndivyo ilivyo. Wakati mimi ninaanza *First Year* nchi nzima tulikuwa wanafunzi 2,700 ndiyo watu walioenda Chuo Kikuu, tumetengeneza deni tukajenga *UDOM* ndivyo ilivyo ni uamuzi tu tungeweza kutokukopa halafu tukabakiza wale watoto waliokuwa wanakwenda shule wale wale, ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa miradi ya aina hii ni mingi tu, nimetaja hii michache tu. Kwa mfano, leo hii tuna-*enjoy 4G, 5G* zote hizo na ku-*peruse* tunakofanya, lakini mkonge wetu wa Taifa ule ni mkopo, kwa hiyo tumetengeneza deni tukaingia kwenye *data,* ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi ya aina hiyo ni mingi na hili linahitaji siku nzima, siku nyingine tupate fursa ili Wawakilishi wa Wananchi wajue hili jambo likoje ili tuwapitishe kuanzia mkopo wa kwanza uliokopwa kuanzia mwaka 1961 baada tu ya Uhuru, mkopo wa miundombinu, tuendelee hivyo tuupitie mmoja na mwingine na mwingine Wawakilishi wajue, kwa sababu wengine hata wanadhani wakisikia hapa deni limeongezeka kwa asilimia 14.4 wanasema ina maana mwaka mmoja tu deni limeongezeka kwa Trilioni Kumi, mwaka mmoja tu deni limeongezeka Trilioni Kumi, yaani kwa mwaka mmoja tu deni limeongezeka kwa asilimia 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaambie Watanzania waelewe pia na kwenye hili, kwamba Deni la Taifa ni tofauti na fedha ya

kwenye *ATM,* siyo unaingiza kadi tu unachomoa deni linaongezeka, deni ni mikataba inayosainiwa na fedha zitakuwa zinaingia kufuatana na mikataba ilivyokubalika, malipo yatakuwa yanalipwa kufuatana na mikataba ilivyosainiwa. Kwa hiyo, kuna madeni ambayo tumemalizia kulipa ya Awamu ya Kwanza. Mimi mwenyewe nimesaini kulipa deni ambalo lilikopwa kabla sijazaliwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna madeni tunamalizia kulipa ya Awamu ya Pili, kuna madeni tunamalizia kulipa ya Awamu ya Tatu, kuna madeni tunamalizia kulipa ya Awamu ya Nne, kuna madeni tunaendelea kulipa ya Awamu ya Tano na kuna madeni ambayo yatakuja kuanza kulipwa ambayo tunakopa sasa hivi, hivyo ndivyo inavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo wala usiumize kichwa kutaka kujua limekopwa lini kwa sababu anayekopa siyo Rais, mnatafuta kitu kwenye kichaka ambacho sicho, *you will never find it,* anayekopa siyo Rais, inakopeshwa Serikali. Mikopo yote ya nchi yetu haikopeshwi kwa awamu, kuna nchi ambazo zinakopa kwa awamu, kwamba unakopa lakini kabla haujamaliza awamu yako uwe umeshalipa, mikopo ya aina hiyo riba zake ni kubwa sana ambazo Taifa haliwezi likamudu kwa mwenendo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mikopo ambayo ni nafuu inakuwa ni ya muda mrefu, huwezi ukaukataa mkopo wa *concession loan* ambayo ni ya miaka thelathini, thelathini na tano ukakataa kwa sababu unaondoka utakuwa umefanya uamuzi wa kibinafsi, *actually* mikopo ile ya muda mrefu ndio inayotakiwa zaidi kuliko ile ya muda mfupi. Kwa maana hiyo, mikopo ya Bwawa la Mwalimu Nyerere ilishasainiwa kwa sababu mradi unaendelea tunaendelea kupokea fedha zake. Mikopo ya *SGR* ilishakopwa tunaendelea kupokea kwa sababu mradi wake unaendelea, hivyo hivyo miradi mikubwa kama hiyo ya Benki ya Dunia, hii *BOOST* na *HEET* pamoja na

miradi mingine mikubwa ya aina hiyo, fedha haitoki siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashahidi, miradi ya vijiji 10 vya maji ilichukua muda gani, wengine mmeanza kusikia mngali hamjawa Bungeni humu, hivyo ndivyo inavyokuwa. Kwa hiyo, mradi ukishasainiwa fedha zake zitaendelea kuingia, kadri fedha zinavyoingia deni linapanda upya siyo kwamba imesainiwa jana. Sasa hivi tumepata mkopo wa masharti nafuu sana ule wa UVIKO, tena mkopo usio na riba, ulikuwa *free* kabisa kabisa hauna riba. Mama yetu ameenda ameongea na Mtendaji Mkuu amepewa mkopo usio na riba, mkopo wa aina hiyo huwezi ukauacha kwa sababu watangulizi walishakopa na deni limeshakuwa kubwa, huwezi ukauacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo na mikopo mingine ipo ya aina hiyo miradi ikiwa inaendelea huwezi ukaacha kukopa kwa sababu unaogopa deni litaongezeka. Chukulieni mfano tu, hivi upi ni uamuzi wa busara kwamba reli iishie Morogoro tu kwa sababu deni litakua au iishie Manyoni pale hadi tulipe deni lote liishe kwa sababu tukiongeza ikaenda hadi Kigoma unajua deni litakua, itakuwa *white elephant* ikiiachia njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, reli siyo daladala hata igeuzie Singida pale, huo ni uamuzi ambao unatakiwa ufanyike ili ufungue uchumi halafu ule uchumi ulipie madeni. Niwahakikishie Watanzania hakuna mkopo unaokopwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, hakuna mkopo unaokopwa kwa ajili ya mishahara, hakuna mkopo unakopwa kwa ajili ya posho, ni miradi ya maendeleo inayofungua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fikirieni kama hivi leo kuna maeneo tumewahi kukopa tukatengeneza miundombinu, tumewahi kukopa mikopo tukatengeneza miundominu, kama hivi sasa ukitaka kutoka hapa Dodoma kwenda Babati tumejenga

kwa mkopo, halafu leo hii kuna Wilaya ambazo hazijawahi kuonja barabara kama hizo za Ifakara, wapi huko kwenda hadi Rumecha huko Songea, hazijawahi kuonja barabara ya lami yaani ufike muda wao wa kuchukua mkopo kujenga barabara hiyo mseme deni limeshakuwa kubwa wao waendelee kulipa ya wengine ambao wanapita kwenye lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya aina hiyo ipo mingi ambayo ina changamoto za aina hiyo, kama huku Manyara kwa ndugu yangu Issaay na Flatei hadi anaamua kupiga *samasoti* hawajaonja barabara ya lami, hivyo hivyo huko wapi huko Sibiti kwa ndugu yangu Isack Francis huko Lalago Maswa, Mbunge wa Ngudu juzi ameongea kwa hisia kali sana na jambo hilo tumeongea na Mheshimiwa Waziri wa kisekta. Deni lipo maadam miradi ya maendeleo tumefanya utaratibu huo, haiwezi ikafikia hatua mojawapo tukauachia mradi njiani, lazima tuendelee, ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuendelei kama vipofu, ndiyo maana Wizara hizi zote zina wataalam, hatuendelei kama vipofu. Deni la Serikali uwiano wake na pato la Taifa bado tupo asilimia 31, ukomo ni asilimia 55. Hivi viwango hivi haijaweka Tanzania ni vya Benki ya Dunia. Tupo asilimia 31 ukomo ni asilimia 40, deni la nje kwa uwiano wa Pato la Taifa tupo asilimia 18 ukomo wake ni asilimia 40. Deni la nje kwa uwiano wa mauzo ya nje tupo asilimia 142 ukomo wake ni asilimia 180.

Mheshimiwa Rais kati ya kitu ambacho anakiangalia sana ni kuhakikisha kwamba moja tupate mikopo ambayo ina masharti nafuu ambayo haiwapi mzigo Watanzania, lakini la pili anaangalia tupate mikopo ambayo inakwenda kwenye shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo liliongelewa sana ni jambo la ukopeshaji wa magari kwa watumishi wa

umma. Hili jambo nchi zilizoendelea zote ndivyo wanavyofanya, ni kwa ajili ya udhibiti wa matumizi ya vitendea kazi hivi na tunapopitisha sheria hatulengi watu, tusiwaze kibinafsi, hatulengi watu, tunatengeneza sheria kwa ajili ya nchi, maana yake nini tunapotengeneza sheria kwa ajili ya nchi ni utaratibu ambao sio wa siku moja maana yake mtu mwingine anaanza kuwaza rafiki yake hapa. Hivi ninyi mnafikiri mimi naweza nikafika hadi ngazi hii hapa niwe sina rafiki, nina marafiki karibu kila eneo, lakini tunapotengeneza mapendekezo tunatafsiri dira ya Mheshimiwa Rais anavyyowaonea huruma Watanzania huruma ya kubeba mzigo mkubwa, anataka fedha hizo ziende kwenye maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake nini, maana yake itafanyika *gradually,* sheria ikishabadilika kama tulivyoanza, sasa hivi Serikali ina magari zaidi ya 15,000 hajanunuliwa leo leo yote yale, yameanza kununuliwa siku nyingi. Kwa hiyo, hata kwenye kuondoka kwenye utaratibu huo hauondoki siku moja, unaenda kwa sheria, kwamba sheria ikishapita wale watakaofuata baada ya hiyo sheria wataanza kwenda kwa matakwa ya sheria yake. Kwa hiyo, wala hamna haki ya mtumishi itakayopotea, ni utaratibu ambao ndivyo nchi nyingine wanavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatupotezi haki ya mtu kwamba anayepanda sasa akopeshwe gari yake, alipe, si ndio sheria itakuwa imesema hivyo atalipa mkopo ule kadri anavyofanya kazi, atapewa huduma nyingine ambazo zinastahili, lakini atasimamia hivi vingine vinavyotupotezea sisi fedha. Hivyo hivyo kwa sababu wataanza kupungua maana yake dereva akistaafu kwa sababu huku watakaokuwa wameajiriwa wameshakuwa na magari yao maana yake hatuajiri wa kada hiyo, wanaenda hivyo hivyo hatufukuzi mtu wala hatupotezi haki ya mtu yeyote, hivi ndivyo wanavyofanya mataifa mengine ili tuwapunguzie Watanzania mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunakubaliana kwakweli matumizi ya sekta hiyo hayapo vizuri. Sasa wengine jambo ukishatoa hoja hivi wanasema mbona wewe unatumia, tunasema tunaanza hatua kwa hatua, Rwanda wenzetu wamebakiza Viongozi Wakuu tu ndio wanaofanya hivyo, Mawaziri wote na watumishi wengine wote wapo hivyo hivyo. Kwa hiyo, hata sisi hilo ni jambo jema tu tukifikia hatua hii hiyo hiyo siyo jambo baya kabisa. Jambo lolote mimi linalohusisha kuwapa Watanzania mambo ya maendeleo namuunga mkono Rais mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la TEHAMA na lenyewe tumelisemea kwa ajili ya kupunguza gharama za matumizi, tumewekeza sana kwenye TEHAMA mambo ya Mkongo wa Taifa, *data center* pamoja na minara ya simu, ni gharama kubwa jamani tuzitumieni hizi mengine ni ya mikopo, huku tumewekeza tunadaiwa, huku hatutumii tunaweka gharama nyingine kwenye kufanya vitu *manually*, angalia jinsi ambavyo Bunge mmepunguza gharama nyinyi hapa baada ya kuondoa vile vitabu. Ilikuwa tukitoka hapa unaondoka hapa na msitu wa vitabu, vingine hata vinabaki njiani huko ukishapambana na shughuli za watu Majimboni unakuta vingine umevidondosha, lakini sasa hivi mnavyoenda kwa TEHAMA vitu vyote vya Bunge vipo salama lakini mmepunguza gharama, hata Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa kisekta ameshapokea maelekezo vizuri na amesema kwamba wapo tayari kuanza kulifanyia kazi jambo hili ili liweze kutekelezeka. Hata mikutano siyo yote, mingine ni ya kikatiba mingine ina ulazima wa aina hiyo, tulisema tupunguze mikutano ambayo haina ulazima wa aina hiyo, kwamba unaweza ukapata *product,* unaweza ukapta *output* ile ile hata kama ungefanya kwa njia ya mtandao hicho ndicho ambacho teknolojia imekuja kutusaidia kupunguza gharama za matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda wa kuhitimisha unaendelea kuisha, kuhusu suala la ma-*DED* Mheshimiwa Waziri wa kisekta ameshalisema vizuri, watu wengine walikuwa wanachanganya wanadhani hata mtu akipata *promotion* anatakiwa apate hiyo, jamani jambo lipo hivi, kwanza Mheshimiwa Rais kitu anachokizingatia sana ni haki za watumishi wa umma na Mheshimiwa Waziri kwenye sekta amesema vizuri sana. Maana yake nini kwenye hili pendekezo, maana yake taratibu za uteuzi zifuate *merits,* zifuate umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mtumishi anayeharibu taratibu za kumuondoa zifuate, sasa kama hivyo vitu vyote vimefuatwa wewe umeaminiwa ukapewa nafasi, halafu na umekosea taratibu za kutolewa zimefuatwa, unataka uendelee kulipwa vilevile kwa fedha za watu wanyonge, yaani wamlipe aliepo kazini wakulipe na wewe ambae haupo kazini, *I think we should not debate on this one*. Lazima tutengeneze utaratibu watu wawe na cha kujutia, hivi ilivyokuwa inaenda sasa hivi walikuwa hawana cha kupoteza, yaani mnachukua cheo chenu yeye anaendelea kulipwa hivyo hivyo! Tutatengeneza utaratibu wa uwajibikaji wawe na kitu cha kupoteza, watu lazima wawe na kitu cha kupoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiaminiwa kwenye majukumu ya umma lazima uwe na cha kupoteza ili uwajibike kwa wale wanaobeba mzigo wa wewe kuwa pale. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo Mheshimiwa Rais anapojali *good governance* ni pamoja na haya, nasi tunaamini sana hiyo dira aliyonayo Mheshimiwa Rais itaongeza uwajibikaji. Fikiria Mheshimiwa Mbunge wa Longido alichokuwa anatolea mfano, Mwenyekiti tu Halmashauri hajasomea ukusanyaji labda *field* yake hata siyo hiyo na jukumu lake siyo hilo la kimsingi yeye ni Mwakilishi, lakini anasimamia makusanyo yanaongezeka. Halafu leo hii akatokea mtu aliyepewa jukumu hilo hafanyi hilo, halafu akiondolewa anataka

tuendelee kumlipa kama yupo pale pale, hiyo Hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi mnafikiri mimi nimefika ngazi hii wale wenzangu niliosoma nao hawapo kwenye hizo ngazi nyingine hizo za kustahili magari au za kustahili katika nafasi hizo? Ninao sana marafiki wa aina hii, lakini nilisema katika tafsiri hii ambayo Mheshimiwa Rais amenituma wakitokea marafiki wa aina hiyo akasema wewe ulitusababisha tatizo ukiwa pale hata siku ukitoka, watu wa aina hiyo wakikukimbia wananchi wa Iramba watabaki ambao wanabaki nami hata nisipokuwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia nawaomba Waheshimiwa Wabunge waipitishe bajeti hii kwa kishindo na ombi la Mheshimiwa Rais, Wabunge mtakapounga mkono bajeti hii mna jambo la kuwaambia Watanzania kule waliowachagua. Jambo la kwanza mtawaambia mmepitisha bajeti hii kuunga mkono zaidi ya Bilioni 954 ziende kwenye kilimo, mtawaambia mmeunga mkono bajeti hii kuunga mkono jitihada za Rais za kupeleka zaidi ya Bilioni 268 kwenye mifugo na uvuvi, mtawaambia mmeunga mkono bajeti hii ili kuwaambia watoto wa maskini wale ambao walikuwa wanapata shida sana kuna Bilioni Nane za kuweza kuwasaidia ambao wengi wao walikuwa wakipata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtawaambia mmeunga mkono bajeti hii ili kuweza kuunga mkono Bilioni 150 ziende kwenye ruzuku, mtawaambia mmeunga mkono bajeti hii ili kuweza kutoa unafuu kwenye maisha ya Watanzania hasa kwenye gharama za vitu wanavyovitumia. Tumefanya hivyo kwenye mafuta ya kula, tumefanya hivyo kwenye ngano, tumefanya hivyo kwenye *fuel* (kwenye mafuta ya nishati) na tumefanya hivyo kwenye mbolea. Mtaenda kuwaambia mmeunga mkono bajeti hii ili kumuunga mkono Mheshimiwa Rais katika jitihada zake za kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia sekta za

uzalishaji. Tumetoa unafuu kwenye zile sekta zinazozalisha kwa kusamehe kodi, tozo, pamoja na ada mbalimbali ili sekta zile zinazozalisha ziweze kuchachua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtasema mmeunga mkono bajeti hii kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kujenga barabara katika maeneo ambayo barabara hizo hazipitiki, viporo vile vinavyounganisha Katavi pamoja na Kigoma, viporo hivi tulivyosema vya Bonde la Ifakara, viporo hivi vya Manyara, viporo hivi vya huku Simiyu, viporo vya kule Geita pamoja na maeneo mengine zile barabara ndogo ndogo ambazo tumezitaja, namuona Mbunge wa Kigoma Kaskazini Ndugu yangu Mheshimiwa Assa anaangalia ikiwemo hiyo ya Mwandiga - Kagunga ambayo Mbunge umeisemea kwa mara nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtasema pamoja na ile barabara ya Masasi - Nachingwea pamoja na Wilaya nyingine inayounganisha, mtasema mmepitisha bajeti hii kuunga mkono jitihada Rais anazozifanya kwenye nishati, gridi ya Taifa pamoja na Mikoa ambayo haijawahi kuwa kwenye gridi ya Taifa kuingia kwenye gridi ya Taifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri umebakiwa na dakika tatu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, mtasema mmepitisha bajeti hii kuunga mkono ujenzi wa *VETA* katika Wilaya ambazo hazijapata, lakini na vyuo hivi vya kiufundi ambavyo vimetolewa katika Mikoa yote ile ambayo ilikuwa bado haijapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia watu wengine wanaweza wasielewe hii habari ya elimu bila malipo kwenye sekondari zetu hasa Kidato cha Tano na Sita. Wengine wanaweza wakaona Shilingi 70,000 ni ndogo, mimi nilipotakiwa kwenda kufanya *matriculation,* mtihani ule wa kujiunga Chuo Kikuu nilikosa Shilingi 20,000 na ilikuwa ghafla

Baba akaniambia nenda kapate kwenye duka lile la pale kijijini siyo duka la Kijiji, ni duka la Ndugu yetu mmoja wa pale kijijini mwenye duka, alishafuata mizigo ikakosekana, nikaambiwa mfuate binamu yako Singida Mjini, nilienda kule nikakuta amefuata mahindi Sumbawanga, siku aliporudi ndiyo ilishabaki siku moja ya kulipia shilingi 20,000, watoto wa aina hii bado wapo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, wazo hili la Mheshimiwa Rais la kutoa ada kwenye Kidato cha Tano na Sita hasa hawa watoto wanaotoka shule zetu za Kata za vijijini, wazazi wa aina hiyo bado wapo. Siku nyingine nilikuwa napata *experience* na Mheshimiwa Ndugai akaelezea kisa cha mwanafunzi anayetokea Jimboni kwake, alikuwa anasoma shule moja kule Kilimanjaro, akaambiwa Mheshimiwa katika shule hii kuna mtoto anatoka kwenye Jimbo lako akitaka kununua hata *sanitary pads* lazima achangiwe na wenzake hapo. Watoto wa aina hiyo ambao wanakosa kabisa hizo fedha wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, hata hilo pendekezo alilolitoa Mheshimiwa Waziri wa kisekta, Waziri wa Elimu kwamba Serikali tutaendelea kuangalia kwa kadri uwezo unavyoruhusu hili jambo ni la msingi, tunaungana na Waziri wa kisekta kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, hivi vitu Mheshimiwa Rais alivyovifanya kwenye bajeti anaonesha anayafahamu maisha ya Watanzania na anawafahamu watu anaowaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twendeni tumuunge mkono na...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri sasa utoe hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Rais wakati anatupa maelekezo ya mwisho ametuambia hata zile Wilaya ambazo mlisemea

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha toa hoja sasa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, zile Wilaya ambazo mlizisemea ambazo zimeachwa nyuma siku nyingi amesema tuendelee kupata tathmini ili tuone mahitaji ni kitu gani kuonesha jinsi ambavyo anawafahamu Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwa mara nyingine waunge mkono bajeti hii kwa kura ya ndiyo na nitoe shukrani *in advance* kwa kura hiyo ya ndiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo nimshukuru tena kwa mara nyingine Naibu Waziri pamoja na wataalam wangu wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ambayo wanafanya bila kuwataja majina yao kwa ajili ya muda.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hoja imetolewa na imeungwa mkono na kwa utaratibu wetu hoja hii huwa inahojiwa kwa kila Mbunge kusema kwa kinywa chake anaikubali au anaikataa, zoezi hilo tutalifanya baadaye ambapo kila Mbunge ataitwa kwa jina lake, kwa hiyo ndiyo maana sijawahoji sasa hivi hoja itakuja baadaye mtahojiwa baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaendelea sana wageni wazito kidogo hawa, hawa ni watoto wetu kutoka Shule ya Sekondari Bunge Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hawa watoto wapo 245 lakini wameongozana na Walimu Watano, karibuni sana Walimu wa shule hii ya Bunge lakini pia karibuni sana watoto wetu tumefurahi sana kuwaona hapa Bungeni karibuni sana. Mtakumbuka shule hii ilijengwa na Wabunge, halafu Wabunge wakaikabidhi Serikali, kwa hiyo ni shule ya Serikali lakini imejengwa na Bunge kwa hiyo Wabunge jipongezeni na ninyi kwa mchango wenu mkubwa mlioutoa katika sekta ya elimu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na kabla sijasitisha shughuli za Bunge nawaomba sana lilitoka tangazo hapa la *CRDB* na semina kwamba tukitoka hapa tunaelekea Msekwa lakini kabla ya kuelekea Msekwa mnaombwa sana muelekee ile sehemu ambayo huwa tunaweka magari pale, halafu wote tutatokea pale kuelekea Msekwa, kwa hiyo tukitoka hapa tuelekee kwanza ile sehemu ya maegesho ya magari halafu tutaelekea Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya semina hiyo muhimu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninasitisha shughuli za Bunge hadi Saa Kumi na Moja jioni leo.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge Lililerejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo.

Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Bajeti Kuu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023; na sasa ni saa ya kupitisha ama kutokupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Na hoja yetu ni kwa kuita jina moja baada ya jingine. Sasa tutaanza kuwaita Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kusikia na kupata idadi ya Wabunge wangapi wanapitisha na Wabunge wangapi hawapitishi. Kura yetu ni ndiyo, hapana au huna uamuzi sijui inaitwaje ile Katibu kwa Kiswahili.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, hakuamua.

**SPIKA:** Kwa hiyo huna maamuzi. Kwa hivyo unasema sina maamuzi, ndiyo au hapana. Maana hii tunayoisemea ndiyo na hapana humu tumeshasema mambo ya kiswahili humu. Kwa hiyo mtu asianze kusema sijui maneno gani gani hivi, maneno ni sina uamuzi juu ya jambo hilo. Sasa tuaanza hilo zoezi Waheshimiwa Wabunge sasa tutaanza.

Katibu.

**KUPIGA KURA**

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

Mhe. Mussa Azzan Zungu……………………..…………………… Ndiyo
Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa.........................................Ndiyo
Mhe. Job Yustino Ndugai………………………………..……… Ndiyo
Mhe. Najma Murtaza Giga…………………………………...Ndiyo
Mhe. David Mwakiposa Kihenzile………………………….... Ndiyo
Mhe. Shamsi Vuai Nahodha……………………………......Ndiyo
Mhe. Salma Rashid Kikwete ………………………………......Ndiyo
Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika ……………………Ndiyo
Mhe. George Boniface Simbachawene …………………...Ndiyo
Mhe. Jenista Joakim Mhagama ……………………………Ndiyo
Mhe. Innocent Lugha Bashungwa ……………………………Ndiyo
Mhe. Selemani Saidi Jafo...................................................Ndiyo
Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako..................................Ndiyo
Mhe. Ummy Ally Mwalimu..................................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji..................................Ndiyo
Mhe. Hussein Mohamed Bashe..........................................Ndiyo
Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki.........................................Ndiyo
Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa...............................Ndiyo
Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba..............................Ndiyo
Mhe. January Yussuf Makamba..........................................Ndiyo
Mhe. Doto Mashaka Biteko……………………………………Ndiyo
Mhe. Balozi Liberata Rutageruka Mulamula..................Hayupo
Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax................................Ndiyo
Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni.....................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Angeline Sylvester Mabula................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro..................................Ndiyo
Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda.......................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima............................Ndiyo
Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana .................................Ndiyo
Mhe. Mohamed Omar Mchengerwa............................Hayupo
Mhe. Jumaa Hamidu Aweso................................................Ndiyo
Mhe. Nape Moses Nnauye...................................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi...........................................Ndiyo

Mhe. Deogratius John Ndejembi.........................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Festo John Dugange...........................................Ndiyo
Mhe. David Ernest Silinde.....................................................Ndiyo
Mhe. Khamis Hamza Khamis…………………………….............Ndiyo
Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga........................................Ndiyo
Mhe. Paschal Patrobass Katambi........................................Ndiyo
Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe.............................................Ndiyo
Mhe. Antony Peter Mavunde...............................................Ndiyo
Mhe. Abdallah Hamis Ulega................................................Ndiyo
Mhe. Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe..........................Ndiyo
Mhe. Atupele Fredy Mwakibete..........................................Ndiyo
Mhe. Hamad Hassan Chande............................................Ndiyo
Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato.....................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa.....................................Ndiyo
Mhe. Mbarouk Nassor Mbarouk..........................................Ndiyo
Mhe. Geophrey Mizengo Pinda...........................................Ndiyo
Mhe. Jumanne Abdallah ......................................................Ndiyo
Mhe. Ridhiwan Jakaya Kikwete...........................................Ndiyo
Mhe. Mary Francis Masanja..................................................Ndiyo
Mhe. Omari Juma Kipanga.................................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel..........................................Ndiyo
Mhe. Mwanaidi Ali Khamisi...................................................Ndiyo
Mhe. Pauline Philipo Gekul..................................................Ndiyo
Mhe. Eng. Maryprisca Winfred Mahundi.............................Ndiyo
Mhe. Eng. Andrea Mathew Kundo......................................Ndiyo
Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka.............................Ndiyo
Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama......................................Ndiyo
Mhe. Vita Rashid Kawawa...................................................Ndiyo
Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo......................................Ndiyo
Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo..........................................Ndiyo
Mhe. Ally Juma Makoa........................................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma...............................Ndiyo
Mhe. Moshi Selemani Kakoso...............................................Ndiyo
Mhe. Dunstan Luka Kitandula..............................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza......................................Ndiyo
Mhe. Daniel Baran Sillo.........................................................Ndiyo
Mhe. Jerry William Silaa.......................................................Ndiyo

Mhe. Fatma Hassan Toufiq....................................................Ndiyo
Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka..................Hakuamua
Mhe. Grace Victor Tendega..................................... Hakuamua
Mhe. Stella Ikupa Alex..........................................................Ndiyo
Mhe. Eric James Shigongo...................................................Ndiyo
Mhe. Vincent Paul Mbogo...................................................Ndiyo
Mhe. Dennis Lazaro Londo...................................................Ndiyo
Mhe. Aloyce John Kamamba ............................................Ndiyo
Mhe. Shabani Omari Shekilindi.............................................Ndiyo
Mhe. Athuman Almas Maige................................................Ndiyo
Mhe. Anne Kilango Malecela..............................................Ndiyo
Mhe. Seif Khamis Gulamali...................................................Ndiyo
Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda..........................................Ndiyo
Mhe. Omari Mohamed Kigua...............................................Ndiyo
Mhe. George Natany Malima..............................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage...........................................Ndiyo
Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga.......................................Ndiyo
Mhe. Selemani Jumanne Zedi............................................Ndiyo
Mhe. William Vangimembe Lukuvi......................................Ndiyo
Mhe. Capt. Abbas Ali Mwinyi..............................................Ndiyo
Mhe. Abdallah Dadi Chikota................................................Ndiyo
Mhe. Abdi Hija Mkasha........................................................Ndiyo
Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood....................................Ndiyo
Mhe. Abdullah Ali Mwinyi.....................................................Ndiyo
Mhe. Abdul-Hafar Idrissa Juma...........................................Ndiyo
Mhe. Abeid Ramadhani Ighondo........................................Ndiyo
Mhe. Abubakari Damian Asenga........................................Ndiyo
Mhe. Aeshi Khalfan Hilaly.....................................................Ndiyo
Mhe. Agnes Elias Hokororo..................................................Ndiyo
Mhe. Agnes Mathew Marwa...............................................Ndiyo
Mhe. Agnesta Lambert Kaiza...................................Hakuamua
Mhe. Ahmed Ally Salum.......................................................Ndiyo
Mhe. Ahmed Juma Ngwali..................................................Ndiyo
Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby...........................................Ndiyo
Mhe. Ahmed Yahya Abdulwakil...........................................Ndiyo
Mhe. Aida Joseph Khenani...............................................Hayupo
Mhe. Aleksia Asia Kamguna................................................Ndiyo

Mhe. Alexander Pastory Mnyeti.........................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Alfred James Kimea.........................................Ndiyo
Mhe. Ali Hassan Omar King.............................................Ndiyo
Mhe. Ali Juma Mohamed.................................................Ndiyo
Mhe. Ali Vuai Khamis......................................................Ndiyo
Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe................................Ndiyo
Mhe. Ally Mohamed Kassinge..........................................Ndiyo
Mhe. Aloyce Andrew Kwezi.............................................Ndiyo
Mhe. Amandus Julius Chinguile.......................................Ndiyo
Mhe. Ameir Abdalla Ameir..............................................Ndiyo
Mhe. Amina Ali Mzee.......................................................Ndiyo
Mhe. Amina Bakar Yussuf................................................Ndiyo
Mhe. Amina Daud Hassan................................................Ndiyo
Mhe. Amina Iddi Mabrouk...............................................Ndiyo
Mhe. Amour Khamis Mbarouk..........................................Ndiyo
Mhe. Anastazia James Wambura.....................................Ndiyo
Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest..........................Hakuamua
Mhe. Angelina Adam Malembeka................................Hayupo
Mhe. Anna Richard Lupembe..........................................Ndiyo
Mhe. Antipas Zeno Mgungusi..........................................Ndiyo
Mhe. Anton Albert Mwantona..........................................Ndiyo
Mhe. Asha Abdullah Juma...............................................Ndiyo

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

Mhe. Asia Abdukarimu Halamga.....................................Ndiyo
Mhe. Assa Nelson Makanika...........................................Ndiyo
Mhe. Asya Mwadini Mohammed............................ Hakuamua
Mhe. Asya Sharif Omar...................................................Ndiyo
Mhe. Augustine Vuma Holle...........................................Ndiyo
Mhe. Aysharose Ndogholi Mattembe...............................Ndiyo
Mhe. Bahati Keneth Ndingo............................................Ndiyo
Mhe. Bahati Khamis Kombo............................................Ndiyo
Mhe. Bakar Hamad Bakar...............................................Ndiyo
Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa...............................Ndiyo
Mhe. Benaya Liuka Kapinga............................................Ndiyo
Mhe. Benardeta Kasabago Mushashu..............................Ndiyo

Mhe. Boniphace Mwita Getere.........................................Ndiyo
Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo................................Ndiyo
Mhe. Boniventura Destery Kiswaga....................................Ndiyo
Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli...........................................Ndiyo
Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata.......................................Ndiyo
Mhe. Catherine Valentine Magige....................................Ndiyo
Mhe. Cecil David Mwambe...............................................Ndiyo
Mhe. Cecilia Daniel Paresso..................................... Hakuamua
Mhe. Charles John Poul Mwijage........................................Ndiyo
Mhe. Charles Muguta Kajege.............................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei........................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Christina Christopher Mnzava.............................Ndiyo
Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka ........................Ndiyo
Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza....................... Hakuamua
Mhe. Condester Michael Sichalwe....................................Ndiyo
Mhe. Constantine John Kanyasu.........................................Ndiyo
Mhe. Cosato David Chumi..................................................Ndiyo
Mhe. Daimu Iddi Mpakate.................................................Ndiyo
Mhe. Daniel Awack Tlemai.................................................Ndiyo
Mhe. Dkt. David Mathayo David........................................Ndiyo
Mhe. Deo Kasenyenda Sanga............................................Ndiyo
Mhe. Deodatus Philip Mwanyika........................................Ndiyo
Mhe. Deus Clement Sangu.................................................Ndiyo
Mhe. Dorothy George Kilave..............................................Ndiyo
Mhe. Esther Lukago Midimu...............................................Ndiyo
Mhe. Edward Olelekaita Kisau............................................Ndiyo
Mhe. Edwin Enosy Swalle...................................................Ndiyo
Mhe. Elibariki Immanuel Kingu............................................Ndiyo
Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai.....................................Ndiyo
Mhe. Emmanuel Peter Cherehani......................................Ndiyo
Mhe. Ester Amos Bulaya............................................Hakuamua
Mhe. Esther Edwin Malleko.................................................Ndiyo
Mhe. Esther Nicholas Matiko....................................Hakuamua
Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa.........................................Ndiyo
Mhe. Fakharia Shomar Khamis...........................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile.............................Ndiyo
Mhe. Felista Deogratius Njau....................................Hakuamua

Mhe. Festo Richard Sanga....................................................Ndiyo
Mhe. Flatei Gregory Massay.................................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Florence George Samizi.......................................Ndiyo
Mhe. Florent Laurent Kyombo..............................................Ndiyo
Mhe. Francis Isack Mtinga ...................................................Ndiyo
Mhe. Francis Kumba Ndulane..............................................Ndiyo
Mhe. Francis Leonard Mtega.................................................Ndiyo
Mhe. Fredrick Edward Lowassa............................................Ndiyo
Mhe. Furaha Ntengo Matondo..............................................Ndiyo
Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe.................................Ndiyo
Mhe. George Ranwell Mwenisongole.................................Ndiyo
Mhe. Ghati Zephania Chomete...........................................Ndiyo
Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi.....................................Ndiyo
Mhe. Haji Amour Haji ...........................................................Ndiyo
Mhe. Haji Makame Mlenge..................................................Ndiyo
Mhe. Halima James Mdee................................................Hayupo
Mhe. Hamida Mohamed Abdallah......................................Ndiyo
Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma.....................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla................................Ndiyo
Mhe. Hamisi Shabani Taletale..............................................Ndiyo
Mhe. Hasan Seleman Mtenga..............................................Ndiyo
Mhe. Hassan Zidadu Kungu..................................................Ndiyo
Mhe. Hawa Mchafu Chakoma............................................Ndiyo
Mhe. Hawa Subira Mwaifunga.................................Hakuamua
Mhe. Husna Juma Sekiboko.................................................Ndiyo
Mhe. Hussein Nassor Amar..................................................Ndiyo
Mhe. Innocent Edward Kalogeris..........................................Ndiyo
Mhe. Innocent Sebba Bilakwate.........................................Ndiyo
Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwelwe....................................Ndiyo
Mhe. Issa Ally Mchungahela................................................Ndiyo
Mhe. Issa Jumanne Mtemvu................................................Ndiyo
Mhe. Iddi Kassim Iddi..........................................................Ndiyo
Mhe. Jackson Gedion Kiswaga............................................Ndiyo
Mhe. Jacqueline Kainja Andrea...........................................Ndiyo
Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi.................................Ndiyo
Mhe. Jafari Wambura Chege...............................................Ndiyo
Mhe. Jaffar Sanya Jussa.......................................................Ndiyo

Mhe. Janejelly James Ntate ..............................................Ndiyo
Mhe. Janeth Elias Mahawanga...........................................Ndiyo
Mhe. Janeth Maurice Massaburi.......................................Ndiyo
Mhe. Jeremiah Mrimi Amsabi.............................................Ndiyo
Mhe. Jesca David Kishoa..........................................Hakuamua
Mhe. Jesca Jonathani Msambatavangu...........................Ndiyo
Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo.................................. Ndiyo
Mhe. John Marko Sallu........................................................Ndiyo
Mhe. Jonas Van Zeeland....................................................Ndiyo
Mhe. Jonas William Mbunda..............................................Ndiyo
Mhe. Joseph Anania Tadayo.............................................Ndiyo
Mhe. Joseph George Kakunda..........................................Ndiyo
Mhe. Joseph Kasheku Musukuma.....................................Ndiyo
Mhe. Joseph Michael Mkundi............................................Ndiyo
Mhe. Joseph Zacharius Kamonga.....................................Ndiyo
Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima..........................Ndiyo
Mhe. Josephat Sinkamba Kandege.................................. Ndiyo
Mhe. Josephine Johnson Genzabuke ...............................Ndiyo
Mhe. Josephine Tabitha Chagula..................................Hayupo
Mhe. Judith Salvio Kapinga................................................Ndiyo
Mhe. Juliana Daniel Shonza................................................Ndiyo
Mhe. Juliana Didas Masaburi...............................................Ndiyo
Mhe. Juma Hamad Omar...................................................Ndiyo
Mhe. Juma Othman Hija..........................................*(Hakusikika)*

**SPIKA:**

Mheshimiwa Juma Othman Hija.......................................Ndiyo

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

Mhe. Juma Usonge Hamad..............................................Ndiyo
Mhe. Jumanne Kibera Kishimba.......................................Ndiyo

**SPIKA:** Ngoja, subiri kidogo Katibu.

Waheshimiwa Wabunge, ukishaitika ndiyo, zima *microphone* yako ili mwingine anapowasha iwake kwa urahisi.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

Mhe. Justin Nyamoga……………………………………………………Ndiyo
Mhe. Kabula Enock Shitobelo……………………………………… Ndiyo
Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni…………………………………Ndiyo
Mhe. Kassim Hassan Haji ……………………………………………Ndiyo
Mhe. Katani Ahmadi Katani…………………………………………Ndiyo
Mhe. Kavejuru Eliadory Felix…………………………………………Ndiyo
Mhe. Kenneth Ernest Nollo……………………………………………Ndiyo
Mhe. Khadija Hassan Aboud…………………………………………Ndiyo
Mhe. Khadija Shaaban Taya…………………………………………Ndiyo
Mhe. Khalifa Mohamed Issa…………………………………Hakuamua
Mhe. Khalifa Salum Suleiman………………………………………Ndiyo
Mhe. Khamis Kassim Ali…………………………………………………Ndiyo
Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo……………………………Ndiyo
Mhe. Kunti Yusuph Majala……………………………………Hakuamua
Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo………………………………Ndiyo
Mhe. Latifa Khamis Juwakali…………………………………………Ndiyo
Mhe. Leah Jeremiah Komanya………………………………………Ndiyo
Mhe. Eng. Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho……………Ndiyo
Mhe. Livingstone Joseph Lusinde…………………………………Ndiyo
Mhe. Lucy John Sabu……………………………………………………Ndiyo
Mhe. Lucy Thomas Mayenga…………………………………………Ndiyo
Mhe. Luhaga Joelson Mpina…………………………………………Ndiyo
Mhe. Maida Hamad Abdallah………………………………………Ndiyo
Mhe. Maimuna Ahmad Pathan………………………………………Ndiyo
Mhe. Maimuna Salum Mtanda………………………………………Ndiyo
Mhe. Margaret Simwanza Sitta………………………………………Ndiyo
Mhe. Mariam Nassoro Kisangi………………………………………Ndiyo
Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri………………………………………Ndiyo
Mhe. Mariam Madalu Nyoka…………………………………………Ndiyo
Mhe. Martha Festo Mariki………………………………………………Ndiyo
Mhe. Martha Nehemia Gwau…………………………………………Ndiyo

Mhe. Maryam Azan Mwinyi.................................................Ndiyo
Mhe. Maryam Omar Said...........................................Hakuamua
Mhe. Masache Njelu Kasaka............................................... Ndiyo
Mhe. Maulid Saleh Ali.........................................................Ndiyo
Mhe. Mbarouk Juma Khatib...............................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani..............................Ndiyo
Mhe. Michael Mwita Kembaki.............................................Ndiyo
Mhe. Michael Costantino Mwakamo.................................Ndiyo
Mhe. Minza Simon Mjika.....................................................Ndiyo
Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu.............................................Ndiyo
Mhe. Mohamed Abdulrahman Mwinyi...............................Ndiyo
Mhe. Mohamed Lujuo Monni...............................................Ndiyo
Mhe. Mohamed Said Issa.........................................Hakuamua
Mhe. Mohamed Suleiman Omar.........................................Ndiyo
Mhe. Mohammed Maulid Ali...............................................Ndiyo
Mhe. Mrisho Mashaka Gambo.............................................Ndiyo
Mhe. Muharami Shabani Mkenge.......................................Ndiyo
Mhe. Munde Tambwe Abdallah........................................Ndiyo
Mhe. Munira Mustapha Khatib...........................................Ndiyo
Mhe. Mussa Hassan Mussa.................................................Ndiyo
Mhe. Mussa Ramadhani Sima.............................................Ndiyo
Mhe. Mustafa Mwinyikondo Rajab......................................Ndiyo
Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge...............................Ndiyo
Mhe. Mwanakhamis Kassim Said.........................................Ndiyo
Mhe. Mwantakaje Haji Juma...............................................Ndiyo
Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis.........................................Ndiyo
Mhe. Mwantumu Dau Haji...................................................Ndiyo
Mhe. Mwantumu Mzamili Zodo..........................................Ndiyo
Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara........................................Ndiyo
Mhe. Nancy Hassan Nyalusi................................................Ndiyo
Mhe. Nashon William Bidyanguze.......................................Ndiyo
Mhe. Ndaisaba George Ruhoro.........................................Ndiyo
Mhe. Neema Gelard Mwandabila......................................Ndiyo
Mhe. Neema Kichiki Lugangira...........................................Ndiyo
Mhe. Neema William Mgaya...............................................Ndiyo
Mhe. Ng'wasi Damas Kamani..........................................Hayupo
Mhe. Nicholaus George Ngassa........................................Ndiyo

Mhe. Nicodemas Henry Maganga......................................Ndiyo
Mhe. Njalu Daudi Silanga...................................................Ndiyo
Mhe. Noah Lemburis Saputu Mollel......................................Ndiyo
Mhe. Norah Waziri Mzeru....................................................Ndiyo
Mhe. Nusrat Shaaban Hanje.....................................Hakuamua
Mhe. Oliver Daniel Semuguruka...........................................Ndiyo
Mhe. Omar Ali Omar.................................................Hakuamua
Mhe. Omar Issa Kombo.........................................................Ndiyo
Mhe. Oran Manase Njeza......................................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.....................................Ndiyo
Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi..............................Ndiyo
Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi........................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato.........................................Ndiyo
Mhe. Phillipo Augustino Mulugo...............................*(Hakusikika)*
Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya.............................................Ndiyo

**SPIKA:**

Mheshimiwa Phillipo Mulugo.................................................Ndiyo

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya...............................................Ndiyo
Mhe. Priscus Jacob Tarimo...................................................Ndiyo
Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan...............................Ndiyo
Mhe. Rashid Abdallah Shangazi..........................................Ndiyo
Mhe. Rashid Abdalla Rashid...................................................Ndiyo
Mhe. Ravia Idarus Faina........................................................Ndiyo
Mhe. Regina Ndege Qwaray................................................Ndiyo
Mhe. Rehema Juma Migilla..................................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Ritta Enespher Kabati..........................................Ndiyo
Mhe. Riziki Said Lulida...........................................................Ndiyo
Mhe. Robert Chacha Maboto.............................................Ndiyo
Mhe. Rose Cyprian Tweve....................................................Ndiyo
Mhe. Rose Vicent Busiga......................................................Ndiyo
Mhe. Saada Monsour Hussein..............................................Ndiyo
Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe..........................................Ndiyo
Mhe. Salim Alaudin Hasham................................................Ndiyo

Mhe. Salim Mussa Omar........................................................Ndiyo
Mhe. Salome Wycliffe Makamba..................................Hakuamua
Mhe. Salum Mohammed Shaafi...................................Hakuamua
Mhe. Eng. Samweli Xaday Hhayuma....................................Ndiyo
Mhe. Santiel Eric Kirumba......................................................Ndiyo
Mhe. Sebastian Simon Kapufi................................................Ndiyo
Mhe. Seif Salim Seif......................................................Hakuamua
Mhe. Shally Josepha Raymond..............................................Ndiyo
Mhe. Shamsia Azizi Mtamba...............................................Hayupo
Mhe. Shanif Mansoor Jamal...................................................Ndiyo
Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya..........................................Ndiyo
Mhe. Silyvestry Francis Koka................................................Hayupo
Mhe. Simai Hassan Sadiki......................................................Ndiyo
Mhe. Simon Songe Lusengekile..............................................Ndiyo
Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda............................Hakuamua
Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo..............................Ndiyo
Mhe. Soud Mohammed Jumah..............................................Ndiyo
Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula......................................Ndiyo
Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya........................................Ndiyo
Mhe. Stella Simon Fiyao.....................................................Hayupo
Mhe. Subira Khamis Mgalu....................................................Ndiyo
Mhe. Suleiman Haroub Suleiman..........................................Ndiyo
Mhe. Suma Ikenda Fyandomo.........................................Ndiyo
Mhe. Sylvia Francis Sigula......................................................Ndiyo
Mhe. Tabasam Hamis Mwagao.............................................Ndiyo
Mhe. Tarimba Gulam Abbas..................................................Ndiyo
Mhe. Taska Restituta Mbogo.................................................Ndiyo
Mhe. Tauhida Cassian Gallos................................................Ndiyo
Mhe. Tecla Mohamedi Ungele..............................................Ndiyo
Mhe. Dkt. Thea Medard Ntara..........................................Ndiyo
Mhe. Timotheo Paul Mnzava..................................................Ndiyo
Mhe. Toufiq Salim Turky.........................................................Ndiyo
Mhe. Tumaini Bryceson Magessa..........................................Ndiyo
Mhe. Tunza Issa Malapo..............................................Hakuamua
Mhe. Twaha Ally Mpembenwe..............................................Ndiyo
Mhe. Ussi Salum Pondeza......................................................Ndiyo
Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo.......................................Ndiyo

Mhe. Venant Daud Protas....................................................Ndiyo
Mhe. Wanu Hafidh Ameir..................................................Hayupo
Mhe. Yahaya Omary Massare.............................................Ndiyo
Mhe. Yahya Ali Khamis.........................................................Ndiyo
Mhe. Yahya Ally Mhata.......................................................Ndiyo
Mhe. Yustina Arcadius Rahhi...............................................Ndiyo
Mhe. Zacharia Paulo Issaay..................................................Ndiyo
Mhe. Zahor Mohammed Haji..............................................Ndiyo
Mhe. Zainab Athman Katimba.............................................Ndiyo
Mhe. Zaytun Seif Swai..........................................................Ndiyo
Mhe. Zubeida Khamis Shaib.................................................Ndiyo
Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka.......................................Ndiyo
Mhe. Zuena Athumani Bushiri..............................................Ndiyo
Mhe. Zulfa Mmaka Omar......................................................Ndiyo

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumehitimisha zoezi la kupiga kura. Sasa zinahesabiwa. Kura zinaenda kuhesabiwa ili tufahamu ni ngapi kura za ndiyo, hapana, ambao hawakuamua na ambao hawapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna baadhi ya Wabunge ambao wametajwa hapa ambao hawapo kupiga kura lakini ofisi tuna taarifa nao, wana changamoto mbalimbali kila mmojawapo, lakini siyo lazima kusema ni changamoto gani. Kwa hiyo, ofisi ina taarifa nao wale ambao tunazo taarifa zao. Tunasubiri majibu, mtupe dakika chache.

*Katibu wa Bunge (Ndg. Nenelwa Mwihambi, ndc) Alirejea Bungeni*

**MATOKEO YA KURA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa matokeo hapa. Ngoja nisimame kwanza kuyatangaza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, idadi ya Wabunge waliokuwepo Bungeni ni 380. Idadi ya Wabunge ambao

hawakuwepo Bungeni ni 11. Idadi ya waliopiga kura ni 379. Hiyo kura moja ya kufikia 380 ni kura yangu kwa sababu hamjanisikia hapa nikipiga kura. Sababu ni moja tu, kwamba kanuni zetu zimeweka utaratibu mzuri, Spika hapigi kura kwa sababu kura zikifungana yeye ana kura ya uamuzi. Ana kura ya uamuzi watu wasije wakasema sasa Spika mwenyewe hakubali bajeti. Kanuni ya 92 fasili ya (2). "Spika wakati amekalia Kiti cha Spika hatakuwa na kura ya kawaida, bali atakuwa na kura ya uamuzi endapo kura za ndiyo na siyo zitalingana." Kwa hiyo, kura yangu inapigwa katika mazingira hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kura za Hapana, sifuri. Kwa hiyo, hakuna Mbunge aliyesema hapana. Kura ambazo hazikuamua ama za Wabunge ambao hawakuamua ni kura 23; na kura za ndiyo ni 356. *(Makofi)*

Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, uamuzi wa Bunge leo ni kwamba Bajeti ya Serikali kwa maana ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yamepita kwa asilimia 94. Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, huo ndiyo uamuzi wa Bunge. Nitazungumza machache baadaye tuendelee na ratiba iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya Shilingi 41,480,579,818,000 kwa matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 kutumia fedha hizo zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo.** ***(A Bill for an Act to apply a sum of 41,480,579,818,000 Shillings out of the Consolidated Fund to the service of the year ending of 30th day of June, 2023 to appropriate the supply granted for that year, to authorized the reallocation of setting appropriations into provide for matters connected with those purpose)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI,** ***ndc*** **- KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2022** ***(The Appropriation Bill 2022)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya Shilingi 41,480,579,818,000 kwa matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo** ***(A Bill for an Act to apply a***

***sum of 41,480,579,818,000 Shillings out of the Consolidated Fund to the service of the year ending on the 30th day of June, 2023 to appropriate the supply granted for that year, to authorized their allocation of certain appropriations and to provide for matters connected with those purposes)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu wa Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2022 *(The Appropriation Bill)* umesomwa kwa hatua zote katika kipindi chetu hiki. Sasa niwahoji Waheshimiwa Wabunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2022 (The Appropriation Bill 2022) ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Haya wote mmeafiki. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge Sheria hii imepitishwa kwa hatua zote kama ambavyo tunatakiwa kufanya kisheria, lakini pia kikanuni na kwa hivyo, tutampelekea Mheshimiwa Rais ili aweze kusaini ili sasa matumizi haya yaanze kwa mwaka wa fedha mpya unaokuja. Kwa hiyo, kwa upande wetu tumemaliza zoezi hili.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii sasa kuipongeza Serikali kwa sababu mlileta Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na sasa Bunge limefanya kwa sehemu yake na mmepitishiwa au mmeidhinishiwa na Bunge. Kwa hiyo, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pongezi hizi siyo za bure kwa sababu Katiba yetu Ibara ya 90 kama tungeikataa, wote tunajua nini kingefuata. Kwa hiyo, ni halali yao kabisa

kupongezwa kwamba Serikali imepitishiwa bajeti yake na Bunge. *(Makofi)*

Pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana Mawaziri wote kwa ushirikiano mliouonyesha kwa kipindi chote hiki kwa Waheshimiwa Wabunge. Mmeonyesha ushirikiano kwenye ngazo ya kisekta tulipokuwa tunajadili, mmesikiliza ushauri wa Wabunge, mmesikiliza hoja zao kutoka kwa watu wanaowawakilisha na baada ya kuzisikiliza mmefanya marekebisho hapa na pale, kuongezea zile barabara ambazo zilikuwa hazimo, kuongeza visima ambavyo vilikuwa havimo, kuongeza mabwawa ambayo yalikuwa hayamo, kwa hiyo tunawashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa ambao mmewapa Waheshimiwa Wabunge, kwenye ngazi ya Kamati lakini pia ngazi ya Bunge tunawashukuru sana kwa kushirikiano huo.

Waheshimiwa Wabunge, pia niwapongeze sana Wabunge wote pamoja na Wenyeviti wetu, kwa kazi nzuri sana mlioifanya, kipindi chote hiki ambacho ni muda mrefu kidogo tumekuwa hapa mmefanya kazi kwa bidii sana kwenye ngazi ya Kamati, lakini hata humu Bungeni mmefanya kazi ya kuisimamia Serikali ilipoleta taarifa kuhusu mambo yaliyofanyika mwaka wa fedha huu tunaomalizia na sasa walipoleta makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaokuja mmetoa ushauri, kwa hiyo mmefanya kazi nzuri sana, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mmetoa mawazo mazuri ambayo Serikali wameyaelewa na wameyafanyia kazi. Kwa hiyo ninawapongeza sana na hasa kwenye hii Bajeti Kuu mmemsikia hapa Mheshimiwa Waziri, akijibu hoja zenu japokuwa hajaweza kuzijibu hoja zote, lakini amejibu hoja nyingi, baadhi ya hoja hizo zikiwa ni sehemu ya yale ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyasema, mmeyawakilisha kwa niaba ya wananchi ambao mnawawakilisha. Kwa hiyo

mmefanya kazi nzuri ameyasema hapa sina haja ya kuyarejea.

Waheshimiwa Wabunge, pengine kubwa lingine sio kwamba ndio kubwa katika hayo yote, lakini ambalo lillisemwa pengine na Wabunge wengi sana ni la asilimia 10 la mikopo. Kwa hiyo hilo jambo mojawapo na hilo linaonyesha namna ambavyo Serikali inasikiliza ushauri wenu Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo nawapongeza sana kwa kazi kubwa mlioifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa pongezi hizo pia nichukue fursa hii kumpongeza sana, Katibu wetu wa Bunge na timu yake yote kwa namna wanavyofanya kazi. *(Makofi)*

Haya ahsanteni sana, sasa hapa kwa sababu haruhusiwa kusimama lakini alitaka kusimama ili apokee shukrani hizi nilizozitoa. Kwa hiyo tunakushukuru sana Katibu pamoja na timu yako yote kwa kazi nzuri mlioifanya katika kipindi chote hiki ambacho tulikuwa tukitazama makadirio ya mapato na matumizi kwa Serikali.

Vile vile, nami niwashukuru wasaidizi wangu Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, namshukuru Mheshimiwa Azzan Zungu, ahsante sana kwa kazi nzuri kwa kipindi chote hiki. Mheshimiwa Najma Giga ahsante sana, Mwenyekiti wa Bunge huyu, ahsante sana. Pia Mwenyekiti David Kihenzile, ahsante sana kwa kazi nzuri, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu hapa nimewataja Mawaziri, Manaibu Mawaziri na watendaji wenu muwapelekee salamu, tunawashukuru sana kwa ushirikiano wao walioutoa. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu zoezi hili Waheshimiwa Wabunge tumemaliza kwa sehemu, kwa sababu bado tutakuwa na kazi ya kuitazama sasa ile sheria ambayo inatafsiri yale ambayo

Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitueleza hapa, tutakuwa na hiyo kazi wiki ijayo. Kwa hiyo ile juhudi kazi, mawazo mazuri tuliyoyaonyesha, sasa ni kazi yetu kuanza kuangalia vile vifungu vimo mle, vimetoka ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema vinatoka au bado vimo, kwa hiyo ni kazi yetu kuyatazama hayo pia ili tuweze kukamilisha sasa zoezi zima la bajeti.

Nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu kama Wabunge wengine mlivyozungumza bajeti hii ina mambo mengi makubwa na mazuri ambayo yanawagusa wananchi moja kwa moja. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusikiliza kilio cha wananchi hapa na pale na ni dhahiri hayawezi kufanyika yote ndani ya mwaka mmoja kwa sababu haya tunayoyapitisha ni kwa ajili ya Mwaka wa Fedha 2022/2023. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hata haya sisi ni mashahidi kwamba ahadi zilizotolewa kwenye bajeti hii ni nyingi na tunaona nia njema ya Serikali ya kushughulika na changamoto za wananchi. Kwa hiyo mambo mengi yamesemwa na mimi sitaki kuyarejea hayo, lakini nampongeza sana sana. Hapa Mheshimiwa Rais tunampongeza kwa sababu kama Naibu Waziri alivyosema amesikiliza kilio cha wananchi huko anakopita, akaona awapunguzie mzigo kwa sehemu kubwa sana. Kwa hiyo miradi inayoenda kutekelezwa, inaenda kuwagusa wananchi wote. Kwa hivyo kama Bunge tunampongeza na tunamtakia kila la kheri katika utekelezaji wa ahadi hizi ambazo zimetolewa katika Bajeti hii ya 2022/2023. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hapa kuna mambo machache pengine ya msisitizo, kwanza ni suala la elimu hasa kuhusu kikokotoo, kwa nini suala la elimu? Mheshimiwa Waziri amelieleza jambo hili vizuri sana na sote Wabunge tumemwelewa na ndio maana tumepiga kura ya ndiyo,

kwamba ipite maana yake kikokotoo si kibaya kama watu wanavyokielezea, kwa hivyo, watumishi wakipata elimu ya kutosha kuhusu hiki kikokotoo, yale malalamiko hata kama hayataisha, lakini yatapungua. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri utazame utaratibu mzuri kabisa wa kutoa elimu ukishirikiana na Vyama vya Wafanyakazi ili na wao waende wakatoe elimu kwa wale watu ambao wako chini yao, itarahisisha sana kupunguza maswali waliyonayo kuhusu kikokotoo. Kwa sababu ulivyotoa maelezo hapa tumeiona nia njema ya Serikali lakini pia nia njema ya Vyama vya Wafanyakazi kwamba tufike mahali tukutane katikati.

Kwa hiyo ni jambo zuri mkiwapelekea elimu hii watumishi wa umma ili waelewe na kama wana jambo sasa la kushauri baada ya hapo, basi muupokee ushauri kama ambavyo sasa hivi mmesema na mimi pia ni shahidi, Serikali ya Awamu ya Sita inawasikiliza wananchi. Kwa hiyo kama watakuwa na jambo wakati mkitoa hii elimu, watakapowaeleza hayo mambo ambayo bado wanayo basi mtaweza kuyafanyia kazi hata kama si sasa lakini taratibu ili tufike mahali ambapo wafanyakazi wanafanya kazi kwa amani na wastaafu pia wanastaafu kwa amani, wakijua mambo yao yako vizuri na tunawatakia kila la kheri katika hilo zoezi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na sisi tuchukue hilo jukumu la kuwaelimisha wananchi, kama na sisi tunahitaji elimu ya ziada, basi tuseme, kama tunahitaji elimu ya ziara kuhusu kikokotoo, tuseme ili tukawaeleze wananchi hiki kikokotoo kinamaanisha nini na tuwaambie nini wananchi na kama wana maswali tuweze kumletea Mheshimiwa Waziri ili waone kama kuna mahali ambapo bado kuna changamoto, lakini nawapongeza sana kwa hatua mliyofikia na kwa utayari mlionao, naamini Wabunge watakapoleta hoja za wananchi hoja za watumishi ambazo bado zinahusu kikokotoo, naamini mtazisiliza na mtazifanyia kazi. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge ni muhimu sana kuwasikiliza wananchi wetu ili tuiletee Serikali, tuishauri na iweze kuchukua hatua.

Jambo lingine ambalo limesisitizwa hapa na ningependa kulisisitiza ni kuhusu mishahara katika kupunguza matumizi ya Serikali, wale watumishi ambao wanatarajiwa kupunguziwa mishahara kwa sababu wameondolewa kwenye hizo nafasi na kwa sababu hili jambo ndio limepitishwa leo hapa na Bunge, halijapitishwa kwa namna ile ya kwamba sasa watu wakapunguziwe misharaha Hapana, watu wakapunguziwe mishahara baaada ya kufuata utaratibu uliowekwa kisheria. *(Makofi)*

Kwa hiyo pamoja na kwamba Bunge linaunga mkono juhudi za Serikali kupunguza matumizi, tunataka sheria ifuatwe, kanuni zifuatwe. Kwa hiyo watumishi wale wanaoondolewa kwenye nafasi zao na tunasisitiza watumishi kwa sababu ziko nafasi ambazo ni za kisiasa ambazo utaratibu wake ni mwingine, lakini kwa wale ambao ni watumishi, kuondolewa kwenye nafasi utaratibu ufuatwe ili tunapozungumza kuhusu kupunguza matumizi, basi yapunguzwe matumizi kwa namna ya utaratibu ule ambao tumejiwekea kisheria na kikanuni pia. Kwa hiyo, tunaamini kwamba hili mtalifanyia kazi, Waheshimiwa Wabunge hili halihusu Wizara ya Fedha, wala haihusu Wizara yoyote ni lenu Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

La mwisho, kabla sijawatangazia wageni walioko hapa Bungeni, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu leo ndio tunahitimisha ndio maana hili linawahusu Serikali kwa ujumla. Waheshimiwa Wabunge, wanapochangia hoja hapa Bungeni kila Mbunge angetamani atajwe ili wananchi wake wajue kwamba alikuwa amesema jambo fulani, kwa hivyo Waheshimiwa Mawaziri kama unalazimika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wake aidha uzijibu kwa ujumla kama umeamua kuwataja na umeona una muda wataje wote kwenye hoja hizo. *(Makofi)*

Nasema hivi kwa sababu ukiwataja wachache, wale ambao na wengine walichangia hoja hizo hizo wanaona kama hivi mimi sikusikika au mchango wangu umeonwa vipi. Kwa hiyo kwa ajili ya kuweka ule usawa, Waziri akiamua kutaja Wabunge waliochangia, awataje Wabunge wote na Waziri akiamua hatawataja ajibu hoja zilizoko mezani. *(Makofi)*

Hilo litatuweka sehemu nzuri ili mwananchi kule asiwe anauliza, sasa mbona wewe umesema barabara, lakini inavyoonekana barabara hiyo Serikali haijasikia, hatujamsikia waziri akisema, lakini ukijibu kwa ujumla kwamba Waheshimiwa Wabunge barabara za maeneo yao, basi hata Mbunge atasema mmemsikia Waziri amesema tumezungumzia barabara za maeneo yetu. Kwa hilo nalo Waheshimiwa Mawaziri niwaombe sana ili humu ndani Wabunge wasiwe wanaona mie mbona huwa sitajwi jamani, nasahaulika au mchango wangu hausikilizwi.

Waheshimiwa Wabunge, michango yenu yote Wabunge, Mawaziri wanaisikiliza lakini kwenye kutaja inaweza ikawa mtihani. Sasa huo mtihani ndiyo tunajaribu kuuweka sana hapa ili Mbunge asijisikie vibaya kwamba yeye mchango wako pengine waziri hakuusikia na ndio maana tuna utaratibu wa Serikali kujibu kwa maandisha hoja zote za Wabunge. Hata hivyo, yale maandishi ni tofauti na ukisema hapa, kwa hivyo ni muhimu sana tuzingatie hilo ili Wabunge wote wajione wako sawa hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge, sasa linalo tangazo hapa la wageni ambao tuko nao jioni hii hapa Bungeni:-

Kwanza ni wageni walioko Jukwaa la Spika, tunao wageni wa Bunge ambao ni viongozi kutoka *CRDB* Benki, kwanza yupo Abdulmajid Mussa Nsekela ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Benki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, lakini ameongozana na ndugu Boma Raballa ambaye ni Afisa Mkuu wa Biashara. Yupo pia ndugu Bruce Mwile ambaye ni Afisa Mkuu Mwendeshaji wa Benki. Yupo pia ndugu Musiba Mugaya ambaye ni Afisa Mkuu wa Fedha. Yupo pia ndugu Prosper Nambaya ambaye ni Mkurugenzi wa Wateja Wakubwa. Yupo pia ndugu Boniventure Paul ambaye ni Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Kati na yupo pia ndugu Wilson Mzava ambaye ni Mkuu wa Bima. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Uongozi huu wa *CRDB* wameambatana na Menejimenti nzima ya *CRDB* na wote msimame sasa kwa pamoja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa hapo sijajua kama Grace ameingia au hajaingia, Grace yupo jamani? Haya jamani naambiwa Grace yuko ofisini anatengeneza mambo yakae sawa. Ahsanteni sana Wageni wetu kutoka *CRDB,* karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao wameingia mchana huu, wote wasimame kwa pamoja. Karibuni sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu jambo moja, kesho saa kumi na mbili asubuhi matembezi yataanzia geti kubwa la hapa Bungeni kuelekea Jamhuri *Stadium* Wabunge wote mnakaribishwa na ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.10 Jioni Bunge Liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 27Juni, 2022, Saa Tatu Asubuhi)*